**OORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Kamal Basha Pandu | Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo. |
| 2.Mhe. Ali Mzee Ali | Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais. |
| 3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe. |
| 4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge. |
| 5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | Kiongozi wa Upinzani/“Waziri Kivuli”–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni. |
| 6.Mhe. Haji Omar Kheri | Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu. |
| 7.Mhe. Soud Yussuf Mgeni | Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Wawi. |
| 8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani. |
| 9.Mhe. Hamza Hassan Juma | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura. |
| 10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais. |

| | |
|---|---|
| 11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe. |
| 12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki | MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais. |
| 13. Mhe. Machano Othman Said | Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni. |
| 14.Mhe. Samia Suluhu Hassan | MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake. |
| 15.Mhe. Burhan Saadat Haji | MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni. |
| 16.Mhe. Asha Abdalla Juma | MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais. |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi. |
| 18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry | MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais. |
| 19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki. |
| 20.Mhe. Zainab Omar Moh'd | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake. |
| 21.Mhe. Idi Pandu Hassan | Mwanasheria Mkuu wa Serikali. |
| 22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Mzee Ali Ussi | Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani. |
| 24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari | Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu. |
| 25.Mhe. Khamis Jabir Makame | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni. |
| 26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole. |
| 27.Mhe. Tafana Kassim Mzee | Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini. |
| 28.Mhe. Omar Ali Shehe | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Chake-Chake. |
| 29.Mhe. Zakiya Omar Juma | "Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake. |
| 30.Mhe. Abass Juma Muhunzi | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Chambani. |
| 31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga. |
| 32.Mhe. Haji Faki Shaali | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Jimbo la Mkanyageni. |
| 33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake. |
| 34.Mhe. Hamad Masoud Hamad | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole. |

| | |
|---|---|
| 35.Mhe. Said Ali Mbarouk | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Gando. |
| 36.Mhe. Rashid Seif Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani. |
| 37.Mhe. Mohamed Ali Salim | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani. |
| 38.Mhe. Asaa Othman Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete. |
| 39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake. |
| 40.Mhe. Najma Khalfan Juma | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake. |
| 41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile. |
| 42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. |
| 43.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini. |
| 44.Mhe. Ali Denge Makame | Jimbo la Amani. |
| 45.Mhe. Ali Haji Ali | Jimbo la Mkwajuni. |
| 46.Mhe. Ali Moh’d Bakari | Jimbo la Tumbe. |
| 47.Mhe. Ali Suleiman Ali | Jimbo la Kwahani. |
| 48.Mhe. Ame Mati Wadi | Jimbo la Matemwe. |

| | |
|---|---|
| 49.Mhe. Ame Ussi Juma | Jimbo la Nungwi. |
| 50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake. |
| 51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila | Jimbo la Fuoni. |
| 52.Mhe. Ashura Abeid Faraji | Nafasi za Wanawake. |
| 53.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Nafasi za Wanawake. |
| 54.Mhe. Dadi Faki Dadi | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba. |
| 55.Mhe. Fatma Abdalla Tamim | Nafasi za Wanawake. |
| 56.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | Jimbo la Mji Mkongwe. |
| 57.Mhe. Haji Mkema Haji | Jimbo la Koani. |
| 58.Mhe. Hasnuu Moh’d Haji | Uteuzi wa Rais. |
| 59.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani. |
| 60.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba. |
| 61.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope. |
| 62.Mhe. Mkongwe Nassor Juma | Nafasi za Wanawake. |
| 63.Mhe. Moh’d Kombo Mkanga | Jimbo la Chwaka. |
| 64.Mhe. Mustafa Moh’d Ibrahim | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja. |
| 65.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake. |
| 66.Mhe. Omar Ali Jadi | Jimbo la Kojani. |
| 67.Mhe. Pembe Juma Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja. |
| 68.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu | Jimbo la Muyuni. |

| | |
|---|---|
| 69.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake. |
| 70.Mhe. Said Khelef Ali | Jimbo la Bumbwini. |
| 71.Mhe. Salim Abdulla Hamad | Jimbo la Mtambwe. |
| 72.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni. |
| 73.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni. |
| 74.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde. |
| 75.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Nafasi za Wanawake. |
| 76.Mhe. Zahra Ali Hamad | Nafasi za Wanawake. |

**Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**.

**Kikao cha Tatu – Tarehe 23 Januari, 2009**

*(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)*

**Dua**

*Mhe. Spika,(Mhe. Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua.*

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii):** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hati ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Moh'd Ali Salim (Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali):** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

## MASWALI NA MAJIBU

**Nam. 55**

**Chombo cha Kuweka Utaratibu wa Kutoa Leseni za Uvuvi wa Bahari Kuu**

**Mhe. Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Kny: Mhe. Anaclet Thobias Makungila)** – Aliuliza:-

Moja kati ya kero za Muungano wakati huu ni suala la uvuvi wa bahari kuu kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ile ya Muungano. Miongoni mwa kazi zinazohusu uvuvi huo ni utoaji wa leseni za uvuvi wa bahari kuu, makusanyo ya ada za leseni hizo na uwekaji viwango vya bei na utaratibu wa biashara ya uuzaji wa leseni kati ya serikali mbili hizo.

Je serikali mbili hizi zimefikia hatua gani ya kutafuta hatma ya kupata chombo kitakachosimamia utaratibu mzima wa utoaji wa leseni za uvuvi wa bahari kuu na viwango sahihi vya bei za leseni vinavyostahiki kutozwa na Tanzania.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri Kiongozi)** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 55 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kabisa miongoni mwa kero za Muungano ilikuwa ni suala la uundwaji wa mamlaka na mgawanyo wa mapato yatayopatikana katika uvuvi wa Bahari Kuu. Suala hili limekuwa ni miongoni mwa agenda zilizojadiliwa na kupatiwa ufumbuzi katika vikao vya kujadili kero za Muungano, vilivyoendeshwa chini ya usimamizi wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambapo kwa sasa vikao hivyo vinaendeshwa chini ya uenyekiti wa Mhe. Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, napenda kutoa taarifa kwamba serikali zetu mbili hivi sasa zimefikia hatua za mwisho za uandaaji wa kuanzisha Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu ya Muungano ambayo Makao Makuu yake yatakuwepo Zanzibar. Hivi sasa wako katika maandalizi angalau kuanzisha Afisi ya muda kabla ya kujenga ile ya kudumu. Kadhalika ni mategemeo yetu kuwa mamlaka itakuwa tayari kufanya kazi zake rasmi ndani ya mwaka huu wa 2008/2009.

Mhe. Spika, miongoni mwa hatua zilizopatiwa ufumbuzi katika uendeshaji wa mamlaka hii ni pamoja na mgawanyo wa mapato, muundo wa Kamati ya Usimamizi na Kamati ya Ushauri, ukamilishaji wa kanuni pamoja na uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na Msaidizi ambao kwa mujibu wa sheria watateuliwa na Mhe.Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, mamlaka ndiyo itayosimamia utaratibu mzima wa utoaji wa leseni za Uvuvi na Bahari Kuu na viwango sahihi vya bei za leseni zitatangazwa na mamlaka hiyo.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba nimuulize Mhe. Waziri, kwa kuwa huu uvuvi wa bahari kuu unaendelea, angalau kwa mwaka huu uliopita.

(a) Je, Tanzania imekusanya kiasi gani na Zanzibar imepata fungu gani katika makusanyo hayo?

(b) Kwa vile tume hii inayoongozwa na Makamu wa Rais sasa hivi kama ni Mwenyekiti, kushughulikia kero za Muungano. Je, ni masuala gani yaliyotatuliwa na vipi wananchi wanapewa taarifa kuhusu hayo masuala ambayo yametatuliwa katika migogoro hii ya Muungano?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri Kiongozi):** Mhe. Spika, kwanza napenda kumjulisha kwamba swali lililoulizwa lilikuwa ni uundwaji wa mamlaka ya bahari kuu na hatua zilizofikia. Kwa hivyo, nadhani kwa sababu wako katika hatua ya mwanzo, yaani ndio kwanza wanaanza siwezi kuzungumzia mapato kwa sasa hivi kama alivyouliza.

Pia ameulizia vile vile suala jipya juu ya mikutano inayofanyika ya ushirikiano, pamoja na kushughulikia kero za Muungano. Kwa muhtasari, hili moja nililolitaja limeshafikia hatua nzuri sasa hivi. La pili ambalo limefikia hatua nzuri ni kuiwezesha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kufanya kazi zake hapa Zanzibar. Mengine hivi sasa ndio yako katika mchakato wa kufanyiwa ufumbuzi ili tatizo hili liondoke.

**Mhe. Spika:** Je, utaratibu wa kuwajulisha wananchi?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri Kiongozi):** Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunitanabahisha.

Mhe. Spika, kila tunapomaliza mkutano wetu juu ya kero za Muungano Mhe. Makamu wa Rais pamoja na Mhe. Waziri Kiongozi, huwa wanakutana na waandishi wa habari kutoa taarifa tumezungumza mambo gani katika suala lile. Wanapokuwa hawakupata nafasi hiyo, basi mawaziri wanaohusika huwa wanakutana na waandishi wa habari kutoa taarifa hizo na zinakuwemo kwenye magazeti pamoja na vyombo vya habari.

**Mhe. Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi nitowe maelezo ya ziada pale alipomalizia Mhe. Ramadhan Abdallah Shaaban. Namshukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake mazuri sana ya ufasaha.

Njia ya pili ambayo tunaitumia katika kuwapasha habari wananchi, juu ya hatua mbali mbali zinazofikiwa katika mazungumzo haya ya kutatua kero za Muungano. Moja ni hiyo aliyoieleza kwamba mawaziri na watendaji mbali mbali wa taasisi hizo zinazozungumza mara zinapomaliza vikao vyao huwa wanatoa taarifa kwa waandishi wa habari.

Pili Mhe. Spika, ni kwa kupitia katika Baraza lako tukufu, kama alivyofanya waziri kwa kupitia Baraza hili. Maana katika kila kikao hapa huwa yanaulizwa

maswali haya yanayohusu Muungano. Kwa hivyo, serikali kwa kupitia mawaziri wake imekuwa ikitoa maelezo hayo.

Pia, kila Bajeti ya Waziri Kiongozi, basi taarifa hiyo huwa inatolewa kwa kupitia Bajeti ya Afisi ya Waziri Kiongozi pamoja na wizara nyengine zinazosimamia na taasisi zinazohusiana na masuala ya Muungano. Hata mijadala ya Bajeti kwa ujumla imekuwa ikizungumzia masuala hayo ya namna gani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikizishughulikia au kusimamia kero hizo za Muungano. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, pamoja na majibu ya mawaziri, lakini hawaoni kwamba utaratibu wa kuleta taarifa za vikao hivyo hauna utaratibu maalum, ndio maana kunakuja maswali kama haya?

Ikiwa hivyo ndivyo wanaonaje kwamba kwa kuwa suala hili lilianzishwa rasmi kwenye Bunge, kwa hivyo baada ya vikao ingekuwa inakuja taarifa rasmi ambayo itafuatiwa baadae kama kuna maswali au mijadala.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri Kiongozi):** Mhe. Spika, hili alilolitoa Mhe. Mwakilishi ni ombi, ambalo bila shaka itabidi lizingatiwe na baadae ndio apate maelekezo.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Ahsante Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza linalohusiana na masuala ya uvuvi wa bahari kuu. Mhe. Spika, hivi karibuni kama miezi miwili hivi iliyopita, waziri wa Muungano anayeshughulikia uvuvi, nafikiria ni Mhe. John Pombe Makufuli, alinakiliwa na vyombo vya habari akisema kwamba meli zinazovua katika bahari kuu, zitalazimika kupiga ripoti katika bandari tatu, akazitaja bandari ya Dar es Salaam, Mtwara na Tanga. Bandari ya Zanzibar haikutajwa kama meli zinazovua zitalazimika kupiga ripoti pale.

Pia akasema kwamba samaki ambao hawawahitaji watalazimika kuuzwa katika soko la ndani. Je, Mhe. Spika, swali langu ni kwamba uwamuzi huu wa Mhe. Makufuli wa kutoitaja bandari ya Zanzibar ni katika utatuzi wa hii kero ya Muungano katika suala hili la bahari kuu. Je, serikali inasemaje katika suala hili na kuhusiana na hili?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri Kiongozi):** Mhe. Spika, aliyozungumza ni kweli lilitokea na limetokea katika hatua za mwanzo za kuanzisha mamlaka ya bahari kuu, ambayo kusema kweli ndio tuko katika kuianzisha. Inaelekea kwamba hatua ile ilikuja baada ya

Mheshimiwa kuona kwamba hii sheria haijaanza kufanya kazi vizuri. Maana hii sheria ndio kwanza iko katika kutengenezewa *regulation* sasa hivi, ambapo hizo *regulation* zitatoa uamuzi wa mambo haya yote namna ya kufanyika. Tayari imeshaundwa *Steering Committee* ambayo inatengeneza hizo *regulation* ambazo zinatakiwa kutumika katika masuala haya.

Lakini hata hivyo serikali zote mbili zinalishughulikia. Nadhani marekebisho yatafanyika kama kawaida. Ahsante sana.

**Nam. 30**

**Kosa la Kuua Bila ya Kukusudia**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu** - Aliuliza:-

Kwa kuwa kuua kwa mujibu wa sheria ni kosa la jinai.

(a) Je, kuua bila ya kukusudia ni kosa la aina gani.

(b) Kosa la kuua bila ya kukusudia ni lipi, na vipi litadhihirika (litathibitika) kama kosa lilotendwa ni la kuua bila ya kukusudia.

(c) Ni jambo gani litalo iridhisha Mahakama kuona kuwa kweli mtuhumiwa kaua bila ya kukusudia.

(d) Kwa kuwa mtu anayeua bila ya kukusudia kwa tafsiri ni mtu aliyeua akiwa hana dhamira ya kuua, je nini adhabu/hukumu ya mtu aliyeua bila ya kukusudia.

(e) Ni nani ataehesabika kaua bila ya kukusudia kati/baina ya mwendawazimu, na mlevi.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 30 la kitaalamu kabisa kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, kabla sijamjibu natanguliza maelezo yafuatayo.

Mhe. Spika, katika hali yoyote mtu mmoja kumuua mwengine ni mauaji. Hata hivyo hii haina maana kwamba mauaji ya aina zote ni makosa, kwani kuna baadhi ya mauaji yanakubalika kisheria, hasa pale inapotokezea katika mazingira yafuatayo:-

1. Kutekeleza sheria za nchi kama vile kutekeleza hukumu ya Mahakama au wakati wa kudhibiti wahalifu.
2. Au wakati wa kutumia nguvu kujitetea/kujilinda mtu yeye mwenyewe au mwenziwe au kulinda mali.
3. Katika tukio la ajali ambayo mhusika hakuwa mzembe katika ajali hiyo.

Baada ya utangulizi huo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 30 lenye vifungu (a), (b), (c), (d) na (e) kama ifuatavyo:-

(a) Kosa la kuua bila ya kukusudia ni kosa la jinai ambalo limetajwa katika Sheria ya Kanuni ya Adhabu Nam. 6/04 ya Zanzibar katika kifungu cha 195. Kifungu hicho kinaeleza kwamba mtu yeyote atakayefanya kitendo kinyume na Sheria au atakayeacha kutenda kitendo cha kisheria na kusababisha kifo cha mtu mwengine atakuwa ameua bila ya kukusudia.

(b) Kuna mambo kadhaa yakidhihirika ndiyo hubainika kwamba kosa hili ni la kuua bila ya kukusudia, mambo yenyewe ni:-

- (i) Kuwepo na mtu aliyeuliwa na mtu mwengine.
- (ii) Iwe ameuliwa kwa kufanyiwa kitendo kilichokuwa kinyume na sheria au ameacha kufanyiwa kitendo kilichokuwa halali kisheria.
- (iii) Kifo hicho kiwe kimetokea ndani ya mwaka mmoja na siku moja tangu alipofanyiwa kitendo hicho au alipokosa kufanyiwa kitendo hicho.
- (iv) Mambo hayo yote idhibitishwe kuwa muuaji asiwe na nia ovu ya kuua, yaani (*maliceaforethought*).

(c) Mambo ambayo Mahkama inayazingatia kuona kuwa kweli mtuhumiwa kaua bila ya kukusudia ni kama vile:-

1. Pale mtu anapokosa kijidhibiti kwa hasira/wasiwasi/woga na kushindwa kutumia busara katika kutoa maamuzi hasa anapofanyiwa vitendo visivyo vya kisheria. Mfano kutukanwa au kudhalilishwa au kufumania mke/mume wake na mengineyo.
2. Mtu anapojitetea/kujilinda dhidi ya mtu mwengine mfano kwenye ugomvi. Iwapo watu watakuwa wanapigana na mmoja wao akafa.
3. Mtu anapolinda mali na ikatokezea kuua wakati wa kulinda mali hiyo.

4. Mtu anapofanya kitendo ambacho katika hali ya mtu wa kawaida hawezi kufikiria kwamba kitendo hicho kinaweza kusababisha kifo mfano mzazi au mwalimu kumchapa mtoto na baadae mtoto yule akafa.
5. Mtu anapoacha kufanya kitendo ambacho analazimika kukifanya kisheria kwa ajili ya kunusuru maisha au afya ya mtu, mfano mtu anapoacha kumpa dawa mgonjwa au mzazi anapoacha kumpa chakula mtoto na hatimaye kusababisha kifo.

(d) Kwa mujibu wa sheria ya Jinai Nam. 6/04 katika kifungu 198 ni kwamba adhabu/hukumu ya mtu aliyeua bila ya kukusudia ni kupewa kuanzia onyo hadi kifungo cha maisha.

(e) Mwendawazimu na mlevi wote watakuwa wameuwa bila ya kukusudia kama Mahkama itakavyoona inafaa na ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo:-

Kisheria kila mtu anaakili timamu pale anapofanya makosa na ni jukumu la mshtakiwa kuithibitishia Mahkama kuwa yeye ni mwendawazimu alipokuwa anafanya kosa. Katika hili itambidi mshtakiwa aioneshe Mahkama kwamba:-

- Alikuwa na maradhi ya akili wakati alipokuwa akifanya kosa. au

- Kutokana na maradhi hayo hakuwa akijua anachokifanya.

Kwa hivyo Mahkama itayazingatia maelezo yote ya utetezi na pia yale ya upande wa Mashtaka katika kuthibitisha kosa. Ikijidhihirisha kwamba kosa limethibitishwa dhidi ya mshtakiwa, na ikiwa mshtakiwa ataishawishi Mahkama kwamba yeye ni mwendawazimu, basi atatiwa hatiani kama ushahidi ulivyowasilishwa na atapelekwa hospitali ya wagonjwa wa akili, ambapo kwa hapa Zanzibar tunatumia Kidongo Chekundu.

Kuhusu mlevi kimahkama hana utetezi mbele ya Mahkama mpaka pale atakapoithibitishia kuwa:-

- Wakati wa tukio hakujua kuwa anachokifanya.
- Vile vile ulevi ule ameupata bila ya ridhaa yake na ulitokana na hadaa au uzembe wa mtu mwengine.

Baada ya kuzingatia hayo na Mahkama ikijiridhisha kuwa mlevi yule hakujua alichokuwa anakifanya au athari ya kile anachokifanya na pia

ulevi ule haukuwa kwa hiari yake. Mahkama itamtia hatiani kwa kuua bila ya kukusudia.

**Nam. 2**

**Pesa za Matumizi Mengineyo "Other Charges" (Oc)**
**Kwa Taasisi za Pemba**

**Mhe. Ali Suleiman Ali: (Kny: Mhe. Ali Abdalla Ali)** - Aliuliza:-

Imeshapita zaidi ya miezi mitatu sasa, taasisi zilizoko Pemba haziingizwi fedha za matumizi mengineyo (*Other Charges*), jambo ambalo linazorotesha utendaji wa kazi za taasisi hizo na kuleta usumbufu mkubwa kwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, pale ambapo Kamati hizi zinapokuwa Pemba.

(a) Ni sababu zipi za msingi zinazopelekea kukosekana kwa pesa hizo kwa kipindi cha miezi mitatu au zaidi.

(b) Je, Mhe. Waziri, huoni kuwa tatizo hili ni miongoni mwa matatizo yanayozorotesha utendaji wa taasisi hizi.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 2 (a) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kutoa ufafanuzi katika swali lililoulizwa. Kutokana na taarifa tulizonazo, ni kuchelewa kupelekwa fedha Pemba na sio kutopelekwa fedha hizo Pemba. Naomba ifahamike hivyo, kwamba sio kama hazipelekwi kabisa hapana. Tatizo lipo kweli la kuchelewa kupelekwa fedha Pemba.

(a) Mhe. Spika, baada ya kupata taarifa kutoka kwa Maafisa Wadhamini waliopo Pemba kuhusiana na upelekaji huo wa fedha Pemba, Wizara ya Fedha na Uchumi ilikaa na kufuatilia jinsi ya kulitatua tatizo hili. Kwa kipindi cha miezi mitatu ya robo ya pili ya mwaka wa fedha 2008/09 (Oktoba/Disemba, 2008) Wizara ya Fedha ilipeleka fedha Pemba kwa uharaka zaidi, na iliamua kufanya hivyo wakati ikiendelea kufanya mawasiliano ya karibu na Watendaji Wakuu wa Wizara zote katika kulitafutia ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo.

Mhe. Spika, naomba kutoa mifano ya baadhi ya taasisi za Pemba ambayo ni kithibitisho cha uingizwaji wa fedha kuanzia July, 2008 hadi sasa kama ifuatavyo:-

- Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ imetengewa kwenye Bajeti ya Tshs. 147,050,000 na hadi sasa zimeshapelekwa Pemba Tshs. 72,879,000 ambazo ni sawa na asilimia 50 ya Bajeti yote.

- Ofisi ya Rais Ikulu Pemba imetengewa katika Bajeti ya 155,549,000 na hadi sasa wameshapokea Pemba Shs. 82,045,788 ambazo ni sawa na asilimia 53 ya Bajeti yote.

- Wizara ya Fedha na Uchumi Pemba imetengewa katika Bajeti ya 347,425,000 na hadi sasa imepata Shs. 175,538,042 ambazo ni sawa na asilimia 51 ya Bajeti yote.

- Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira Pemba imetengewa Bajeti ya Shs. 1,366,523,000 na hadi sasa imeingiziwa Shs. 666,795,114 ambazo ni sawa na asilimia 49 ya Bajeti yote.

- Mkoa wa Kusini Pemba umetengewa Bajeti ya Shs.773,570,000 na hadi sasa imepata Shs. 370,584,344 ambazo ni sawa na asilimia 48 ya Bajeti yote.

- Mkoa wa Kaskazini Pemba umetengewa Bajeti ya Shs. 672,810,000 na hadi sasa imepata Shs. 322,768,623 ambazo ni sawa na asilimia 48 ya Bajeti yote.

Mhe. Spika, tunakiri kwamba ni kweli kulikuwa na tatizo la upatikanaji wa fedha katika kipindi cha miezi mitatu ya mwanzo, lakini hili halikuwa tatizo la Pemba peke yake, hili lilikuwa ni tatizo la serikali nzima Unguja na Pemba.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa swali lilikuwa ni *Other Charges* ambazo sio sehemu ya mishahara, na jibu lake kubwa lilikuwa ni kwa jumla.

a) Je, hizi *Other Charges* anatupa taarifa gani kuhusiana na utaratibu uliopo sasa hivi?

b) Kwa huko nyuma kabla ya kipindi hiki cha Bajeti iliyopita ilikuwa utaratibu ni kupelekwa fedha moja kwa moja. Kwa mujibu wa taarifa iliyoko kwa kupitia Kamati ufanisi mkubwa ulikuwepo. Lakini baada

ya mabadiliko yaliyotokea ya kuanza kupitia hapa na sio kupelekwa moja kwa moja ndio utaratibu huo ukakosekana. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba kubadilisha utaratibu ni kuelekea kwenye ufanisi na sio kupunguza ufanisi, anatueleza nini kuhusu suala hili?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, hizi fedha nilizozitaja ni pamoja na *Other Charges*.

a) Nimesema kuanzia Julai mpaka sasa hivi, pesa zilizopelekwa Pemba, kwa hivyo hii *figure* niliyoitaja ni pamoja na *Other Charges*, sikuweza kutoa ufafanuzi tu labda mishahara ngapi na *Other Charges* ngapi. Lakini hizi ni pesa zote pamoja na *Other Charges.* Kama nilivyosema kuwa sio kuwa hazikupelekwa hapana, zilichelewa tu kupelekwa.

b) Kweli zamani tulikuwa na utaratibu wa kupeleka fedha moja kwa moja Pemba. Baadae hapa kati kutokana na maombi ya Makatibu Wakuu kwamba wao ndio wasimamizi, kwa hivyo inabidi zipitie kwao kama kuziona tu lakini hawazigusi, sasa ikawa zinachelewa. Kwa hivyo, tukapata malalamiko, sasa tumesharudi kwenye ule ule utaalamu wa zamani. Tayari tumo katika mipango kamilisha, ule mtandao wetu wa *Intergrated Financial Management System* (yaani IFMS), ambapo utaratibu ule utawezesha moja kwa moja kwa njia ya mitandao tu fedha zile kupelekwa Pemba moja kwa moja, hizo taratibu tunazikamilisha.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, katika jibu mama la Mhe. Waziri alitupa mifano, ili kutuonesha kwamba fedha zimepelekwa na alianza na vikosi na Afisi ya Rais kama kawaida.

Swali langu ni kwamba kutokana na umuhimu katika jamii Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tulikuwa tunaona nayo ina umuhimu mkubwa wa kuona ni kiasi gani imeingiziwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atutajie kiwango ambacho japo kwa hiyo asilimia kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kwamba kama nilivyosema kuwa hii ni baadhi ya mifano tu. Hatukuichagua kama ni Afisi ya Rais Ikulu Pemba au Vikosi. Kulikuwa na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, labda pengine hakuisikia. Mkoa wa Kusini Pemba na Mkoa wa Kaskazini.

Wizara ambazo hatukuzitaja kwa kweli hizo Wizara ni nyeti mno, na kama fedha hazikwenda, basi ujuwe kazi zinalala. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali sina *figure* kamili, lakini kama haziendi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba ujuwe ni hatari. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kama *Other Charges* haziendi pia ni hatari zaidi. Kwa hivyo, huko mambo ni mazuri zaidi, sikuzipata zile *figure* tu.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Ahsante Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, wakati Mhe. Waziri alipokuwa akifanya majumuisho katika hotuba ya bajeti ya wizara yake iliyopita, aliahidi kwamba tatizo hili ambalo linazungumzwa leo lingepatiwa ufumbuzi. Bahati mbaya inaonekana hapo katikati hakupata wasaa wa kulipatia ufumbuzi bado linajadiliwa leo kwenye kikao hiki cha Januari.

Wakati uliopita aliliahidi Baraza lakini ahadi yake haikukamilika. Kwa hivyo, katika kikao hiki kuhusu suala hili Baraza analiahidi nini, ili tatizo hili liwe historia.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, mwaka wa fedha haujamaliza tunaendelea nao na utekelezaji ni jambo moja, wakati unapotekeleza ndio unabaini matatizo, kwa sababu kama hutekelezi siku zote matatizo huyaoni. Kwa hivyo, ninamuomba sana Mhe. Mjumbe atupe fursa na sisi tumechukua ahadi suala hilo tutalirekebisha.

**Nam. 85**

**Uuzaji wa Chumvi isiyo na Madini Joto**

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Salmin Awadh Salmin)** – Aliuliza:-

Sheria ya Vyakula, Madawa na Vipodozi ya mwaka 2006 Zanzibar, inahusu udhibiti wa uuzaji, utengenezaji na usambazaji wa vyakula, madawa, dawa za miti shamba, vipodozi na vifaa vya tiba. Kwa kuwa hivi sasa kuna wafanyabiashara wengi Zanzibar katika kisiwa cha Pemba wanouza chumvi isiyo na madini joto.

(a) Je, Mhe. Waziri wizara yako haihusiki na udhibiti wa uuzaji wa chumvi ya aina hii ?

(b) Kama inahusika, ni kwa nini inaachia wafanyabiashara waendelee kuuza chumvi isiyokuwa na madini joto ?

(c) Kutumia chumvi isiyokuwa na madini joto kunaleta madhara gani kwa binaadamu ?

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 85 lenye vifungu vya (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa sheria ya vyakula, madawa na vipodozi ya mwaka 2006, Zanzibar inahusu udhibiti wa uuzaji, utengenezaji na usambazaji wa vyakula, madawa, dawa za miti shamba vipodozi na vifaa vya tiba.

Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kwa kushirikiana na Kitengo cha Lishe cha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii zinahusika na kuhakikisha kuwa chumvi inayozalishwa na Jumuiya ya Wazalishaji Chumvi Zanzibar (*AZASPO*) ina madini joto ya kutosha kwa kiwango kinachotakiwa.

Katika utekelezaji wa jambo hilo Bodi inashirikiana kwa karibu na Jumuiya ya Wazalishaji Chumvi.

Mhe. Spika, kutokana na mashirikiano ya Bodi na Jumuiya ya *AZASPO* mzunguko wa chumvi isiyokuwa na madini joto umepungua kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Spika, madhara yanayoweza kujitokeza kwa kutumia chumvi isiyokuwa na madini joto ni maradhi ya tezi ya shingo (*Goiter*). Hata hivyo maradhi hayo ni machache katika kanda za pwani kutokana na wananchi kutumia vitoweo kutoka baharini kama vile samaki, pweza, ngisi na kadhalika ambao wanaongeza kiasi kikubwa madini joto.

**Nam. 17**

**Uimarishaji wa Vyuo vya Elimu ya Juu Zanzibar**

**Mhe. Ali Denge Makame -** Aliuliza:-

Hivi sasa kumekuwa na Vyuo vingi vya Elimu ya Juu hapa Zanzibar vinavyotoa fani mbali mbali ikiwemo Elimu, Sheria na Biashara na serikali imekuwa ikisomesha wanafunzi wengi katika vyuo hivi.

(a) Je, wizara inavisaidia vipi vyuo hivi hasa katika kuhakikisha kwamba inalipa madeni yake yote inayodaiwa na vyuo hivi, ili kuvijengea uwezo mkubwa wa kifedha vyuo hivi na hivyo kuviimarisha zaidi ?

(b) Serikali inachukua jitihada gani katika kuhakikisha kwamba wanafunzi wa Zanzibar wote wanasomeshwa katika vyuo vya ndani ya Zanzibar, kozi zote zinazofundishwa katika vyuo hivyo na kuacha tabia ya kuwasomesha huko Tanzania Bara katika vyuo kama vile CBE na IFM, ambapo gharama za chuo na maisha kwa wanafunzi wetu huwa ni za juu sana ?

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba wanafunzi wengi wa Zanzibar wanasoma katika vyuo vinne vya Elimu ya Juu viliopo hapa Zanzibar. Vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Chuo Kikuu cha Zanzibar, Chuo cha Elimu Kishiriki cha Chukwani na Chuo cha Fedha, Chwaka.

Wengi wa wanafunzi wa Zanzibar wanaosoma katika vyuo hivi hugharimiwa na Mfuko wa Mikopo ya Elimu ya Juu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na baadhi wanagharimiwa na Mfuko wa Mikopo ya Elimu ya Juu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania.

(a) Wizara ina mashirikiano mazuri na vyuo vya elimu ya juu vya hapa Zanzibar sio tu katika kulipa ada za wanafunzi wanaogharimiwa na Serikali ya Zanzibar, bali pia katika kufuatilia maendeleo yao. Kwa hivi sasa, wizara haina deni lolote la ada za wanafunzi kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Chuo cha elimu Kishiriki cha Chukwani na Chuo cha Fedha cha Chwaka. Hata hivyo ni kweli wizara inayo deni la malipo ya ada kwa Chuo Kikuu cha Zanzibar kiliopo Tunguu.

Mhe. Spika, kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi tunaopeleka katika chuo hiki kila mwaka, uwezo wetu wa kuwalipia wanafunzi wote kwa wakati mmoja sio mzuri. Hata hivyo juhudi zimechukuliwa kupunguza madeni ya chuo kadri tunavyoingiziwa fedha.

Kwa mwaka wa fedha 2008/09, jumla ya Shilingi 200,000,000/= zimelipwa kwa chuo hiki na tunakabiliwa na deni la Shilingi 498,980,000/=. Juhudi zinachukuliwa kulipa deni hilo hatua kwa hatua na uongozi wa Chuo Kikuu cha Zanzibar pamoja na wanafunzi wamekuwa wakitupa ushirikiano mzuri katika suala la kumalizia deni hilo.

Malengo yetu ni kuwapatia wanafunzi wetu wengi zaidi nafasi za kusoma huku tukipunguza deni hilo hatua kwa hatua badala ya kuwapatia nafasi za masomo wanafunzi wachache ambao tutaweza kuwalipia gharama zao za masomo.

(b) Hivi sasa wanafunzi wetu wengi wanasoma katika taasisi za elimu ya juu zilizopo Zanzibar kwa fani za masomo zinazofundishwa na vyuo vya ndani. Hata hivyo, tunawajibika kuwapeleka baadhi ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu vya Tanzania Bara na hata nje ya nchi kwa fani za masomo zisizofundishwa katika vyuo vya hapa Zanzibar.

**Mhe. Haji Mkema Haji:** Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri amezungumza kuwa wizara yake inadaiwa na Chuo Kikuu cha Tunguu. Mhe. Spika, mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Koani ambapo chuo hicho kimo kwenye jimbo langu.

Mkuu wa chuo amenilalamikia kuhusu deni hilo ambalo ni la muda mrefu na uendeshaji wa chuo unategemea ada za wanafunzi. Kwa hivyo, ni lini watahakikisha angalau wanalipa nusu ya deni hilo, ili chuo hicho kisishindwe kufanyakazi zake pamoja na kutoa huduma za taaluma hapa kwetu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, hivi leo ambapo tunazungumza hapa tayari tumeshapeleka *cheque* ya shilingi milioni 130 katika hatua za kupunguza deni hilo *(Makofi)*.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nichukue fursa hii kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na serikali kwa jumla kutokana na maelezo mazuri ambayo yameelezwa hivi punde. Kwa sababu wizara imejitahidi kuhakikisha kwamba haina madeni katika chuo vyote isipokuwa Chuo Kikuu cha Zanzibar Tunguu.

Swali langu lipo hapa kwa kuwa suala la deni bado lipo katika Chuo hicho na wanafunzi wetu mara nyingi hupata adha ya kutokamilisha mitihani yao au kutishwa kufanya mitihani yao. Lakini ninajua kwamba mazungumzo ndio njia ya busara na kuleta mafanikio. Je, wizara inachukua hatua gani pamoja na deni hilo kulipwa kidogo kidogo, ili kuhakikisha kuwa inapofika kipindi cha mitihani au majaribio wanafunzi wale wafanye bila ya matatizo ?

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, wizara inachukua kila aina ya jitihada ya kuhakikisha kwamba malipo haya yanakamilika na wanafunzi hawafukuzwi chuoni. Mimi mwenyewe binafsi nimeshazungumza na Mkuu wa Chuo wakati wa mahafali na ndio maana

tumeanza kuchukua jitihada za kupunguza madeni haya. Sambamba na hilo tunahakikisha kwamba wanafunzi watafanya mitihani yao kama kawaida.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Mhe. Spika ahsante sana. Kwa kuwa hili suala la deni ni jambo ambalo linajulikana sana katika wizara. Hivyo, kwa nini wizara inawaachia wanafunzi wakateseka katika kutishwa karibu na mitihani kwamba watafanya au hawafanyi ?

Kutokana na hali hiyo kwa nini wasichukue hatua za dharura za kulipa kabla ya muda, ili ule utulivu wa wanafunzi katika kusoma kwenye vyuo vikuu vyetu ukapatikana, badala ya kuwa kila ikifika mitihani wanafunzi wale kujitayarisha na mitihani wanajitayarisha kupeleka madai yao kuhusu malipo ?

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu mama ni kwamba tumekuwa tukichukua hatua mbali mbali za kuhakikisha tunafuta madeni. Vile vile nilisema mwaka jana tulilipa zaidi ya shilingi milioni 200 kwa hatua hiyo ya kupunguza madeni na kuhakikisha wanafunzi hawapati usumbufu katika kipindi cha mitihani.

Mhe. Spika, jitihada kubwa inachukuliwa na wizara pamoja na serikali katika kuhakikisha kuyamaliza kabisa madeni haya. Ndio maana Chuo pekee ambacho kinatudai ni Tunguu na hii inaonesha jitihada kubwa ambayo imefanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kuhakikisha inalipa madeni yake.

Pamoja na hayo kama nilivyosema hili halitegemei kila wakati inapokaribia kufanya mitihani ndio wizara inachukua hatua za kulipa, lakini wakati wote wizara iko tayari na inayaona madeni yake na inafuatilia na inachukua jitihada za kupunguza madeni hayo.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, kwa kweli majibu yako sawa, lakini napenda kuchukua fursa hii kwa kuliweka sawa zaidi.

Kwanza napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wanafunzi wote wa Zanzibar wanaosoma vyuo vikuu kwa kuwa na utulivu pamoja na usikivu. Ninawapongeza sana kwa sababu kwa kipindi chote hiki ambapo kumetokea matatizo upande mmoja vijana wetu walionesha nidhamu ya hali ya juu kuhusu masuala ya ulipaji wa masomo yao.
Pili napenda kumshakikishia Mhe. Mjumbe kwamba bajeti zetu tunazopanda bilashaka zinawekwa na kiwango fulani, lakini mwamko wa wanafunzi kusoma umekuwa ni mkubwa. Kwa mfano, kama tutaweka bajeti ya shilingi milioni 800, tungeweza kuwasomesha wanafunzi 100 au 200.

Lakini linalojitokeza ni wenye sifa wanakuwa wengi na wote tumewaahidi kwamba kila mwenye sifa za kwenda chuo kikuu tutampeleka. Kwa hivyo, matokeo yake wanafunzi wanakwenda vyuo vikuu ni wengi sana kiasi ambacho wanapita ile bajeti ambayo tumeweka.

Kwa maana hiyo, hii inatusaidia kutokana na tunavyojifunza kuongezeka kwa wanafunzi kila mwaka. Ndio maana huwa tunaomba fedha za ziada Wizara ya Fedha na Uchumi na tunashukuru pale ambapo tunapoziomba huwa tunapatiwa.

Mhe. Spika, isionekane labda hawa ni wanafunzi pengine ni idadi maalum walikuwa ndio wameandaliwa bajeti yao maalum, lakini hatuwezi kuwalipia. Kweli ni tumeifanyia bajeti, lakini idadi ya wanafunzi tuliyoifanyia bajeti ilikuwa ni 200 na waliokwenda vyuo vikuu ni 400 na wala hatuwezi kuwazuia kwa sababu ni wakati wao hivi sasa kusoma.

## Nam. 41

## Ujenzi wa Jengo la Wizara Usiokamilika

**Mhe. Hasnuu Moh'd Haji –** Aliuliza:-

Katika Afisi ya Mawasiliano Pemba kuna jengo ambalo limejengwa muda mrefu sasa, ukiliangalia linafanana na gofu.

(a) Je, ni muda gani tokea lijengwe ?

(b) Huoni kwamba ujenzi kama huo usiokamilika ni matumizi mabaya ya fedha za wananchi zinazokusanywa kwa kulipa kodi ?

(c) Utaratibu kama huu utamalizika lini kwa kuanza ujenzi bila kumaliza?

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi –** Alijibu:-

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima. Kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 41 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba katika Afisi ya Mawasiliano Pemba kuna jengo ambalo limekusudiwa kuwa Idara ya Barabara, ambalo limekuwepo kwa muda mrefu bila ya kukamilika mpaka kuonekana kama ni gofu. Katika kipindi chote hicho wizara yangu ilishindwa kuendeleza ujenzi huo kutokana na ukosefu wa fedha.

Hata hivyo, wizara imeandaa mpango wa kulikamilisha jengo hilo kupitia Mradi wa Barabara za Kusini Pemba unafadhiliwa na *NORAD*. Jengo hili linakusudiwa kuwa ni afisi ya wataalamu wanaosimamia mradi huo. Baada ya kukamilika mradi huo, jengo hilo litakuwa ni Afisi ya Mhandisi Mkaazi wa Barabara kisiwani Pemba.

**Nam. 36**

**Uwekezaji kwenye Ufukwe wa Mchangamle Kusini Unguja**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu –** Aliuliza:-

Tarehe 18/12/2006 Serikali ya Mkoa wa Kusini Unguja iliwaandikia barua Mkuu wa Wilaya Kusini Unguja, Sheha wa Shehia ya Dimbani, Sheha wa Shehia ya Muyuni C na Mkurugenzi Idara ya Ardhi na Usajili kwa kumbukumbu Nam. MKS/U/M.120/4/VOL.11/83 KUH: ENEO LA MCHANGAMLE, kwamba Serikali ya Mkoa wa Kusini Unguja ilipokea agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar la kutaka eneo la Mchangamle liachwe bila ya kuharibiwa au kufanywa kitu chochote hadi atakapopatikana mwekezaji mwafaka wa kuwekeza eneo hilo.

Kwa kuwa jukumu la kutafuta mwekezaji mwafaka amepewa Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji na hivi sasa ujenzi mkubwa wa hoteli kubwa ya kitalii umeshamiri na unaendelea kwa kasi.

(a) Wananchi wa Shehia za Dimbani na Muyuni C wangependa kujua mwekezaji wa mradi huo ni nani ?

(b) Je, hizi ni zile juhudi za Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji katika kumtafuta mwekezaji mwafaka au ni mwekezaji mwengine aliyekuja kuwekeza kinyume na maelekezo na maagizo ya jukumu alilopewa Waziri wa Utalii ?

(c) Kwa kuwa serikali iliwataka wananchi wa shehia hizo kuwa na mashirikiano ya pamoja kulidhibiti eneo hilo kwa faida ya vijiji vyao. Je, wananchi wa vijiji hivyo watafaidika vipi na mradi huo wakati tangu mapema ilionekana hali ya wananchi wa vijiji hivyo kudhulumiwa kwa baadhi yao kutokulipwa fidia ya vipando vyao au kulipwa pungufu ya malipo halisi?

(d) Je, wananchi wangapi wamelipwa fidia ya vipando vyao na kiasi gani kimelipwa kwa kila mmoja wao ?

**Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 36 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

Eneo la Ukanda wa Mchangamle awali lilikuwa eneo la serikali, baada ya shamba hilo kutaifishwa. Baadaye serikali ililikata shamba hilo eka na kuwapa wananchi mbali mbali na wengi wao walikuwa kutoka sehemu ya Muyuni C na Kizimkazi Dimbani. Wizara yangu inafahamu kwamba serikali iliagiza eneo hilo lidhibitiwe mpaka wapatikane wawekezaji watakaojenga hoteli ya daraja la juu.

Ujenzi unaofanywa hivi sasa ambao Mhe. Mjumbe ameutaja unafanywa na mwekezaji kutoka Mauritius, ambaye anajenga hoteli ya daraja la nyota tano, ambao utakuwa na jumla ya vyumba 100 na kila chumba kikiwa na huduma zote muhimu pamoja na mabwawa ya kuogelea. Maamuzi ya kuupeleka mradi huo ni agizo la serikali. Baada ya utangulizi huo sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake.

(a) Mwekezaji wa mradi huo ni Kampuni ya *Hotel and Property Development Limited*, ambayo kama nilivyosema kwenye utangulizi wenyewe ni kutoka Mauritius.

(b) Kama nilivyosema kwenye maelezo yangu mwekezaji huyo kapewa eneo hilo kutokana na agizo la serikali. Pamoja na kuwepo kwa agizo hilo la serikali mwekezaji huyo alifuata taratibu zote za kuwekeza nchi sambamba na kupata kibali cha mradi na ujenzi katika Kituo cha Uwekezaji (*ZIPA*).

(c) Kwa vile mradi huo ni mkubwa na unategemewa kuchangia kiasi kikubwa kwenye mapato ya serikali. Wananchi hao wakiwa ni sehemu ya jamii ya Wazanzibari watafaidika kwa kuongezeka huko kwa pato la serikali kutokana na mradi huo.

Faida nyengine ambazo vijiji hivyo vitapata ni pamoja na kushirikiana na wenye mradi kwa kuweka huduma na mambo mengine ya maendeleo kwenye vijiji hivyo. Hili linawezekana kama ilivyowezekana kwenye sehemu nyengine za nchi yetu kama vile Kiwengwa, Pwani Mchangani ambapo wenye hoteli hukaa pamoja na wanaviji na kukubaliana juu ya huduma mbali mbali zitakazowekwa kama majengo ya huduma, biashara ambazo wanakijiji watafanya na hoteli pamoja na kuwapatia wanavijiji ajira ambazo wanaziweza.

(d) Jumla ya wananchi 24 wamelipwa fidia na walilipwa shilingi 42,320,000/-. Utaratibu wa kulipa fidia uliotumika ni kwamba wananchi hao waliitwa na kuelezwa juu ya suala hili, baadaye chini ya usimamizi wa Sheha walileta orodha ya miti pamoja na mazao yao. Thamani ya miti na mazao hayo ilitiwa kwa kufuata ushauri na vigezo vya Idara ya Misitu.

Hata hivyo, viwango vilivyopendekezwa na misitu viliongezwa. Kwa mfano, mapendekezo ya Idara ya Misitu ilikuwa ni kiasi shilingi 5,000/- kwa kila mnazi mkubwa, lakini mwekezaji alilipa shilingi 20,000/- kwa kila mnazi wa aina hiyo.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Spika ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuulizwa swali la nyongeza.

Mhe. Spika, maelezo yote yaliyoelezwa hapa kwa upande wangu sina pingamizi nayo na hasa nikizingatia kwamba tunapoambiwa mwekezaji anapokuja katika maeneo yetu tunayoishi, huwa kuna matarajio mema wananchi hupata. Kwa mfano, barabara, maji, umeme pamoja na ajira ambacho ndio kilio kikubwa kwa wananchi wetu.

Katika jibu la Mhe. Naibu Waziri ameeleza kwamba wananchi wengi wamefaidika katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu wakiwemo wananchi wa Kiwengwa, Pwani Mchangani, Matemwe, Nungwi pamoja na sehemu nyengine.

Je, Mhe. Waziri kwa kuwa hivi sasa kuna adha kubwa ya wananchi wa Kiwengwa ambao wananchi hawa baada ya kupatikana wawekezaji wengi wa mahoteli mazuri ambapo wananchi wanapata kufanya kazi zao tofauti. Lakini walikewa huduma ya maji ambapo maji hayo hawakuchimba wao, isipokuwa ni maji ambayo Mwenyezi Mungu ameyajaalia kwenye sehemu ya pako kubwa ambayo yanatiririka na wananchi wanafaidika na maji hayo.

Kwa kuwa wawekezaji wanayafunga maji hayo na hivi sasa kumekuwa na vita vikubwa sana mpaka wananchi kufikishwa vyombo vya sheria na hata kulazwa ndani. Je, Mhe. Waziri ana wito gani kwa wawekezaji wa ukanga wa Kiwengwa kuhakikisha kuwa hii baraka ya maji ni ya nchi yetu na wala hayatoki kwao, ili wananchi wa maeneo yale wasidhulumiwe na wala wasipate shida ya kutezwa kwa kufungwa maji kwa makusudi.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, nilifikiri unataka useme tatizo ambalo limetokea Kiwengwa lisitokee Mchangamle. Ni vyema ukaliandika swali la msingi.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Zanzibar hivi sasa uchumi wake sehemu kubwa unategemea utalii, lakini wananchi wa Zanzibar wanahitaji ardhi kwa ajili ya matumizi. Vile vile sekta ya utalii imekuwa sana badala ya kuwa serikali kufanya utaratibu wa fidia.

Hivyo, serikali haioni ni vyema ikawakaribisha wawekezaji kwa njia mbili ya ubia ama bei ya soko na ardhi ilivyo sasa, ili kuondoa tatizo la kuona wananchi wanachukuliwa ardhi yao bila ya kupata faida kubwa ?

**Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Spika, utalii unaweza kuwa katika hali zote kwa ubia au mgeni peke yake. Isipokuwa mzalendo ambaye anayo ardhi yake akitaka kuwekeza na mwekezaji mgeni katika ubia hilo linawekana na utaratibu huo upo.

Vile vile sisi tunapendekeza zaidi wale watu wa ukanda wa pwani ambao wanazo ardhi zao, basi waingie ubia. Lakini suala la hofu limejengeka sana kwa wananchi wetu na ukiwatajia suala la ubia wanakwambia ubia ni njia tu na wanasema nipe changu nikuachie.

Mhe. Spika, kuhusu thamani ya ardhi. Wakati nilivyokuwa nikijibu suala la mama nilisema kwamba kinachofanyika ni kulipa fidia za vipando ambavyo vimepandwa.

Kwa kweli vipando hivi vinalipwa kwa thamani kubwa sana na nilitoa mfano Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kupitia Idara ya Mazao na Misitu ilifanya tathmini ya mnazi mmoja mkubwa kwa shilingi 5,000/-, lakini mwekezaji alilipa shilingi 20,000/-, yaani mara tatu zaidi.

Kwa hivyo, bado jitihada zinafanywa kuona fidia inakuwa ni kubwa ambayo ya kuridhisha, ili wananchi wetu wasiwe na malalamiko.

**Mhe. Haji Mkema Haji:** Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Eneo hili la Mchangamle ninakubali kwamba lilikuwa ni la serikali ambalo walipewa wananchi wa Muyuni C pamoja na Kizimkazi Dimbani. Lengo lao wananchi hao kupatiwa sehemu ya ardhi, ili walime na waweze kujiajiri kwa kuendesha maisha yao katika shughuli za kilimo pamoja na mambo mengine.

Lakini kwa bahati mbaya ulitokea ugomvi ambao ulipelekea serikali kutafuta mwekezaji, ili eneo hili kuwa na mwekezaji na kuendesha shughuli nyengine.

(a) Hivyo kumpa mwekezaji eneo hilo ndio suluhisho zuri la ugomvi baina ya wananchi wa Muyuni C na Kizimkazi Dimbani ?

(b) Hawa watu waliopewa lengo lao ni kuondosha umasikini, hivyo hizo fedha walizopewa Mhe. Waziri anahakika zitaweza kuendeshea wao pamoja na watoto kwa maisha ya kila siku kama alivyokusudia Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ?

**Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Spika, eneo la Mchangamle kwa kipindi kirefu lilikuwa na ugomvi kati ya wananchi wa Kizimkazi Dimbani na Muyuni C na serikali ilikuwa ilikishughulikia suala hili kuona hakutokei matatizo zaidi.

(a) Eneo hili kupewa mwekezaji hivi sasa ni wazi kabisa ule mzozo uliokuwepo kati ya sehemu mbili hizo umefikia tamati.
(b) Kuhusu fedha walizolipwa fidia wananchi hao, inawezekana kabisa baadhi yao wanaweza kuzitumia kufanyia biashara na kuweza kuendelea zaidi. Isipokuwa nataka niseme kitu kimoja kwamba fedha fedheha, yaani ukiwa nazo utajuta na ukiwa huna pia utajuta.

**Nam. 18**

**Juhudi za Kupambana na Bidhaa Bandia**

**Mhe. Ali Denge Makame –** Aliuliza:-

Hivi karibuni tumeshuhudia wimbi kubwa la uingizaji bidhaa bandia katika nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania, kutoka mataifa mbali mbali ikiwemo China.

(a) Kwa kiasi gani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejidhatiti kupambana na wimbi hilo kwa umakini zaidi, ili kulinda maisha ya wananchi wa Zanzibar ?
(b) Ni chombo gani kinachosimamia uchunguzi wa bidhaa hizo hapa Zanzibar na mpaka sasa kimeshateketeza bidhaa zenye thamani gani?
(c) Chombo hicho kina wataalamu wangapi wanaoweza kufanya kazi za uchunguzi wa bidhaa zinazoingizwa hapa nchini?

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 18 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba hivi karibuni kumezuka wimbi la uingizaji nchini bidhaa au vifaa bandia au vyenye viwango visivyokubalika, kutokana na kutokuwa na utaalam na vifaa vya kufanyia kazi hiyo kitengo cha kumlinda mtumiaji kilijielekeza zaidi kwenye uchunguzi wa bidhaa za vyakula na mafuta ya magari.

a)

i) Kutokana na hali hiyo ilivyo hivi sasa Serikali imekusudia kufanya marekebisho ya kanuni za sheria ya kumlinda mtumiaji na kuelekeza nguvu katika bidhaa za ujenzi na vifaa vya umeme. Pamoja na huduma kama za ndege na nyenginezo badala ya kuangalia chakula peke yake.

ii) Kuimarisha uwezo wa kitengo ili kiendane na kazi inayokusudiwa kufanywa.

iii) Kufanya tafiti kwa kushirikiana na TBS na mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na taasisi kama hizo nje ya nchi na kupata namba za bidhaa za viwango hafifu, au zisizokubalika nchini na nchi zinakotoka. Taarifa hizo zitawekwa katika mtandao wa taarifa za biashara kwa ajili matumizi ya umma.

iv) Kuanzisha kisheria kitengo cha uangalizi wa viwango vya bidhaa za vifaa vya ujenzi na vifaa vya umeme pamoja na huduma zinazotolewa nchini.

b) Mhe. Spika, ni kwamba sheria ya kumlinda mtumiaji sura ya 2 kifungu cha 3(1) inatoa uwezo kwa kitengo cha kumlinda mtumiaji kuangalia ubora wa bidhaa zinazoingia na huduma zinazotolewa nchini, kwa hivyo chombo kinachotakiwa kufanya kazi hiyo ni kitengo cha kulinda mtumiaji.

Niseme tu hakuna bidhaa ya vifaa vya ujenzi vilivyoteketezwa kwa kuwa kazi hii haikuwa ikifanyika kutokana na sababu nilizozieleza hapo awali.

c) Mhe. Spika, kitengo cha kumlinda mtumiaji kina wafanyakazi 22. Unguja 14 na Pemba 8 wafanyakazi hawa wanaweza kuchunguza bidhaa za vyakula na mafuta ya magari, lakini hawana uwezo kwa sasa wa kuchunguza bidhaa nyengine kama swali lilivyoulizwa.

**Mhe. Ali Denge Makame:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kuwa baadhi ya bidhaa hizo zimeingizwa hapa nchini. Je, ana uhakika bidhaa hizo zilizoharibika na kuingizwa hapa nchini zimeathiri watu kiwango gani, na kama wameathirika waletaji wamechukuliwa hatua gani.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Naomba Mhe. Muwakilishi atenganishe bidhaa za aina mbili, nilisema kitengo cha kumlinda mtumiaji kinaweza kuangalia bidhaa za vyakula pamoja na mafuta ya kuendeshea magari, lakini hakina uwezo wa kuchunguza vifaa vya ujenzi pamoja na vifaa vya umeme.

Kwa upande wa vifaa vya vyakula kitengo cha kumlinda mtumiaji pamoja na bodi ya madawa na vipodozi tunajitahidi sana kuhakikisha kwamba bidhaa zinazoharibika hazisambazwi kwenye maduka nchini, tunajua kwamba baadhi ya maduka wanazo lakini tunajitahidi sana kuondosha bidhaa hizo.

Lakini kwa upande wa bidhaa za *hardware na electronic* kama nilivyosema mwanzo bado hatuna uwezo wa kujua na tunashirikiana na *Tanzania bureaude standard* pamoja na mamlaka ya mawasiliano ya Tanzania ili kupata *coads* na tuweze kuziweka kwenye mtandao na kufundisha wafanyakazi wetu ili wawe na ujuzi huo.

**Mhe. Omar Ali Jadi:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa sababu wakati wa kujibu maswali ya msingi Mhe. Waziri kakubali kwamba bidhaa hizi zinaingia. Je? Ni wafanyakazi wangapi waliokuwa wamekamatwa na kama wapo ni hatua zipi zilizochukuliwa kwa wafanyabiashara hao.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Spika, nilikiri katika jibu mama kwamba kitengo cha kumlinda mtumiaji kwa hivi sasa hakina uwezo wa kujua bidhaa za *hardware na electronic*, kwa maana hiyo hatujakamata wala hatujaadhibu.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri alipokuwa akijibu suala la msingi kakubali kwamba ni kweli bidhaa hizo zimeingia, lakini katika kujibu suala la nyongeza anasema kitengo chake cha kumlinda mtumiaji hakina vifaa wala utaalam wa kuweza kukamata vifaa vya *hardware na electronic* hiyo taarifa aliyoipokea ina ukweli gani na ameipata wapi, na katika Baraza hili Waziri hutakiwa aseme ukweli. Wapi amepata taarifa na hana vifaa hivi.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Katika majibu yangu nilisema kwamba tunafanya kazi na *Tanzania Bureaude Standard* kitengo cha kuangalia viwango cha Tanzania, wote tulisikia mwezi wa November na Disemba na nyuma ya hapo, kitengo cha kuangalia viwango Tanzania kiliteketeza bidhaa nyingi ambazo zilikamatwa katika Bandari ya Dar es Salaam. Kwa maana hiyo kuna uwezekano mkubwa sana kwamba baadhi ya bidhaa zilipenya na kuingia Zanzibar kwa sababu mwelekeo wa wafanyabiashara wetu katika kipindi cha hivi karibuni ni kuleta vifaa vya aina hiyo, kwa hivyo ili apae uthibitisho Mhe. Mwakilishi naomba tushirikiane na kitengo na tufanye *research* duka baada ya duka. Namhakikishia kwamba tutakuta waya za umeme ambazo ziko chini ya viwango, tutakuta redio na vifaa vyengine vya *electronic* ambazo ziko chini ya viwango.

Lakini ningemuomba Mhe. Mwakilishi afanye utafiti mdogo tu wa simu tunazozitumia kusanya simu kama sita kuna *code number* nitakupa uweke, katika namba ile kati kati unatakiwa upate namba ziro mbili au ziro moja, katika simu tunazotumia nyingi huwezi kupata *code* namba hii ambayo simu ndio inakubalika kimataifa.

**NAM. 7**

**Uimarishaji wa Kilimo Zanzibar**

**Mhe. Ali Abdalla Ali** **–** Aliuliza:-

Tunaipongeza Serikali kwa ununuzi wa Matrekta mapya yaliyogaiwa Unguja na Pemba. Hata hivyo, yapo Matrekta mengi mabovu na Serikali inashindwa kuyatengeneza kutokana na ukosefu wa fedha za kununulia vipuri. Hivyo, Matrekta hayo yanazidi kuharibika na matokeo yake Serikali inaendelea kupata hasara kubwa.

(a) Kwa kuwa Serikali imeshindwa kuyatengeneza Matrekta hayo kwa muda mrefu sasa, Je, kuna sababu zipi zinazoizuia kuyauza.

(b) Kwa kuwa Matrekta hayapatiwi fedha za kuyafanyia matengenezo *“service”* kwa wakati. Je, Mhe. Waziri huoni kuwa hii husababisha kuharibika mapema kwa matrekta hayo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 lenye vifungu (a) na(b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza napenda kumshukuru Mhe. Mwakilishi kwa kuona umuhimu wa suala la Matrekta na kutaka kuokoa mali za Serikali zisipotee.

(a) Nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kuwa Serikali haijashindwa kuyatengeneza Matrekta makongwe isipokuwa kila mwaka Matrekta hayo hufanyiwa tathmini ili kuona yepi ambayo yanaweza kutengenezeka. Vile vile Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inatenga fedha za kuyafanyia matengenezo matrekta makongwe kila mwaka. Kwa mfano kwa mwaka wa fedha 2008/2009,Wizara imelenga kutengeneza matrekta 8 makongwe. 4 Unguja na 4 Pemba, hadi kufikia Disemba, 2008, matrekta 5 Unguja na 1 Pemba yalifanyiwa matengenezo. Ingawa mfumko wa bei za vipuri husababisha kushindwa kufikia lengo lililokusudiwa.

Naomba ieleweke kuwa ingawa katika msimu wa 2008/2009, Serikali ilinunua matrekta 12 mapya, lakini kabla ya hapo matrekta makongwe ndio yaliyokuwa yakitengenezwa na kutumika. Hata hivyo, Wizara ya Kilimo itaendelea kuyafanyia tathmini ya kiufundi
matrekta yote makongwe na yale ambayo yatayoonekana hayatengenezeki kabisa. Serikali juu ya maamuzi sahihi ya kuchukuliwa.

(b) Miongoni mwa fedha zinazotengwa katika Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa matengenezo ya matrekta, kila mwaka ni pamoja na zile za kufanyia huduma *(service)* matrekta yote. Hata hivyo, mfuko wa bei za vipuri imesababisha gharama za huduma za matrekta kuwa kubwa sana kiasi ambacho husababisha wakati mwengine huduma za matrekta kuchelewa kwa kusubiri fedha za ziada.

Mhe. Spika, ni kweli Wizara yangu inakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa matrekta kutoyafanyia *service* kwa wakati inasababisha maharibiko ya mara kwa mara, kwa hivyo ni muhimu fedha hizo za matengenezo kutoka bajeti ya serikali zikapatikana kwa wakati vile vile kazi za wakati zinakwenda na wakati wa msimu.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu cha a na bi kama ifuatavyo:

Kwa kuwa nchi au jumuiya huwa ina viwango vya kutumia magari muda gani Wizara ya Kilimo inawekea trekta jipya litumike kabla halijaondoshwa katika kazi, kwa mfano katika Umoja wa Mataifa gari zao huwa wanatumia kwa miaka mitano halafu wanauza kwa sababu ya gharama kubwa ya kuendesha kitu kikiwa kikongwe.

a) Je, Wizara ya Kilimo ina utaratibu gani wa kutumia matrekta hali akaiondoa katika *service.*

b) Kwa kuwa matrekta yanahitaji kutengenezwa haoni kwamba wale wagonjwa wawili walio mahututi yaani Karakana ya Mbweni na Karakana ya Wawi pale, ndio sababu kubwa iliyosababisha yasiwe kutengenezwa kwa wakati.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Nilijibu katika suala mama kwamba tunayafanyia tathmini yale Matrekta ya zamani na kuweza kuishauri serikali juu ya njia gani iweze kufanyiwa, lakini kwa sisi nchi yetu ya kimasikini hatujajipangia malengo labda tutumie matrekta kwa miaka mitano halafu tuondoe, wenzetu wao ni mtajiri wanaweza kutumia hata miaka miwili halafu wakasema hayawafai wakauza.

a) Lakini kutokana na unyonge wetu sisi huwa tunayatengeneza yale yale ambayo ni mabovu, na pale tunapopata mapya au ya ziada zaidi kikishatimilia kile kiwango cha kuwa na matrekta ya kutosheleza, basi yale ambayo ni mabovu sana tutaishauri serikali ili yaweze kuuzwa.

c) Suala la Karakana ambayo iko Pemba Wawi na hii hapa ya Unguja si sababu tosha ya kusema ndio ambayo inasababisha matrekta haya yazidi kuwa mabovu, nimesema hii inaokana na bajetu yetu ya serikali kuwa finyu. Pale bajeti ya serikali itakapoweza kujitosheleza zaidi basi tatizo hili litaondoka mara moja.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Serikali baada ya kusikia kilio cha wananchi hasa wakulima ilijitahidi kufanya kila mbinu ili kuona kwamba mkulima anakomboka, miongoni mwa mambo haya ambayo serikali imejitahidi ni kuagizia matrekta, lakini hata ile kupunguza bei ya mbolea kwa asilimia hamsini ni kwango kikubwa. Hivi leo Mhe. Waziri ukisema kwamba bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira hasa ya *survice* ya matrekta inachelewa.

Je? Serikali inatwambia nini bado ina juhudi au inakwamisha hiyo juhudi ya kilimo.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduz anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi:** Nakubaliana na maelezo ya msingi aliyoeleza kwenye swali lake la nyongeza Mhe. Ame Mati Wadi, kwamba serikali inajitahidi kuhakikisha kamba sekta ya kilimo hasa mahitaji ya wakulima yanatimizwa kwa mujibu wa uwezo wetu kwa wakulima, juhudi hiyo kama alivyosema ni kununuliwa matrekta mapya yale makubwa ya *ford* pamoja na yale ya kuburura kwenye umwagiliaji.

Tunamhakikishia kwamba lengo letu ni kupata matrekta hamsini na moja na hilo tumeshaweka kwenye bajeti yetu na tutajitahidi mwaka huu kupata mengine mpaka kufikia lengo hilo, lakini kuhusu utengenezaji wa matrekta serikali inajitahidi kwa mujibu wa uwezo wetu wala hatuyaachii yakafa, na uwezo wa kuishi matrekta ni muda mrefu sana miaka sitini mpaka sabiini kama utatembelea mikoa ya Arusha au Mbeya utakuta yapo mimi na wewe Mhe. Ame Mati hatujazaliwa ni mazee kabisa, kwa sababu yanapata vipuri.

Kwa hivyo ni lengo na sisi serikali kujitahidi kadri yanavyoharibika tujitahidi tupate pesa na tuweze kuyatengeneza, lakini naomba kutoa mwito maalum hasa kwa viongozi kama Mhe. Ame Mati Wadi watusaidie kwa wakulima wetu kwamba ufanisi unapatikana trekta linapokwenda kulima wanakuwepo wote na wanajitayarisha isiwe lime eka moja hapa, kule mbili. Lakini linapoingia likalima eka hamsini kwa mpigo au eka mia basi ufanisi unapatikana na hata utunzaji wake unapatikana vizuri, kwa hivyo ningeomba sana waheshimiwa watusaidie wakiwa kama wawakilishi kuelimisha wakulima wetu twende sambamba.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Nakushukuru Mhe. Spika, na naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Pamoja na jitihada nzuri ya Serikali kama ilivyoelezwa ya ununuzi wa matrekta ya ziada lakini umadhubuti wa karakana za matrekta ni jambo muhimu sana katika kuyatengeneza matrekta yenyewe, kwa sababu karakana zote mbili za Mbweni na Wawi zina ukosefu wa vipuri, zinaukosefu wa mashine za kufanyia matengenezo na kwa sababu karakana zenyewe zinaidai serikali pesa nyingi ambazo zingehitajika katika kununua vifaa hivyo.

a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kulipa pesa hizi kwa karakana hizo ili ziweze kujiimarisha na kuweza kutengeneza matrekta yenyewe.

b) Kwa sababu karakana zenyewe siku hizi zimetangazwa kama ni shirika ambalo haliendi. Je, Wizara ina mpango gani wa kuirudisha kama ni idara ya Serikali ili iweze kupata bajeti kama taasisi nyengine ili iweze kushughulikia *survece* za matrekta yetu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduz anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi:** Ni kweli kwamba karakana hizi zina zinazidai taasisi za serikali fedha nyingi, sasa kwa mujibu wa utaratibu wetu wa fedha hivi sasa taasisi hizo zina wajibu wake kulipa madeni hayo kwa sababu wanapatiwa *o/c* sasa wafanye taratibu zao wenyewe walipe, lakini kwa yale madeni waliyonayo Wizara ya Kilimo kwa sababu mdai mkubwa ni Idara ya Kilimo na hili ni Shirika kwa hivyo wenyewe watafanya utaratibu wa kulipa deni hilo kwa kupitia kuomba fedha hizo serikalini, serikali itajitahidi tuwapatie fedha hizo walipe.

Lakini naomba nizungumzie uwezo wa karakana zile zina uwezo mkubwa kabisa, mashine walizokuwa nazo ni za kisasa mimi nakumbuka Waholanzi wale walipojenga walijenga kwa uwezo wa haili ya juu kabisa tena sio matrekta tu hata gari wanatengeneza, nafikiri hivi sasa wameruhusiwa wantengeneza magari kwa kujipatia pesa zaidi za ziada. Tatizo ni kwamba inapoharibika inabidi zipatikane *spear* zinunuliwe, sasa hizo labda kwa wakati ule pengine huwa shida kupatikana pesa kwa wakati lakini pesa wanapatiwa zinanuliwa *spear* halafu zinatiwa kwenye matrekta.

Lakini hata hivyo tukubali kwamba *spear* zenyewe za matrekta ni ghali sana, sasa utashangaa ukiambiwa shilingi milioni mia tano *spear* zake unaweza kuzichukua hata kwenye mkoba tu, hizo *bush* zake moja ni ghali mno.

## SHUGHULI ZA SERIKALI

### Mswada wa Sheria wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia Zanzibar

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia Ijumaa ya leo kuwa wazima na wenye afya, pili naomba nichukue nafasi hii kutoa pole kwa wale wote ambao walipata mitihani ya kufiliwa.

Mhe. Spika, serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua umuhimu wa elimu katika kuendeleza maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni katika nchi na watu wake kwa jumla.

Aidha serikali inatambua mchango mahususi unaotolewa na sekta ya elimu ya ufundi sayansi na teknolojia katika kufanikisha upatikanaji wa maendeleo hayo, kwa hivyo mara tu baada ya Mapinduzi ya Mwaka 1964 SMZ kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani ilianzisha Chuo cha Ufundi huko Mbweni mwaka 1966, kikiwa na lengo la kulipatia taifa wataalam katika fani mbali mbali za ufundi. Chuo kilianza na wanafunzi 57 ambao walisomea fani za uhandisi wa umeme na uhandisi wa mitambo, mafunzo yaliyotolewa yalilenga kutayarisha vijana ambao wataweza kufanya kazi za kukarabati na kutengeneza mashine ndogo ndogo na kuendelea na elimu ya Chuo kikuu katika fani mbali mbali za ufundi na uhandisi.

Katika mwaka 1972 Chuo kilibadilishwa jina na kuitwa Chuo cha Ufundi Karume kwa lengo la kumpa heshima muasisi wa mapinduzi yetu na Rais wa Kwanza wa Zanzibar marehemu Sheikh Abeid Amani Karume, kwa kuzitunza na kuziendeleza fikra zake sahihi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka 42 tangu kuanzishwa kwake Karume *technical college* imepata mafanikio makubwa, wahandisi na mafundi wakubwa wengi tulikuwa nao hapa Zanzibar wamesoma Chuo cha Karume, fani za ufundi zinazotolewa katika chuo hicho zimeongezeka na sasa Karume inatoa mafunzo katika fani za uhandisi wa mitambo, umeme, magari, ujenzi na teknolojia ya habari na mawasiliano.

Vile vile kiwango cha elimu inayotolewa imepanda kutoka ngazi ya cheti FTC na kufikia ngazi ya Stashahada *(Diploma intechnical education)*, aidha Karume inatoa mafunzo ya muda mfupi ya kujiendeleza katika fani mbali mbali na ushauri wa kitaalam kwa taasisi za serikali na watu binafsi. Kutokana na mchango mkubwa wa sayansi na teknolojia katika maendeleo ya nchi kuna haja kubwa ya kukiimarisha Chuo cha Karume ili kukiwezesha kukabili ipasavyo mabadiliko ya kazi yanavyotokea ulimwenguni hasa yanayohusiana na maendeleo ya Sayansi na teknolojia, hagtimae kutoa mchango mkubwa zaidi katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, madhumuni ya mswada huu ni kuwasilisha mapendekezo ya kuanzisha taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia inayojitegemea wenyewe kiutawala, mchakato wa kuanzisha taasisi ya teknolojia hapa Zanzibar ilianza tangu mwaka 1986 pale serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipofanya juhudi za makusudi za kumleta mtaalam wa kutoka India, ili kufanya uwezekano wa taasisi ya teknolojia hapa Zanzibar. Katika ripoti yake aliunga mkono wazo la kuwa na taasisi ya kuwa na teknolojia, lakini akapendekeza iitwe jina la taasisi ya teknolojia ya Afrika, ili iweze kutoa taaluma kwa wananchi wa Zanzibar na wakati huo huo kuchukua wanafunzi kutoka nchi mbali mbali za Kiafrika.

Hata hivyo juhudi hizo zilikwamba kutokana na hali ngumu ya kiuchumi iliyolikabili taifa wakati huo na pia kukosekana washirika wa maendeleo wa kusaidia gharama za mradi huu, juhudi ziliendelezwa mwaka 1994 baada ya mtaalam huyo kuja tena Zanzibar na baada ya utafiti mwengine ilikubalika kwamba taasisi ya teknolojia ianzishwe hatua kwa hatua, kwa kukiimarisha na kukikuza chuo cha ufundi cha Karume.

Mhe. Spika, Chuo cha Ufundi cha Karume ni moja kati ya vyuo vitano vilivyoanzishwa mara tu baada ya uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 ya hapa Zanzibar, vyuo vyengine vya wakati huo vilikuwa ni Chuo cha Ufundi cha Dar es Salaam, Chuo cha Ufundi cha Arusha, Chuo cha Ufundi cha Mbeya na Chuo cha Ardhi cha Dar es Salaam. Vyuo vyote vitano vilikuwa vikitoa vyeti vinavyolingana vya ufundi sanifu na kufuata muhtasari mmoja. Kwa maana hiyo Mtanzania yoyote angelisoma kimoja ya vyuo hivyo vilivyotajwa na kupata vyeti vinavyolingana, hata hivyo vyuo vinne vianzilishi vilioko Tanzania Bara vimeongezewa hadhi na kugeuzwa kuwa taasisi zinazojitegemea kiutawala na zenye uwezo wa kutoa vyeti, stashahada na hata shahada. Majina mapya ya vyuo hivyo ni Dar es Saalam *institute of technology, Mbeya Institute of Science of technology, Ardhi Universty.* Mhe. Spika, kuna haja kubwa Chuo cha Karume nacho kupandishwa daraja ili kiweze kutoa wataalam wa daraja za juu zaidi hapa nchini.

Mhe. Spika, Chuo cha Ufundi cha Karume kama vilivyo vyuo vyengine vinavyotaka kutambuliwa rasmi ni mwanachama wa Baraza la Taifa la Ufundi tangu mwaka 2002, masharti ya kuendelea kuwa mwanachama ni pamoja na chuo kuwa na uwezo wa kujiendeleza kiutawala na kuwa na bajeti yake, kwa hivi sasa chuo cha ufundi Karume hakina tofauti na skuli za kawaida kwani hakikuanzishwa kisheria. Kwa hivyo hakiko huru katika uendeshaji wake, vyuo vingi vilivyopo Zanzibar vyenye hadhi sawa na Chuo cha Karume tayari vimeanzishwa kisheria na vinategemea ruzuku yake maalum kutoka serikalini.

Mhe. Spika, Nate imeanzisha mfumo mpya wa mfunzo unaoitwa *compitance base education of training,* mfumo huu mpya unamuwezesha mwanafunzi kuhitimu kutoka ngazi ya cheti na kujiendeleza hadi kufikia shahada ya uzamili yaani PhD katika fani ya elimu za ufundi, kama vinavyoonekana kwenye maelezo haya ambayo nimeyasambaza kwa waheshimiwa wajumbe.

Mhe. Spika, Chuo cha Ufundi cha Karume ndio pekee hapa Zanzibar kinachotoa elimu ya ufundi hadi ngazi ya stashahada, chuo hiki kikiimarishwa kuwa taasisi ya Karume ya Sayansi na teknolojia kitakachokuwa na uwezo wa kutoa stashahada na shahada itapanua wigo wa taasisi za elimu ya juu na hivyo kuongeza elimu ya juu kwa wanafunzi hapa Zanzibar. Aidha kuwepo kwa taasisi ya sayansi na teknolojia itatoa fursa zaidi ya kutoa fani mpya za

mafunzo ya ufundi na kufanyika utafiti katika masuala ya sayansi na teknolojia ambazo hivi sasa ndio msingi wa maendeleo duniani, kuanzishwa kwa taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia kutaongeza kasi ya upatikanaji wa utaalam wa daraja la juu zaidi ambao hivi sasa wanahitajika sana katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa baadhi ya fani za ufundi chuo cha ufundi cha Karume tayari kina vifaa vya kisasa na wataalam wa kuendesha mafunzo katika daraja za juu zaidi kuliko ile ya sasa ya *level* VI. Kukigeuza chuo hicho kuwa taasisi iliyo huru kiutawala na kiuendedsha kutoa fursa ya kukiimarisha na kuwapa maslahi bora zaidi watumishi wake na kuwanusuru na ushawishi wa kuondoka nchi kwa lengo la kutafuta maslahi bora zaidi nchi nyengine.

Mhe. Spika, kuanzishwa kwa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia kutaongeza idadi ya Taasisi za Elimu ya juu nchini na kwa hivyo kutakuwa ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa ilani ya CCM "Mpango wa kuondosha umasikini na kukuza uchumi za Zanzibar" na Sera ya Elimu ya mwaka 2006.

Mapendekezo ya Mswada, Mhe. Spika, mapendekezo ya Mswada wa sheria wa kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, waheshimiwa wajumbe wanayo. Mswada huo umegawika sehemu tano kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| Sehemu ya Kwanza : | Inaelezea jina na tafsiri ya maneno mbali mbali yanayotumika katika sheria hii. |
| Sehemu ya Pili: | Inaelezea kuhusu uanzishwaji wa taasisi na idara zake. Kazi za taasisi na utaratibu wa kutunuku vyeti. |
| Sehemu ya Tatu: | Inaelezea masuala ya utawala yakiwemo uundwaji wa Baraza la Taasisi, uwezo wake na taratibu zake za kufanya kazi. Undwaji wa Bodi ya taaluma na uwezo wake. Utaratibu wa kupata viongozi na watumishi wa taasisi na uundwaji wa jumuia ya wanafunzi. |
| Sehemu na Nne: | Inaelezea masuala ya fedha na taasisi yakiwemo vyanzo vya mapato, uwekezaji, bajeti, ukaguzi wa mahesabu na uwasilishaji wa ripoti. |
| Sehemu ya Tano: | Inaelezea mambo mbali mbali ya jumla yakiwemo uwezo wa Baraza la Taassi |

kutunga sheria ndogo ndogo, taratibu za kushughulikia makosa ya kinidhamu na ukataji wa rufaa na uwezo wa Waziri anayehusika katika kutunga kanuni mbali mbali za kurahisisha utekelezaji wa sheria hii.

Mwisho Mhe. Spika, kuwepo kwa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia hapa Zanzibar kutaiwezesha nchi kwenda sambamba na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia ulimwenguni, kwa kutayarisha wataalamu wa hali ya juu. Kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika fani mbali mbali za sanyansi na teknolojia.

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuuchangia Mswada huu na hatimaye kuupitisha rasmin.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii):** Mhe. Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, nikiwa na afya njema, ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii juu ya Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia na Mambo Mengine Yanayohusiana nayo.

Mhe. Spika, aidha nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwanzo katika Mswada ulio mbele yetu ambao umewasilishwa hapa Barazani na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati, niruhusu nitoe shukurani za dhati kwa Kaimu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mheshimiwa Mwinyi Haji Makame, Wanasheria pamoja na watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuweza kuisaidia Kamati, wakati wa kujadili Mswada, kwa kuipatia ufafanuzi wa maelezo pale ilipobidi.

Mhe. Spika, Kamati yetu ilitekeleza kazi ya kuupitia Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknoloijia, hapa Afisi ya Baraza la Wawakilishi, siku ya Jumatano ya tarehe 14/01/2009 na napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano wao

mkubwa waliouonesha, wakati Kamati ilipoupitia kwa kina Mswada huo. Naomba niwataje wajumbe hao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Ali Suleiman Ali | - | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Ame Mati Wadi | - | Makamo M/kiti |
| 3. Mhe. Ali Haji Ali | - | Mjumbe |
| 4. Mhe. Ali Mzee Ali | - | Mjumbe |
| 5. Mhe. Haji Faki Shaali | - | Mjumbe |
| 6. Mhe. Hasnuu Moh'd Haji | - | Mjumbe |
| 7. Mhe. Mohammed Ali Salim | - | Mjumbe |
| 8. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | - | Mjumbe |
| 9. Mhe.Raya Suleiman Hamad | - | Mjumbe |
| 10. Mhe.Salim Abdalla Hamad | - | Mjumbe |
| 11. Ndg.Ramadhan Kh. Masoud | - | Katibu, |

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati napenda kuchukua fursa hii, kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na serikali kwa ujumla kwa kutuwasilishia mbele ya Baraza lako tukufu Mswada wa Sheria ambao unakusudia kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia itakayojitegemea kiutawala.

Mhe. Spika, Mswada huu umewasilishwa hapa Barazani katika wakati muafaka na hasa ikitiliwa maanani kwamba nchi nyingi za dunia ya tatu zimeanza kujihusisha na dhana hii muhimu ya Sayansi na Teknolojia kwa kuanzisha Taasisi, Vyuo Vikuu na hata wizara zenye kuhusika na masuala ya Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kujiletea maendeleo.

Mhe. Spika, kuchangia maelezo yangu kuhusu mswada huu wa uanzishwaji wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia sina budi kuelezea japo kwa muhtasari kuhusu umuhimu wa dhana ya sanyansi na teknolojia katika jamii.

Mhe. Spika, kama inavyoeleweka, dhana ya Sayansi na Teknolojia ni moja wapo ya vipengele muhimu vilivyoziwezesha nchi ambazo hivi sasa ni tajiri duniani na baadhi ya nchi za dunia ya tatu kwa mfano India na China kupiga hatua kubwa za kimaendeleo katika nyanja mbali mbali za kiuchumi na kibiashara, kisiasa na kijamii.

Mhe. Spika, wataalamu wa masuala ya Sayansi na Teknolojia, katika kuelezea umuhimu wa dhana hii, wanasema kwamba Sayansi na Teknolojia ni moyo au mzizi wa Maendeleo ya Jamii ambayo mwanadamu anaishi ndani yake.

Kwa upande wao, Maprofesa wa Uchumi, katika Chuo Kikuu cha New Delhi – India, ambao pia ni Waandishi mashuhuri wa makala na vitabu vya uchumi, Bwana Ruddar Datt na K.P.M Sundaram, katika kitabu chao kiitwacho ***"INDIAN ECONOMY"*** wanasema kwamba "Sayansi na Teknolojia ni dhana na njia aitumiayo Mwanadamu katika kuyabadilisha mazingira yake".

Mhe. Spika**,** hivyo basi, jamii yetu, kama zilivyo jamii nyengine ulimwenguni, haiwezi kuepuka kujihusisha na dhana hii muhimu kwa kuitekeleza kwa dhati; kinadharia na kivitendo kwa lengo la kujiletea maendeleo katika nyanja zote za maisha.

Mhe. Spika, Kamati yetu inafarajishwa sana na hatua iliyochukuliwa na Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya kutuwasilishia mswada huu mbele ya Baraza lako tukufu. Hatua hii inamaanisha kwamba Nchi yetu ya Zanzibar nayo imekuwa na azma ya kutaka kufika kule wenzetu waliko hivi sasa.

Mhe. Spika**,** hivyo basi,kwa niaba ya Kamati, nawaomba wajumbe wote tuuchangie kwa dhati Mswada huu na hatimaye tuupitishe ili tuanze safari ya kuifanya Zanzibar kuwa ni nchi ya Sayansi na Teknolojia.

Mhe. Spika, Kamati yetu inatarajia yafuatayo mara baada ya mswada huu kupitishwa na kuwa Sheria:-

a) Kuwa na taasisi ya Sayansi na Teknolojia itakayoundwa kwa mujibu wa sheria na itakayoweza kujitegemea kiutawala.

b) Kuwa na taasisi itakayotoa wataalamu wenye mwelekeo wa vitendo zaidi kuliko nadharia na wenye kukubalika katika soko la ajira katika mfumo wa sasa wa utandawazi.

c) Kuwa na taasisi itakayotoa walimu watakaotumika katika skuli zetu mbali mbali na kupunguza tatizo liliopo hivi sasa la uhaba wa walimu wa sayansi katika skuli zetu za Unguja na Pemba.

d) Kuwa na taasisi itakayotoa wataalamu watakaotumika kuishauri ipasavyo serikali na nchi yetu kwa ujumla.

e) Kuwa na taasisi itakayokuwa na nafasi na uwezo wa kubuni na kutoa maamuzi makini ya utekelezaji wa mipango yake kwa madhumuni ya kuimarisha elimu itakayotolewa na Taasisi hiyo.

Mhe. Spika**,** hata hivyo, Matarajio ya Kamati na lengo la uanzishwaji wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, yanaweza yakaleta matunda mazuri kwa nchi yetu ikiwa mamlaka husika zitazingatia na kutekeleza yafuatayo:-

1. Kuweka maandalizi ya kutosha kwa ajili ya kuipatia Taasisi itayoanzishwa mambo yafuatayo:-.

    a) Majengo ya kisasa yanayojumuisha madarasa, ofisi mbali mbali, maktaba, maabara na karakana, mabweni ya wanafunzi na nyumba za wafanyakazi.

    b) Walimu wa kudumu na wa kutosha wenye sifa zinazokubalika.

    c) Ruzuku ya kutosha na misaada mbali mbali itakayoiwezesha Taasisi kujiendesha kama ilivyokusudiwa.

    d) Maslahi mazuri na yenye kuvutia kwa Walimu na Wafanyakazi wengine ili Taasisi itakayoanzishwa isije ikakimbiwa.

    e) Fursa za kutosha kama vile kujiendeleza kielimu na kupatiwa mikopo kwa walimu na wafanyakazi.

    f) Uongozi bora na mipango mizuri itakayokuwa chachu ya kuiletea Maendeleo Taasisi hii.

2. Serikali kuipa kipaumbele dhana ya Sayansi na Teknolojia likiwemo suala la uendelezwaji wa taasisi itakayoanzishwa kwa lengo la kutaka kufika kule tunakotaka kwenda.

3. Kuwepo kwa mashirikiano ya kutosha kati ya Serikali na Taasisi itakayoanzishwa ili taasisi hiyo iweze kufikia malengo itakayojipangia.

4. Kuwepo kwa mahusiano ya kutosha kati ya taasisi itakayoanzishwa na taasisi za nchi za nje zinazojihusisha na masuala ya Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kujenga urafiki na kupatiwa misaada mbali mbali itakayoiimarisha Taasisi hiyo.

5. Kuwepo kwa mipango madhubuti itakayowawezesha wahitimu wa Taasisi inayokusudiwa kuanzishwa, kuwa na mazingira mazuri ya

kuajiriwa katika sekta mbali mbali kama vile Kilimo, Biashara, Viwanda, Afya, Habari na Mawasiliano.

Mhe. Spika, bila shaka kila Mjumbe wa Barazani amepatiwa nakala ya marekebisho ya Mswada uliopo mbele yetu. Hivyo kwa kuokoa muda ni vyema nisirudie yale ambayo yamekwishaelezewa katika nakala hizo za marekebisho.

Mhe. Spika**,** baada ya maelezo hayo, naomba uniruhusu nikushukuru kwa mara nyengine na kwa niaba ya Kamati, naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja.

Naomba kuwasilisha. Ahsante Mhe. Spika.

**Muhammed Ali Salim (Mulla) (Waziri Kivuli Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali):** Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa viumbe wote, mstahiki wa shukrani kwa neema kubwa aliyotubariki ya uhai na uzima na tukaweza kukutana hapa na kujadili mambo ya maslahi ya taifa letu. Namuomba Allah aniwezeshe kutoa maoni haya kwa upole na utulivu na ayajaalie yawe maoni yenye faida.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu kama inavyoagiza Kanuni ya Baraza hili la Wawakilishi. Nawaomba wajumbe wako watukufu wa Baraza hili wanisikilize na wanivumilie mpaka nimalize.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kusikitika kwa ucheleweshaji wa kupatikana Miswada. Kanuni ya Baraza hili kifungu cha 78 (2) kinaeleza wazi ni muda gani mdogo wa mwisho unaostahiki mswada kutolewa. Lakini kwa mujibu wa barua ya mwaliko wa Baraza wa mkutano huu Miswada imepokelewa Barazani tarehe 9.01.2009 siku 11 tu kufikia siku ya kusomwa miswaada hiyo. Sasa ikiwa Barazani Miswada imefika tarehe hiyo, jee, Mjumbe aliyeko Pemba anatarajiwa aupate siku ngapi kabla ya kusomwa kwa mara ya kwanza Barazani.

Jambo hili Mhe. Spika, limekuwa likizungumzwa Barazani mara kadhaa lakini matokeo yake hakuna marekebisho yanayofanywa. Nakuomba Mhe. Spika, kwa kuwa wewe ndiye msimamizi mkuu wa habari hii utafute dawa ili Miswada ipatikane kwa mujibu wa Kanuni niliyoitaja. Inawezekana kama tutatimiza wajibu.

Mhe. Spika, jambo jingine la jumla na ambalo katika Mswada huu limo ni makosa mengi ya uandishi. Kwa kweli mara nyingi huwa tunajiuliza jee, haiwezekani makosa haya angalau kupunguzwa kama sio kuondoshwa kabisa?

Tunavyoelewa Mswada unapita sehemu kadhaa mpaka ukafika Barazani. Hivi kweli vikao vyote hivyo huiangalia miswada ipasavyo na makosa yote wasiyaone? Katika hili Mhe. Spika, naomba kurekebisha marekebisho ya Kamati ukurasa wa pili kifungu cha 6, mstari wa tano neno ”atakaeteuliwa” lisomeke ”atakayeteuliwa”. Aidha kifungu cha 10 ukurasa watatu mstari wa kwanza neno ”atastahiki” lisomeke ”atakayestahiki”.

Mhe. Spika, hivi sasa tunacho Chuo Cha Ufundi cha Karume. Chuo hiki ni cha muda mrefu na kimeshatoa wahitimu wengi. Lakini kwa muda wote huo hakikuwa na sheria yake isipokuwa kikitumia Sheria ya jumla ya Elimu. Leo tunaujadili mswada ambao umekusudiwa uwe sheria itakayobadilisha mambo kadhaa, kuanzia jina la chuo, utawala wa chuo, elimu itakayotolewa na tunuku zake. Sijambo baya kuanzisha taasisi ya sayansi na teknolojia lakini wengi wanauliza jee uwezo wa kufanya hivyo tunao? Au kama kawaida ya baadhi ya watu tunataka tumuige ndovu?.

Mhe. Spika, ukitafunwa na nyoka, ukiona ukuti tu huwa unashtuka. Tumejaribu kumulika hali halisi ya hivi sasa tulivyo na tunaona kuna matatizo kadhaa katika skuli zetu mbali mbali. Kwa mfano ukiangalia skuli kama vile, skuli ya ufundi Kengeja, skuli ya Sekondari ya Utaani, Skuli ya Sekondari ya Fidel Castro, Skuli ya Sekondari ya Lumumba ambazo zote ni za kale bado zina mashaka kadhaa ya ubovu wa majengo, uhaba wa walimu, ukosefu wa dakhalia na hata upungufu mkubwa wa vifaa vya kusomea na kusomeshea na hasa vya sayansi. Skuli hizi nimezitaja kwa ukongwe wake lakini sio hizi tu, kwa kweli skuli zetu zote zina matatizo mbali mbali ambayo ni ya muda mrefu na yamekosa marekebisho. Kwani ikiwa kilemba kimeroa seuze mkuti? Hapa tunamaana kuwa ikiwa skuli hizi kubwa na za kale zina matatizo yote haya, jee skuli ndogo na za vijijini zitakuwa na hali gani?
Mhe. Spika, matatizo katika Wizara ya Elimu ni mengi sana na wizara mpaka sasa imeshindwa kuyatatua. Kuna majengo ambayo wananchi wamejenga kwa nguvu zao na kuikabidhi wizara kwa kuyamaliza lakini wizara imeshindwa. Hatuna haja ya kuyaorodhesha matatizo ya wizara kwani wajumbe wote wanayaelewa.

Mhe. Spika, kuyataja haya hatuna nia ya kukumbusha kilio matangani, bali tunakusudia kutoa indhari kwa serikali katika hatua zake za matayarisho.

Sisi Kambi ya Upinzani tunajiuliza maswali kadhaa yanayohusu matayarisho ya taasisi hii inayotaka kuanzishwa. Taasisi ya Sayansi na Teknolojia inahitaji kuwa makini katika kuitayarisha. Kwani kuwa na sheria ni kitu kimoja na kuitekeleza ni kingine. Tunajiuliza jee ni majengo gani yatakayotumika kwa Taasisi hiyo? Ni yale yaliyopo au kuna mpango wa kujenga mengine? Jee, kuna wataalamu wa kutosha watakaofundisha katika taasisi hiyo au

tumekusudia kubaka huku na kule. Nyenzo za kusomea na kusomeshea tayari tumezitengea fedha au zimeshaagizwa? Lakini muhimu zaidi tunao wanafunzi tuliowatayarisha katika masomo ya sayansi watakaojiunga na taasisi hiyo au tutategemea zaidi wageni?

Mhe. Spika, maswali haya na mengine kadhaa yahusuyo matayarisho na utayari wetu kwa taasisi hii tunayauliza kwa nia njema ili Mswada huu utakapopita kusiwe na vikwazo vingi katika utekelezaji wake.

Mhe. Spika, ni jukumu la serikali kuwafahamisha wajumbe wa Baraza hili tukufu utayarishaji wake katika kuanzisha taasisi hii ili watakapoupitisha Mswada wasiwe na wasiwasi.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunivumilia na nawashukuru wajumbe kwa kunisikiliza. Naomba mswada huu uchangiwe vizuri ili kama itaanzishwa taasisi hiyo iwe ya uhakika.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Nashukuru na mimi nakiri kwamba kweli Miswada ilichelewa na kwa sababu hiyo hata mimi nilishiriki katika kuisambaza ili kuona kwamba inawafika wajumbe sio kwa kuchelewa zaidi. Nilikwenda Pemba na nikaifanya kazi hiyo, kazi ambao huwa wanafanya maafisa wangu lakini mara hii na mimi nilishiriki kikamilifu. Lakini jitihada nitachukua ili kuona Miswada inapatikana kwa wakati kwa mujibu wa taratibu za Kanuni zilivyo.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya mwanzo baada ya Mhe. Waziri, Mwenyekiti wa Kamati na Waziri Kivuli na mimi sitakuwa na mchango mkubwa kwa sababu Mswada wenyewe ni mfupi kidogo. Ila pamoja na ufupi wa Mswada wenyewe ni muhimu sana.

Kwanza naomba niingie ndani ya Mswada ili kuweza kueleza mawili machache, halafu nende katika maelezo ya jumla. Kwanza ambalo nataka nishauri ni katika kifungu cha 2 imeelezwa ”Waziri”. Waziri maana yake ni Waziri anayehusika na Elimu. Mimi nishauri hapa isiwe Waziri wa Elimu kwasababubu kesho na keshokutwa inawezekana tukaandaa Wizara ya Sayansi na Teknolojia na labda pengine inaweza ikawa chini ya wizara hiyo. Ningeshauri kwamba waziri ikawa anayehusika na masuala ya Sayansi na Teknolojia.

Suala la pili kifungu cha 6 ni kwamba Mwenyekiti atateuliwa na Rais, lakini hapa haikuelezwa kwa sifa zipi. Ningeshauri ni vizuri asaidiwe Rais katika uteuzi wake iwekwe japo sifa ambayo Mhe. Rais ingemsaidia katika kuteuwa Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi.

Kifungu cha 11 ni uteuzi wa Mrajis hapa pia hakuna sifa za kielimu za huyo Mrajis atakayeteuliwa. Na hapa pia ningeshauri kwamba pawe na sifa za kielimu za Mrajis atakayeteuliwa na Baraza kwa ushauri wa Mkurugenzi.

Sasa niende moja kwa moja katika maelezo. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametupa karatasi ambayo aliisoma wakati anazungumza. Kwa kweli na mimi naomba nikubaliane na maoni ya Waziri kivuli kwamba jina halitoshi na ”jina si mboji” Waswahili wanasema. Sioni kama kuna matayarisho ya maana yaliyofanywa katika kuanzisha taasisi hii. Si utaratibu mzuri Mhe. Spika, kubadilisha tu majina na kukawa hakuna maandalizi ya maana yaliyofanywa, tutakuwa hatusaidiani sana katika kuendesha nchi vizuri. Ukiangalia hali halisi ya masuala ya sayansi na teknolojia leo ni mambo muhimu sana tena sana na yanahitaji maandalizi mazuri. Lakini tunapoangalia tuna matatizo makubwa na msingi wetu ni mbovu sana.

Mhe. Spika, mara nyingi huwa tunalalamika kwamba hatuna walimu wa sayansi, hatuna walimbu wa hesabu, maabara zetu huko kwenye skuli za kawaida ni mbuvu au hakuna. Kwa kweli tumefika pahali pabaya. Nadhani tungeanzisha msingi imara na tukajitayarisha kwenye elimu ya msingi na sekondari katika masuala ya sayansi. Huko ndio tutakapopata *input* ya chuo hiki. Hatuwezi kuwa huko chini ni kubovu tukaanzisha Chuo cha Sayansi na Teknolojia, sasa *input* tutatoa wapi wakati hawa ambao watakaoingia huko huku ni kubovu, msingi kwanza madhubuti ndio ungeliangalia huko na hili ni jambo ambalo ni la mwanzo.

Kamati ya *PAC* kama wiki zilizopita ilikwenda *SUZA* wakaonana na uongozi pale kwa kweli wanalalamika kwamba ile diploma ya sayansi wanayoitoa huenda ikakwama. Ikakwama kwa sababu fedha kwa ajili ya *laboratory* imekwama hawana na kwa hivyo wanaonekana wanafanya *more theory* kuliko *practical*. Sasa huko ndiko kwenye msingi hapo tunasema *SUZA* hali ni hiyo kwamba ile diploma ya sayansi hawa tungeliwatarajia kwamba watoke wende chini huko kwenye sekondari wakatupikie vijana ambao watakuwa wazuri ama kuingia katika chuo hiki au kwenye vyuo vyengine. Lakini pale *SUZA* wanasema jamani kamati tusaidieni kwani hali ni ngumu. Kwa hivyo, mimi nasema kuanzisha suala hili linaonekana ni zuri kinadharia, lakini linahitaji maandalizi mapana, ya nguvu na yawe makubwa.

Mhe. Spika, mimi nashauri kwamba ni jambo zuri kubadilisha jina kama alivyosema Mhe. Waziri kuwa na vyuo vya elimu ya juu zaidi, lakini maandalizi Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie kwa umakini sana. Kwa sababu tumefika pahali kila mtu analalamika hapa kwamba matokeo ya sayansi yakitoka katika sekondari kila mmoja anajishika kichwa kwamba hali ndio hii. Kwa hivyo, msingi unatakiwa huko, hilo ni la kwanza.

Mhe. Spika, la pili mimi nilikuwa sijui kwamba *FTC* imefutwa pale Mbweni na sasa tunatoa ngazi ya stashahada ya *technical education*. Kwa mtazamo wangu mimi mambo haya mawili ni tofauti sana. Elimu ya *full technician certificate* ni tofauti kabisa na elimu ya *technical education*. Sasa ikiwa tuliifuta tunaweza tukakwama huko mbele, na labda tuangalie mtaala ambao utaweza kufudhu mambo haya mawili. Elimu ya *full technician certificate* inakuwezesha kuchukua *diploma* au *advance diploma* au *high nation diploma* ya *engineering* au *degree in engineering*. Hawa ndio watu ambao wanaweza wakapanda wakachukua *master level* au *PhD*.

Mhe. Spika, nilikuwa naangalia watu wa *technical education* hawa kwa ninavyoelewa mimi labda Mhe. WAziri akija anaweza akanisaidia maarifa zaidi, maandalizi yao ni kurudi kusomesha elimu ya ufundi, sio kuwa wahandisi. Mfano, Mikunguni na Kengeja ukiwa na diploma ya *technical education* unaweza ukawa mwalimu mzuri pale kuliko mtu ambaye ana *FTC*. Kwa hivyo, *FTC* ameandaliwa kuwa muhandisi na huyu ameandaliwa kuwa mwalimu. Kwa hivyo, ukimchukua mtu wa *FTC* ukimpeleka pale Mikunguni kuwa mwalimu unampa kazi ya ziada ya kujifundisha au kujisomea masuala ya mambo ya *psychology* ya kufundisha. Lakini mtu ambaye anasomea *technical education* tayari yeye masuala hayo atakuwa nayo.

Mhe. Spika, mimi nahisi hapa pana mambo mawili tofauti na ikiwa tunaanzisha Taasisi ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia kwa msingi huu wa *diploma* ya *technical education* nahisi tuangalie vizuri zaidi. Nina wasi wasi kwamba elimu ambayo tutaitoa katika chuo hiki inaweza ikawa na mapungufu makubwa katika kufanya *experiment, research* na mambo mengine. Kwa hivyo, hapa namshauri Mhe. Waziri aangalie zaidi mtaala ambao anafundisha katika *technical education* na mtaala uliokuwa unafundishwa katika *full technician certificate* haya ni mambo mawili tofauti ninavyoelewa mimi na kama hatukuyaangalia vizuri tukachupia reli ambalo litatupeleka pahali sipo.

Mimi nilisoma Mbweni miaka hiyo ya zamani *FTC* pia nikasoma *Dar es Salaam Technical College* miaka hiyo, ambapo hapo palikuwa panatolewa diploma mbili, moja ni hii ya *technical education* watu wake walikuwa wanatoka katika watu waliomaliza vyuo hivi vya ufundi, wengine wanapata *grade test* siku zile wamemaliza *form four* wanajiunga moja kwa moja na *diploma* hizi. Watu ambao wanachukua *diploma* ya *engineering* ni wale ambao lazima wametoka *FTC*. Nilipoona kwamba *FTC* imefutwa pale Mbweni halafu inaingizwa *all technical education* nahisi Mhe. Spika hapo pana tatizo.

Mhe. Spika, jambo jengine ni masuala ya vifaa na katika hili ningeliwauliza Wajumbe wa Kamati bila shaka watakuja badala yangu kuja kuzungumza kabla ya wakati wanaupitia huu mswada walipata angalau nafasi ya kukitembelea kile

chuo wakakiona vile kilivyo. Ningeshauri mambo kama haya tusikae hapo juu tukapitisha tu mswada, ilikuwa ni vizuri tupate *visit* ya kwenda kuona hali halisi ya ile taasisi ambayo inataka kugeuzwa kuwa taasisi nyengine. Mimi nadhani kama wangelipata nafasi kamati ama kabla ya kukaa hapo juu wakapitisha vifungu hivi vya mswada wakenda pale Mbweni wakakiangalia kile chuo kilivyo, wakapitia madarasa, wakapitia *laboratory*, wakapitia *workshop* zilivyo sidhani kwamba wangelikubali katika hali kilivyo kuanzisha kama ni taasisi ya sayansi na teknolojia.

Mhe. Spika, mimi naomba Mhe. Waziri akija anisaidie maelezo kwamba tumejiandaa vipi na suala hili. Mhe. Spika, wenzetu wanaoamua kuanzisha mambo kama haya huwa wanajitahidi kufanya maandalizi mazuri hawakurupuki haraka haraka wanafanya *enough preparation*. Hili ndio ambalo tunamuomba Mhe. Waziri najua nia yake ni nzuri, lakini naona amekuja na kasi mpya na ari mpya. Sasa mambo ya kasi mpya na ari mpya ni mazuri lakini yanataka maandalizi mapya nayo bila ya hivyo kasi yake na ari yake anaweza akajikwaa visiki akaanguka, na hili itakuwa hakuanguka yeye ametuangusha sote.

Mhe. Spika, tunahitaji chuo ambacho kitaisaidia Zanzibar kiteknolojia na kiufundi. Wataalamu wengi tulionao sasa hivi tunawaagiza kutoka nje, vijana wetu wamepoteza ari ya kusoma masomo haya, wengine wanaingizwa Mbweni basi wanatoka wanatafuta masomo ya *art* wanasoma. Hii maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba vijana wamepoteza ile ari na moyo wa kusoma haya masomo. Vijana wanafaulu vizuri katika hizi sekondari za ufundi, lakini ukimpeleka pale anakwambia mimi bwana bora niende Lumumba, mimi bora hata nipatiwe nafasi nyengine kwa sababu hana ile hamu, hapa mimi nasema kuna tatizo. Kwa hivyo, hili nalo linataka kufanyiwa kazi na juhudi kubwa vyenginevyo tutakuja kuibiwa kwa sababu nchi ambayo haiwezi kujitosheleza katika masuala ya teknoloji kwa kweli hulazimika kuagiza wataalamu kutoka nje na wataalamu wakija nje hapa ni rahisi kutuibia mambo mengi tu. Kwa hivyo, hili ningemuomba sana Mhe. Waziri katika hilo.

Mhe. Spika, mimi ningemshauri kwamba mbali ya fedha ambayo alieleza kwamba humu itapatikana lakini awe na taratibu wakiwakaribisha serikali kuu na serikali za mitaa na wafadhili wengine kutoa ruzuku kwa chuo. Kwa sababu bajeti ya serikali inayopitisha hapa haitaweza kuisaidia taasisi hii, lazima kuwe na mpango mwengine ama wa serikali kuu, serikali za mitaa au taasisi nyengine lakini kuwe na utaratibu lazima wapate fedha za ziada kuanzisha shughuli hizo.

Mhe. Spika, fedha hizo zinahitajika katika kuanzisha miundombinu, maabara kwani inahitajika sana maabara katika masuala haya *research*, *experiment* na

mambo mengine mengi ni muhimu mno. Sasa kama hatukujiandaa hivyo basi tutafika pahala tutakwama sana. Mara moja nilipata rafiki yangu mmoja Mhe. Spika anatoka Pakistan yeye ni muhandisi nikamuuliza umesomea chuo gani? Akaniambia nimesomea chuo kimoja kinaitwa *Buto Institute of Science and Technology*. Katika maelezo yake nikahusudu namna kile chuo kilivyowekwa na labda kwa kumsaidia rafiki yangu Mhe. Waziri nimpe tu kidogo mawili matatu ambayo labda yanaweza kumsaidia naye kuona kwamba taasis anayoanzisha angalau itusaidie.

Kwanza ni chuo ambacho kinategemewa kwa *research finding* pale Pakistan. Pia ni chuo ambacho kinashughulikia *skill training* ya Pakistan. Ni chuo ambacho kinasaidia *research* ya *renewable energy*. Ni chuo ambacho kinasaidia *science and laboratory equipment* watu wote ambao wana matatizo wakifika pale huwa wamemaliza matatizo yao. Ni chuo ambacho kimeanzisha na kinaendeleza *computer and design.* Ni chuo ambacho kimeanzisha na kinaendeleza *proto type manufacturing and testing.* Ujue Wapakistan wameanzisha na hivi sasa ni taifa pekee la Kiislamu ambalo liko katika mambo ya *nuclear program*. Kwa hivyo, hata hiki chuo *laboratory* zake, *experiment* zake na *station* zake nayo ni sehemu ya mafanikio hayo ya nchi ya Pakistan.

Mhe. Spika, kwa hivyo dhana ya Mhe. Waziri ya uanzishaji wa taasisi hii sio mbaya, lakini maandalizi yake na hofu hayajakuwepo. Ili tufanikiwe lazima kabisa kuwe na maandalizi ambayo yataonekana hasa kile chuo kilianzishwa mwaka huo 1966 ni kweli, lakini ni kwamba hakijabadilika sana. Ukiangalia majengo yake ndio yale yale, ardhi yake inapungua na sisi Baraza ni sehemu ya hilo ya kupunguza ile ardhi kwa hiyo inatakiwa kuonekane kwamba pana *facility* ambazo zimeanzishwa ambazo tunakwenda nazo katika dhana ambayo tumekusudia. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa pili baada ya mchangiaji wa kwanza ambaye ni mchangiaji baada ya wachangiaji wakubwa. Mhe. Waziri mwenyewe, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati na Waziri Kivuli.

Mhe. Spika, mimi Chuo cha Ufundi cha Karume nimebahatika kuwa mwanafunzi katika chuo hicho kwa muda wa miaka minne. Vile vile nimebahatika kuwa mwalimu katika chuo hicho. Nilikuwa mwanafunzi kuanzia mwaka 1973 mpaka 1976 na nilikuwa mwalimu kuanzia mwaka 1981mpaka 1983. Kwa hivyo, kwa kiwango cha kutosha na katika kipindi hicho Chuo cha Karume nakifahamu sana. Chuo hiki kina historia ndefu na sisi tulivyoelezwa ni kwamba chuo kile kilijengwa kwa msaada wa Serikali ya Wamarekani. Ni kweli kwa sababu hata sisi tulipoingia wakati wenzetu wengi walishaingia chuo hiki, basi kila kitu kilikuwa na nembo ya inayoonesha kwamba Marekani kama

serikali ndiye ambaye alikuwa ndio *Chief Dollar* kuanzia vitabu, vifaa na mambo mengi tu.

Wenzetu tuliowakuta pale walitueleza kwamba wao walipoanza basi kwa kweli hawakujiona kwamba kweli wako katika chuo kilichoko Zanzibar, walijisikia kama vile wako katika chuo kilichoko Ulaya au mahali nje ya Zanzibar kwa namna ambavyo walivyopokelewa, walihifadhiwa kimalazi na chakula lakini zaidi kimafunzo kwani kulikuwa na walimu wa kutosha. Kwa siku hizo wenzetu walitwambia kwamba ni wale ambao wana *special talent, special brain* ambao walipelekwa katika Chuo cha Ufundi cha Karume, *product* ya wale tunaiona sasa hivi.

Mhe. Spika, lakini chuo kile tulitegemea kwamba kingekuwa ni chuo kinachoendelea kila siku. Ukilinganisha na hali ya sasa hivi kwa kweli kimepoteza taswira ambayo ilikuwa nayo hapo awali. Mimi na wenzangu mwaka 1973 chuo kile wakati wa kula ilikuwa huruhusiwi kula kwa kutumia mkono ni kijiko, umma na kisu. Siku moja wakati tunakula kulikuwa na *Supervisor* Mhe. Spika, mwenzetu mmoja wakati tunakunywa chai alichukua mkate wake ameshazoea kwao shamba, basi ilikuwa huruhusiwi kuchukua mkate ukauchovywa kwenye chai.

Ulitakiwa uchukue mkate wenye siagi kushoto unakamata kikombe cha chai na kulia una kipande cha mkate, unakula halafu unakunywa chai. Sasa mwenzetu mmoja alikuwa ameshazoea mazingira hayo ambayo tumezoea, akachukua mkate akauingiza mle kwenye chai muda haujapita *Supervisor* wakati anapita akaona kwenye kikombe hakuna chai na kate limevimba. Aliulizwa na watu walivyokuwa na heshima siku hizo mpaka mwanafunzi alikuwa anaitwa *mister, Mr. so and so where is your tea* akamtazama anatetemeka akasema *its under braid Sir*. Basi alichezea konzi tukamuonea huruma na sote pale tukaona kwamba sasa kazi imeanza, basi hakuna aliyesahau tena. Mimi naeleza vile ambavyo kilianza chuo hicho na mpaka itafikia hali kwamba hiyo chai huipati, huo mkate haupo mkibahatika katika mwaka 1976 bado ni mwanafunzi basi maharage ambayo mnapikiwa nusu ni wadudu na nusu ni maharage.

Mhe. Spika, ni kwamba mambo yanabadilika lakini ninachokusudia kusema kwamba ingekuwa *trained* ile tuliyoanza nayo ilikuwa inapanda, basi mimi mswada huu ningeuunga mkono mia mbili juu ya mia kwamba tumefika mahali kuwa *Karume Technical Colloge* kugeuzwa kwa sheria maalum kuwa *Karume Institute of Science and Technology.*

Mhe. Spika, katika hali hiyo mimi nasema hilo ni upande mmoja lakini twende kwenye mafunzo halisi. Tulipokuwa wanafunzi tulikuwa na walimu wa kutosha, serikali ilikuwa na mpango maalum benchi yetu ya kwanza wanafunzi

pale tulitoka wanafunzi kumi na nne, tukenda Chuo Kikuu 1977-1978 wote masomo ya *engineering* ukiachilia mbali ambao walikwenda katika taasisi nyengine. Bahati nzuri katika wanafunzi kumi na nne kumi na mbili tukatoka pale na *degree* ya kwanza. Wengine Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakaona ni vizuri wa-*retain* wafanye *masters* na *PhD* na kuendelea. Lakini bado hao Serikali ya Zanzibar ikasema hapana tuna upungufu wa walimu Karume na kwa hivyo wengine ambao walikuwa tayari wameshakuwa *retained* ikabidi warudi basi tulirudi pale kufundisha. Tulikuwa walimu kumi na mbili wote ambao tulitoka pale basi mmoja wao nilikuwa mimi.

Mhe. Spika, pale tulijaza pengo kama lilikuwepo la walimu, wanafunzi ambao tulianza nao zamani *FTC* kwa sababu ya walimu wazuri, basi ilikuwa ni nadra mtu kukosa *FTC*. Lakini rekodi zipo benchi yetu ya kwanza iliyotoka sisi kama tukiwa walimu tulitoka pale asilimia 86 ya wanafunzi walipasi na ndio hao waliokwenda Chuo Kikuu cha Ardhi na mahali pengine. Naelezea umuhimu wa chuo kama kile kuwa na walimu, lakini tumefika mahali mimi kama mwanafunzi na mwalimu wa chuo kile, basi tulifika mahali *department* nzima ya *civil engineering* ambayo mimi *profession* yangu ilikuwa na mwalimu mmoja. Masomo zaidi ya matano ukiachilia mbali *mathematics* lakini kuna *engineering science*, *engineering drawing*, *structures* na mengine hayo na mwalimu ni mmoja tena mwalimu wenyewe amemaliza pale pale si hata kwamba anatoka Chuo Kikuu kufundisha.

Mhe. Spika, mimi naonesha kiasi ambacho hiki chuo kilivyoanza na kilivyokuwa kinateremka na kupanda. Sasa hivi sijui hali ikoje lakini siamini kwamba hali ni nzuri kiasi ambacho yakutaka kuvuka kizingiti chengine. Mimi nasema kuanzisha kitu chochote sio vibaya, lakini na sisi wenyewe tujiangalie hivyo kweli tukianzisha chuo hiki tuna nguvu ya chuo hiki maana yake hili jina ni kubwa *Karume Institute of Science and Technology*. Wale wenzetu iliyokuwa *Dar es Salaam Technical College* wao sasa hivi inaitwa *DIT* (*Dar es Salaam Institute of Technology*) sayansi hawajaiingiza kwa nini? Kwa sababu ni mzigo mkubwa sio mchezo, sasa wale ambao wana *all facilities* wamekuwa wakitoa *FTC*, wakatoa *oral diploma*, wakatoa *diploma*. Wao wamechukua *institute* of *technology*, sisi tutachukua *science and technology* jamani tafsiri yake tunaijua, upana wake tunaujua au tunaujua kwa tafsiri yetu sisi tu hatuangalii na wenzetu wengine duniani watatafsiri vipi.

Mhe. Spika, kwanza mimi nilikuwa nashauri hili jina ni kubwa mno katika hali tuliyonayo na naamini itafika kwa sababu haya mambo ni endelevu ilikuwa *Karume Technical College* inaweza ikawa *Karume Institute of Technology* tukiona kwamba nguvu ni nzuri basi tukaongeza na sayansi na mambo mengine yote. Lakini tukate kitambaa tushone koti kwa mujibu wa kitambaa tulichonacho. Kwa hivyo, mimi nilikuwa napendekeza sana jina lifikiriwe upya

kama mtachukua sayansi peke yake au teknoloji peke yake, lakini mimi ningependelea iwe *Karume Institute of Technology* sayansi ni mambo makubwa.

Amesema hapa Mhe. Said Ali Mbarouk kwamba dhana za kufanyia mambo hayo hazipo na kwa hali ilivyo hivi sasa. Nasema tena kwamba hili koti ambalo tunataka kulishona na kulivaa kitambaa tulichonacho hakitoshi na hatuna walimu hivi sasa. Pia hali ya masomo Karume ni mbaya kupita kiasi wanafunzi wengine hivi sasa wanashindwa kuendelea hata mwaka wa pili au wa tatu kwa sababu ya hali ngumu ya mafunzo. Humu imeelezwa vizuri kwamba hii itakuwa ni taasisi, sasa hivi ni chuo kinaendeshwa na serikali, pamoja na kwamba kinaendeshwa na serikali lakini bado wanafunzi wanachangia. Huo mchango mdogo wanaochangia basi wengi sana wanashindwa hata kuendelea na masomo na wengine wanaahirisha. Leo unaitoa huko mzigo huu unataka kutwikwa watoto wa wanyonge na masikini hivi kweli tutafika.

Mhe. Spika, jina ni kubwa kwa sababu kitakuwa kinajitegemea japo kutakuwa na ruzuku ndogo ya serikali lakini mategemeo makubwa ni *school fees.* Hizo *school fees* waheshimiwa hapo *DIT* wale walimu wa *part time* basi malipo wanaolipwa sio ya mchezo maana yake lazima uwe na *incentive* ya kumtoa mtu anapofanya kazi. Pengine ni Mkurugenzi wa Taasisi Serikalini lakini anaona hapana kwamba saa kumi na mbili nina kipindi, kwa hivyo ile *payment per hour* ndio inayomvutia yeye kuacha shughuli nyengine baada ya kazi akaelekea chuoni, vyuo kama vya Tunguu wanafanya hivyo, Chwaka wanafanya hivyo, Chukwani wanafanya hivyo, sisi tutamudu? Tusije tukafika pahali tumeanzisha jambo halafu ikaja ikawa tunaona aibu. Jina nasema bado ni kubwa, hali ya chuo kile sasa hivi ni kama hiyo na pengine kuna zaidi ya hiyo mimi siyajui sana yaliopo sasa hivi, lakini najua kwa sababu na mimi baadhi ya wanafunzi wananijia, tunazungumza, tuna-*disscus,* tunafakari hali ya wanafunzi ni mbaya. Je, waheshimiwa hili litawezekana?

Mhe. Spika, hiyo ni *general comment* kuhusu kuanzishwa kwa chuo hiki. Narudia tena si vibaya kuanzisha jambo lolote, lakini tuangalie tunaanzisha hapa tunatoka wapi. Tulitoka wapi, tukenda wapi.

Jengine ni hali halisi ya chuo kilivyo. Ukiingia kwenye mswada wenyewe mimi naamini kabisa kwa sababu mswada huu umeletwa, basi utapita tu pamoja na marekebisho madogo madogo.

Nilikuwa naangalia hizi *version* bahati nzuri tumepewa nakala ya Kiingereza. Nakala hii ya Gazeti Rasmi ambayo jana ilizungumzwa kidogo namna ambavyo makaratasi yameandikwa, lakini Mhe. Naibu Waziri Kiongozi ali-*confess* kwamba kweli *quality* ya maandishi na hata karatasi zenyewe na vitu

vyengine katuahidi kwamba hili halitatokea tena. Lakini nasema ukilinganisha haya mawili ukifungua ukurasa wa Kiingereza 309 na ukifungua ukurasa wa Kiswahili 221 kifungu nambari 6 kuna a, b, c katika Kiswahili na katika Kiingereza kuna a,b,c sasa mimi niko kwenye c kote kote.

Kifungu c cha Kiingereza kinasema:

> " *Five members who shall be appointed by the Minister, after the consultation with relevant institutions as follows"*.

Hapo zimeorodheshwa moja, mbili, tatu, nne, tano kwenye Kiingereza lakini Kiingereza hicho hicho kuna d ambayo kwenye Kiswahili hakuna. Kwenye Kiswahili kuna c(i), c(ii), c(iii) mpaka c(viii). Sasa hili kwa sababu huu mswada ni mmoja na tumeambiwa kwamba wa Kiingereza hutafsiriwa kwa Kiswahili au wa Kiswahili hutafsiriwa kwa Kiingereza hapa wanaotafsiri kidogo wametuchanganya. Kwa hivyo, hii Mhe. Waziri naona aiweke sawa.

Chengine ambacho nilikuwa nazungumzia ni hizi taasisi ambazo zitakuwa *consulted.* Mwaka jana tulipitisha sheria hapa ya kuanzisha bodi ya wahandisi, kusanifu majengo wakati yale majengo *contractor* miswada miwili ilipita. Sasa ukizisoma kote kwenye Kiingereza na Kiswahili hii ni *institute of technology (underline* neno *technology)*. Humu nilifikiria kwamba watungaji wa mswada huu wangeifikiria ile taasisi ambayo sisi tumeianzisha hapa kwa sheria maalum. *When you talk of engineers* ndio ile teknolojia tena. Kwa hivyo, nashauri kwamba pamoja na hawa wanane waliotajwa, basi tuongeze na mmoja katika taasisi itakayoshauriwa ni nani anafaa na nani hafai,, basi nafasi hii nayo iongezwe.

Mhe. Spika, jengine ni hali halisi ya chuo kimajengo. *SUZA* ime-*observe* vyuo vingi tu hapa, kuna chuo ambacho ni maarufu duniani kote kwa jina la *Nkrumah Teacher's Trainning College*. Sasa hivi baada ya kuanzishwa *SUZA that name is almost dead,* chuo kile historia yake nyinyi mnaijua zaidi lakini *all over the world* walimu karibu wote wa nchi hii na wa nchi nyengine wametoka pale, lakini *SUZA is absored everything* na sasa hivi.

Chengine Chuo cha Kiislamu kipo, lakini nasema kipo jina sivyo kilivyokuwa na huko tutakakokwenda sivyo kitakavyokuwa. Mimi sikatai mabadiliko, lakini ule uasilia naupenda sana, ukiisahau asili itakukumbusha.

*SUZA* imekuwa hivyo kwa sababu imejikuta imeanzishwa majengo haina, sasa basi mkubwa ameze mdogo sijui baada ya kujengwa Chuo Kikuu kipya kwa jina la *SUZA* huko Tunguu kama inavyosemekena na namuomba Mwenyezi Mungu ajaalie iwezekane, sijui kama taasisi hizi zitarudi tena kama uasilia

wake, yaani *Nkrumah Teacher's Trainning College* na Chuo cha Kiislamu, naamini kuna na vyengine kama Chuo cha Uchumi.

Hili nasema tena Karume kwa majengo yaliyokuwepo na jina hili kubwa taasisi hii mimi nasema tuoneni fahari kuanzisha jambo na watakapokuja watu wakatwambia basi twende tukaone *infact* sisi tuwaambie wakaone kabla ya wao kutwambia huo ndio ufahari wa jambo, isifike mahali kwamba wanataka kwenda *Karume Institute of Science Technology* ukasema maana yake hivi, ratiba haioneshi hivi yaani unakinga.

Mimi naona kwa majengo yaliyopo pale hali hiyo inaweza ikaja, unakwenda kumwonesha nini? Sasa taasisi inaweza kuanzishwa, lakini nasema eneo la pale ni kubwa tusianze na kutoa jina na kuanza kazi, lakini vile vile tuangalie hiki chuo na hadhi na jina hili kitafanana kweli? Mimi nashauri tuwe na kidogo lakini kizuri kila mtu akipende kuliko kuwa na kikubwa lakini hakina maana hiyo ya ukubwa.

Mhe. Spika, mimi kwa leo huu ndio uliokuwa mchango wangu nakushukuru ahsante.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi katika siku ya leo ya Ijumaa kuchangia kidogo kuhusiana na mswada huu. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai na uzima na kupata kauli ya kuzungumza. Labda leo nitaanza vyengine Mhe. Spika.

Naomba nianze kwa kumpongeza sana rafiki yangu, mwalimu mwenzangu, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Baada ya muda mrefu kuzungumza hapa Barazani kuhusiana na jengo la Maktaba nafurahi sasa hivi kupita pale nikaona milango iko wazi. Kwa hivyo, tunamuomba sasa atufanyie ufunguzi rasmi ili taifa lijue kama maktaba ile imefunguliwa.

Baada ya hayo nije katika mswada wenyewe. Kwa kuwa taasisi inayoundwa ni ya elimu lazima itoe ukweli halisi ulivyo. Kwa sababu tunashuhudia vichwa vya habari vya magazeti au matangazo ya maduka, lakini ukienda utaona sivyo ilivyo, ni ule ukubwa wa lile tangazo au ukubwa wa kichwa cha habari, lakini ukisoma utaona kauza gazeti au kauza tangazo. Sasa mimi kama ni mwalimu wenzangu waliotangulia kusema kwamba kuna *science* siridhiki kabisa kwamba kuingizwa *science* wakati si kweli kwamba panasomeshwa au patasomeshwa *science*.

Matawi mawili haya ni tofauti, ukisema *science* ina maana kwa lugha ya kigeni tutasomesha *pure science* yaani *biology*, *chemistry*, *physics* kwa maneno ya waziri mwenyewe alipokuwa akitoa hotuba yake ya kuwasilisha mswada, alitoa

historia ya chuo kile na akasema kwamba hatua hii ya kuanzisha taasisi sasa hivi ni kukikuza hiki chuo na hakutumia hata mara moja kubadilisha. Sasa katika kukikuza chuo kile na ni cha ufundi nategema kwamba itakayokuzwa ni ile elimu ya ufundi. Kwa hivyo, jina sahihi hasa la kwamba mtu ukienda pale hatokuuliza swali jengine litakuwa ni taasisi ya teknolojia. Hili ni jina halisi ikiwa tunataka kweli kusema ukweli la kama tunataka kupachikiza.... Mhe. Spika, naoma radhi.

Ikiwa tunataka kupachikiza jina basi huenda tukaja tukagundua katika ulimwengu wa leo ambao tunaita wa utandawazi katika kuandika zile *paper* za mambo yetu itabidi tupate na masuala mengine. Je, sayansi kweli inasomeshwa pale na sasa tumeshaipokonya *SUZA* na vyuo vyengine kusomesha sayansi pale?. Kwa hivyo, ilivyokuwa ni *speciality* yake ni teknoloji au elimu ya ufundi, basi tuite Taasisi ya Teknolojia.

Kabla sijaingia ndani ya maudhui yenyewe naona sifa na majina yamechanganywa kidogo, tunapata jina Hospitali ya Abdalla Mzee na Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, kuna lile neno lenyewe na sifa yake, lakini hapa kidogo pamechanganywa tunapata neno halijatimia taasisi, haijatimia imewekwa Karume halafu mwisho sayansi na teknolojia. Ni kwamba ilikuwa lile neno taasisi litimie kabisa kwamba Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume au Taasisi ya Teknolojia ya Karume kama ninavyopendekeza mimi. Lakini hii ni kuchanganya na kuchukua yale maneno ya Kiingereza tukayatia moja kwa moja bila ya kuzingatia Kiswahili chetu kinavyoandikwa.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo mimi nasema kuanzishwa au kuendelezwa kwa vyuo ni jambo ambalo linakwenda na wakati, wakati wenyewe unadai ingawa waziri alishindwa kueleza madhumuni hasa ya kuanzisha. Je, tuna shida ya wataalamu, upungufu wa wataalamu, tuna kitu gani kilichojitokeza? Lakini la pili hiki ni chuo kinachopandishwa daraja na kuwa taasisi ya teknolojia au taasisi ya sayansi na teknolojia. Chuo hiki kinataka kuchukua kutoka chini lakini jambo la kusikitisha kwamba hivi vya chini havishughulikiwi. Kwa mfano, miaka kumi au zaidi iliyopita kilianzishwa Chuo cha Ufundi kule Kengeja mpaka leo limebakia lile jina tu Chuo cha Ufundi, lakini hata *screw driver* hawana, hata patasi hawana, *tester* ya umeme hawana. Sasa kwa kweli inatushangaza kwamba tunapandisha daraja, lakini hatutayarishi zile nyezo za hawa wanaotoka huku wakenda kwenye daraja ya juu.

Kwa hivyo, kabla Mhe. Waziri hajatayarisha chuo hiki basi avitayarishe hivi vyuo ambavyo vitachukuliwa kule, cha Kengeja, Mikunguni, Gulioni, hivi vilikuwa vitayarishwe ili viweze kuwa na *out fit* yao ndio *in put* ya chuo hicho, lakini kutayarisha chuo kikubwa wakati vidogo vidogo havina nyezo, havishughulikiwi kwa kweli ni jambo ambalo linatushangaza kidogo.

Jambo jengine ambalo napenda kulizungumza ni malengo. Je, tuna malengo ya kutoa wanafunzi au vijana waliohitimu katika kiwango gani? Leo Mhe. Waziri alipokuwa akijibu baadhi ya maswali alisema kwamba wanalazimika kupeleka wanafunzi wengi kuliko uwezo wao kwa vile wengi walipasi. Lakini na hivi vyuo tunavyovitayarisha vitachukua wanafunzi zaidi ya uwezo wao kuliko vinavyoweza? Je, ile elimu itakayotolewa pale itakuwa ina kiwango? Sasa anapoona kwamba bajeti yake ni ndogo basi naona njia zipo, kuna njia kama tatu za kuongeza bajeti. Kwanza ni kuja katika Baraza na kuomba *supplementary budget,* mimi sijaisikia wizara hii tangu mwaka nilioingia hapa kuja kuomba *supplementary budget*. Pili ni kupunguza matumizi hususan katika sherehe.

Kwa hivyo, ikiwa wizara iko *serious* katika kuleta mabadiliko katika elimu na kuzidisha miundo mbinu katika elimu, basi wangeishauri serikali ikapunguza ukubwa wa sherehe kutokana na uwezo wetu, tukafanya sherehe kwa uwezo wetu si kulazimisha kufanya sherehe kubwa ambazo hazimo ndani ya uwezo wetu. Hilo jengine.

Mhe. Spika, tuje katika huu mswada wenyewe. Mimi nitausoma huu wa Kiingereza kwa sababu huo wa Kiswahili siuoni.

Kifungu Nam. 4:

> *"The institute may in exercise of its functions associate with college or institution which offers courses in science and technology, either inside or outside Zanzibar"*.

Mhe. Spika, kifungu cha tano vile vile zimetajwa *science*, *science*, *science*. Sasa ilivyokuwa Mhe. Waziri kazitaja ndani ya maandishi ningelipenda akija hapa katika majumuisho yake atueleze hasa kaipangaia vipi hii *science?* Itasomeshwa kweli au imeingizwa tu humu katika chuo chenyewe? Hilo nilitaka nilizungumze.

Jengine kwa vile Mhe. Waziri kaleta mswada ilikuwa katika hotuba yake pamoja na kwamba humu katika mswada haikuandikwa atueleze angalau huu mswada ukishapita hapa ukawa sheria kwa mipango ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ingeanza lini? *Immediately* baada ya kupita tu hapa au mwaka mmoja baada ya hapo na mipango yake anayoipanga ili kupata walimu? Kwa sababu pale pana wanafunzi tayari wameingia kwa *qualification* za *Karume Technical College,* sasa inabadilishwa kuwa *Karume Insitute* hivyo *automatically* wao watakuwa ni *Karume Insititute* au *Karume Technical College* wataendelea mpaka wamalize muda wao?

Hapa Mhe. Waziri bahati mbaya hakutueleza ule mpango wote ili wale wanafunzi na wao wajijue kwamba watakuwa wameshaingia katika *Karume Institute Technology and Science* au *science*. Mambo haya ni muhimu sana kwa sababu katika elimu wanataka vyeti wale wakitoka, sasa cheti hicho wakitoka kwa mfano tumepitisha sheria sisi hatukusema kwamba itaanza kutumika kipindi fulani, kwa sababu sheria kupita ni sehemu moja na kutumika ni sehemu ya pili, lakini kama sheria haikusemwa kwamba itatumika katika kipindi fulani je, watu wakitoka vyeti vyao vitakwenda wapi? Vitakwenda kwenye ule ule muhuri wa *Karume Technical College* au *Institute* wakati sisi tumeshapitisha na chuo ndio kile kile kimeshakuzwa? Itakuwa ni halali kuwapa cheti cha *Karume Technical College* wakati Baraza limeshapitisha kwamba ni *Karume Institute?* Wao wakidai kwamba wapewe *Karume Institute* itakuwa ni halali kwao kupata? Kwa hivyo, ni muhimu sana kutajwa mambo haya ili yawe wazi na yakawa ya kisheria.

Kwa mfano, hapa pametajwa *NECTA* kwamba ni bodi au ni chombo kinachosimamia vyuo hivi, navyo wanataka kujua hii imetolewa kwa kiwango gani? Hawa wanafunzi waliopo kweli wana kiwango hicho cha kuwa katika *institute* au shahada iliyopo. Sasa ni kwamba mambo mengi ambayo ya kuanzishwa *institute* hii yamefinywa finywa na kwa kweli kwa sababu chuo kipo ingelikuwa kuanzishwa chuo kipya kama vile vyuo vyengine vilivyokuja hapa ingelikuwa ni rahisi, lakini sasa hivi chuo kipo lakini kinataka kukuzwa kwa hivyo mambo yake badala ya kuelezwa ile historia tu inaelezwa na ile *prospect* ya kile chuo kilichopo vipi kitakuwa *phase*d *out* na mambo ambayo yatalingana na hapo.

Tukienda katika mswada wenyewe hapa katika vifungu vya sita uongozi wa chuo, sasa *council* ya Baraza lile unasema kuna chombo hapa kinachoitwa Chombo cha Wafanyabiashara, sasa haikutajwa kwamba inatokana na chombo hicho au *business community* maana yake ni mfanyabiashara yeyote atakayeteuliwa. Kwa sababu chombo chao wanacho kwa hivyo ilikua kitajwe kwamba kitatokana na *Chamber of Commerce.* Kutokana na mfumo mpya wa ulimwengu unatakiwa kuwe na ushirikiano baina ya Taasisi za Kiserikali na Taasisi za Binafsi. Kwa hivyo, hawa kuandika tu kwamba *business Community* mimi nafikiri haitoshelezi, kwa sababu inawezekana ikawa ni kitu cha binafsi akachaguliwa mtu binafsi. Lakini madhali chombo cha *chamber* kipo, basi inatajwa *a member from the Chamber of Commerce*, memba kutoka chemba ya biashara hiyo.

Halafu neno ambalo sikulifahamu katika kifungu hiki ni hapa aliposema *member from employers association.* Kuna mbili hapa sasa hivi kubwa, kuna hii ya wafanyakazi kuna na ya walimu ipi iliyokusudiwa? Kwa sababu hiki ni chuo kwa hivyo, watachukua ipi ya wafanyakazi au watachukua ile ya walimu

kutokana na yenyewe? Kwa sababu lazima itajwe wazi wazi imo ndani ya sheria kama watachukua ile ya wafanyakazi moja kwa moja au watachukua ile *special* ya walimu.

Mhe. Spika, mwisho mimi sina mashaka ya kusema kwamba tunaanzisha au tunakiendeleza chuo, lakini kunatakiwa kutokezee mabadiliko yaani *parallel development* katika kila hali. Fani ya ufundi ni fani ambayo sisi Zanzibar ingetusaidia sana kupata wataalamu tena wazuri, kwa sababu sisi ni nchi ndogo na ukiangalia katika ulimwengu wa leo wataalamu wa kiufundi wana nafasi kubwa sana. Kwa mfano, Ujerumani ni nchi ambayo ni ngumu sana kupokea wageni, lakini katika kipindi cha karibuni iliamua kwa makusudi kabisa kwamba wataalamu kutoka India na kwengineko wanawachukua kwa wingi tena katika fani za kompyuta na mambo mengine.

Inaonesha kwamba hii fani ya kiufundi kiteknolojia ni fani ambayo inaweza ikatusaidia sana kutoa wataalamu ambao sio kutusaidia ndani tu, hata nje ya nchi. Kusaidia nje ya nchi haina maana kwamba wao watakwenda kutafuta *green pasture*, hii inawezekana ni mpango maalum wa serikali utakuwa wa kuwapeleka wataalamu kama tunavyoagiza sisi kutoka nchi nyengine na sisi tunaweza kupeleka wataalamu kwa mikataba maalum wakafanya kazi katika nchi zile na wakatuletea manufaa. Lakini tofauti na *field* nyengine, *field* ya kiufundi inataka itayarishwe kwa zana.

Mhe. Spika, sisi tulipokuwa tukisoma tunakumbuka kwamba wale watu wanaosoma masomo ya *art* tulikuwa tukiwaita ndege, kwa sababu kuna ndege fulani wanaitwa *penguin*, wao kazi yao vitabu tu hawagusi kitu chengine. Mimi ndio nastaajabu hata hivi vyuo vya sasa tulivyonavyo kidogo vina matatizo. Nakumbuka tulipokuwa Chuo Kikuu tukisoma *science* tulikuwa muda wa masaa sita kwa kila wiki tunaingia *laboratory* kuanzia saa tano mpaka saa kumi na mbili jioni mfululizo, kwa sababu palikuwa na muda wa saa moja ya kwenda kula ile ilikatwa, saa saba mpaka nane tunakwenda kula halafu tunarejea tena. Sasa mimi huwauliza hawa vijana wanaosoma siku hizi kweli nyinyi mnapata saa hizo? Wakati si mbali tuliposoma sisi ni hapo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam miaka ya 1978 mpaka 80.

Kwa hivyo, kama sisi wenyewe tulivyopata ile elimu na sisi tuwatayarishie vijana wetu elimu angalau iliyofanana na ile tusiite majina tu Chuo cha Teknolojia, lakini zana hakuna. Kwa hivyo, tujitayarishe na mapema.

Mhe. Spika, mimi wito wangu ni huo kwamba wizara ijitayarishe na mapema, ikiwaita wanafunzi sasa ingieni wajue kuwa kweli tunaingia chuoni.

Siku moja hapa nilitoa mfano ukawa *repeated* juu ya jukwaa kwamba haitokuwa hivyo msumeno mmoja unaazimwa kila skuli ikifika siku ya mtihani leo uko Makunduchi, siku ya pili uko Paje, ya tatu uko Jambiani, msumeno mmoja huo huo ndio kama tunavyoazimana *burette* sasa hivi. Ikifika siku ya mtihani *burette* moja inatafutwa Utaani, moja inatoka Mkoani zikusanyike, haya Mhe. Waziri yamalize tena. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe nawashukuruni nyote. Kunagawiwa barua za semina inayohusiana na masuala ya bima, tayari wametayarisha mifuko ambayo ndani yake mna makabrasha mtayapata hapo *reception* kuhakikisha kila mjumbe amepata kabrasha lake.

*(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**Mhe. Naibu wa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuweza kuhudhuria kikao hiki jioni hii.

Baada ya hapo Mhe. Spika, napenda nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuwa mchangiaji wa mwanzo jioni hii katika mswada huu ulio mbele yetu. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kwanza kabisa, Mhe. Spika, napenda kumshukuru Mhe. Waziri kwa kuwasilisha mswada wake huu kwa makini kabisa na umeandaliwa vizuri na unajitosheleza. Lakini vile vile nawashukuru watendaji wake ambao wamemsaidia katika kuhakikisha mswada huu umeletwa na umeeleweka.

Baada ya hapo pia nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati kutokana na hotuba yake aliyoitoa imekuwa dira na kielelezo na ufafanuzi mzuri juu ya mswada huu

Mhe. Spika, nikianza na mchango wangu nianze na kifungu hiki cha 3: 2 (g) kinachoeleza kuwa:

" Uwezo wa kutoa vyeti na stashahada pamoja na kushirikiana na taasisi nyengine za nje na ndani ya nchi yetu".

Mhe. Spika, madhumuni ya maelezo haya ni kwamba bila shaka chuo chetu hiki kitakuwa kinatoa vyeti ambavyo vinatambulika ndani ya nchi lakini na vile vile nje ya nchi kwa sababu ya mahusiano hayo ambayo yameelezwa. Mategemeo yetu kwamba tutakuwa na walimu ambao watatoka nje ya nchi kuweza kusaidia pale ambapo patahitajika.

Mhe. Spika, kumekuwa na maelezo mengi ya baadhi ya Wajumbe wale ambao pengine wameunga mkono moja kwa moja na wale ambao wamekuwa na wasi wasi pengine juu ya kuletwa kwa sheria hii ya kuanzishwa hiki chuo.

Mhe. Spika, kwanza kabisa mambo haya ya maendeleo inatakiwa kuwe na sheria na baada ya kuwa na sheria na kuanzisha jambo unakusudia kulifanya na hapo ndio mambo mengine yote yatakuja kidogo kidogo. Kwa hivyo, mimi nataka kuwakumbusha Waheshimiwa Wajumbe kwamba tusiwe na wasi wasi juu ya uanzishwaji wa chuo hiki. Kwa sababu leo hii kama tunataka kuomba misaada mbali mbali ambayo itawezesha kuendesha chuo hiki kama hatujaanzisha na hata hiyo sheria yenyewe hatuna sasa sijui tutaanzia wapi.

Lakini kwanza vizuri tuanze na baada ya kwisha kuanza basi tutajua kwamba kuna mapungufu gani na yale mapungufu yaliopo kwa kushirikiana na wenzetu wa nje na ndani basi tunaweza kupata msaada mbali mbali wa kuweza kutuwesha kufikia lile lengo ambalo limekusudiwa.

Lakini kwa kusema tu tukae tufunge mikono na tungoje mpaka tuweze kuwa na hayo ambayo wameyataja Waheshimiwa Wajumbe kwamba labla tuwe na walimu wa kutosha na mambo mengine basi tutachelewa katika kuhakikisha kwamba tunaanzisha mambo yetu mbali mbali. Lakini kwanza tuanze halafu baadaye mengine yote yatakuja kama kawaida.

Mhe. Spika, jengine ambalo nilikuwa nataka kulizungumza katika mswada huu ni kuhusu Baraza la Chuo kwamba litakuwa na Wajumbe na Wajumbe wenyewe wakatajwa. Sasa hapa Mhe. Spika, mimi nilikuwa na ushauri kwamba siku hizi kwa kweli kunakuwa na mambo mengi ambayo yanahitaji mambo ya sheria. Basi katika muono wangu nahisi kwamba katika wale Wajumbe tungekuwa na nafasi kwamba alau tukaweka mjumbe mmoja ambaye ana shahada ya sheria. Kwa maana kwamba pale ambapo patakuwa na tatizo lolote la mambo ya sheria basi aweze kusaidia hii taasisi.
Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulizungumza ni kifungu cha 9 (2) kinachozungumzia wajumbe na kusema kwamba:

" Nusu wa wajumbe wanaweza kuifanya hiyo *quorum* kuwa sahihi".

Uzoefu unaonesha Mhe. Spika, ni kwamba katika kikao chochote kile ambacho kinahitaji maamuzi basi lazima kuwe na zaidi ya nusu ya wajumbe ndio ule mswada au jambo linahitaji kupitishwa pale linakuwa na nguvu ya kisheria au kupata kukubalika.

Sasa mimi ningeomba kwamba tukaingia hilo baada ya kusema kwamba tuwe na nusu. Kwa sababu tukisema tutakuwa na nusu ni maana ya kusema kwamba tutakuwa nne kwa nne bado hatujakuwa na ile zaidi ya nusu ambayo iwezesha mambo mengi ambayo ya maamuzi yanatakatiwa yawe zaidi ya nusu ya watu katika kutolea maamuzi mambo fulani.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nilizungumze katika mswada huu ni kuhusu kile kifungu cha 21 ambacho kinazungumzia utaratibu wa kukata rufaa iwapo kutakuwa na aidha mfanyakazi ama mwanafunzi ametenda kosa. Kwa hivyo, hakuridhika na adhabu iliyotolewa moja kwa moja basi kama ilivyo kunakuwa na taratibu za kukata rufaa. Sasa hapa kumetolewa taratibu mbili moja ni ya kawaida ile ambayo inazungumzia mtu yeyote amefanya kosa basi ana uwezo wa kukata rufaa ndani ya siku 14 ili kupinga maamuzi ambayo hakuridhika nao.

Lakini pia kulikuwa na kifungu ambacho kinasema kwamba aandike barua au aeleze nia yake hiyo kwa maandishi na kuipeleka kunakohusika ndani na siku tatu. Maana yake iwapo hakuandika hiyo barua ambayo ataandika kwa maandishi basi hata kama atapeleka rufaa inawezekana kwamba ile rufaa yake ikawa haina uzito. Lakini kwa nini kukawa na rufaa mimi nilikuwa nahisi hapa Mhe. Waziri atakapokuja angetusaidia kidogo kupata ufafanuzi wa hili. Je, iwapo mhusika hakuandika hiyo barua lakini ameandika rufaa moja kwa moja ndani ya siku 14 ambayo itakuwa ndani ya ile siku ambazo zinakubalika kwa makubaliano ambayo yamewekwa na sheria yake imetolewa itakuwaje, rufaa hiyo haitasikilizwa kwa sababu tu hakuandika yale maelezo yake kwa zile siku tatu ama rufaa yenyewe itatosha kukuudhi kuona kwamba matakwa yake yasikilizwe na kutolewa maamuzi.

Mhe. Spika, kwa kweli sikuwa na mchango mkubwa katika hili. Isipokuwa nia na madhumuni yangu ni kuchangia na mimi katika mswada huu. Kwa hayo, machache niseme tu kwamba mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Chaani nakubaliana na mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia mswada huu wa Sheria ya kuanzishwa kwa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia.

Mhe. Spika, kuanzishwa kwa chuo ni muhimu sana hapa Zanzibar. Mimi nina wasi wasi mkubwa wa kuanzishwa kwa chuo pale ambapo patakosekana yale mahitaji ambayo yanatakiwa katika chuo hicho.

Mhe. Spika, kwa mfano kukosekana kwa vitendea kazi vya chuo na kutokuwa na wataalamu bora ambao wana vipaji zaidi vya kusomesha pale chuoni. Hiki kama kitakosekana Mhe. Spika, ni tatizo ambalo chuo bado hatujakiweza.

Mhe. Spika, taasisi hii ihakikishe imepata wataalamu wa kutosha kwani kuwa na wataalamu ndio kutakaowafanya wanafunzi kuwa na uelewa zaidi mzuri na kutoa wanafunzi wazuri katika chuo hicho. Mhe. Spika, ikiwa wataalamu tunao wa kutosha na walio na vipaji vya juu zaidi naamini chuo kitakuwa na wanafunzi wazuri ambao watatoka katika chuo hicho.

Mhe. Spika, kwa kuwa watoto wengi masomo ya Sayansi yanawapiga chenga naomba chuo kiwe na uchunguzi au utafiti wa hali ya juu kabla ya kutolewa matokeo ya wanafunzi katika chuo hicho. Mhe. Spika, kwa sababu wakati mwengine watoto husoma na wakajitahidi lakini wanapofika katika chuo hutolewa matokeo huwa hayaridhishi.

Mhe. Spika, pia chuo kione umuhimu wa kuona wanafunzi ambao wamefanya vizuri katika masomo yao ya Sayansi kuwatumikia zawadi ili kuwapo uwezo wanafunzi walioko nyuma yao kufuatilia na kufanya masomo yao vizuri. Hii Mhe. Spika, ikiwa tutakuwa na watoto ambo watasoma pale na kipaji cha juu ambao watapata zawadi au motisha zaidi nadhani na watoto wa walioko nyuma yao watafatia na wao watafanya zaidi vizuri.

Mhe. Spika, mwisho kwa sababu sina mchango mkubwa sana chuo au taasisi iwe na udhibiti na imani ya kuona matokeo ya wanafunzi waliopasi wanapasishwa na wanafunzi waliofeli wanafelishwa. Kwa sababu ikiwa chuo kitakuchukuwa wanafunzi walio pasi tu lakini walikuwa walipasi kwa wakafelishwa hili litakuwa ni tatizo gumu. Kwa sababu ikiwa kapasi na ukamfelisha na ukamchukuwa mwanafunzi aliyefeli na kumpasisha itakuwa bado chuo hatujakiweza. Na hii Mhe. Spika, itakuwa chuo hakitendi haki kwa wanafunzi hao na pia kutoa wataalamu wazuri na serikali kuporomoka. Lakini ikiwa waliopasi wakaachiliwa itakuwa bado chuo hakijatenda haki na bado taifa litaanguka. Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru.

**Mhe. Ali Denge Makame:** Ahsnate Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada ya sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia na mambo mengine yanoyohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza niipongeze wizara hii kwa juhudi zake kubwa za kuletwa mswada huu ili kupata kuuchangia na kuupa baraka. Mhe. Spika, sasa inaonesha dhahiri tunapiga hatua nyengine mbele kwa kuwepo taasisi hii italeta maslahi mazuri kwa wananchi wetu hususan hawa wasomi ambao itawapa faraja kubwa kwa kuwa na chuo hiki katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa kuwa chuo hiki kiko katika maeneo mazuri ambayo yana uwanda mkubwa wa kuweza kuongezea majengo mengine au kufanya utanuzi. Kwa hivyo, mimi napongeza haya haya mabanda yaliokuwepo tuanzie hayo na tuendelee nayo pindipo hali ikiruhusu wakati uwanja upo basi tutaendelea kujenga mengine yaliokuwa ya kileo. Lakini kwa kuwa sasa tunayo basi tuanzie yale yale waswali wanasema kwamba "kila ndege huruka kwa ubawa wake". Kwa hivyo chuo hiki tukianzishe kama kilivyokuwa kimekusudiwa kianze rasmi.

Mhe. Spika, kwa kuwa tunakotoka vyuo hivi vilikuwepo baadhi yao muda mrefu tunakwenda navyo kidogo kidogo hatua kwa hatua tokea tulikuwa hatuna chuo hata kimoja sasa hivi tuna vyuo vingi tu vinaendelea kidogo kidogo.

Kwa hivyo, chuo hiki kitakuwa kinaleta faraja kwa wananchi wetu. Mhe. Spika, ukweli wa mambo ulivyo sisi tutaondoka hapa baada ya wananchi kutusikia wengi wao wamefurahi baada ya kusikia mswada huu umeletwa wa kuanzishwa chuo hiki. Kwa hivyo mimi ningeomba kiendelee na kipatiwe nyezo zote ili kifanikiwe haraka kuanzisha masomo haya kwa mujibu wa utaratibu ulivyo.

Mhe. Spika, kama inavyoeleweka serikali hii inajitahidi kutafuta maendeleo na kuboresha mambo mbali mbali kwa wananchi wake, ingawa wachache hawafurahi wanazuia misaada hii ili wananchi wasiendelee kufanikiwa na baraka hizi. Lakini mimi ninavyojua na kuamini kwa Mhe. Waziri wa Elimu kwa juhudi zake kubwa anazochukua za kutafuta misaada mbali mbali inshaalla tukianzisha chuo hiki huenda tukapata mafanikio mbali mbali ya vifaa, majengo ili kufanikisha ubora wa chuo chetu hiki.

Mhe. Spika, ingawa masomo haya yako zamani lakini yalikuwa hayajaundiwa taasisi maalumu. Kwa hivyo, ilikuwa mara nyingi yanakwenda lakini mafanikio yake yalikuwa si mazuri. Kwa hivyo, kwa sasa hivi kwa kuwa imeundwa taasisi maalumu hii ya kushughulikia masomo na matunda ya masomo haya tutayaona, kama tulivyokuwa tunajua mara nyingi sana sehemu zetu nyingi zinakuwa na kikwamo cha wataalamu wa Sayansi na wa fani mbali mbali huwa tunakwazwa. Kwa hivyo, kwa kuwa kitaanzishwa chuo hiki, baadhi ya sekta zetu nyingi tutakuwa na wataalamu wetu wenyewe bila ya

kutegemea wataalamu kutoka nchi za nje. Kwa hivyo kwa kuanzishwa chuo hiki Mhe.Spika, kitaleta matumaini makubwa kwa wazanzibari na hata wageni kutoka nchi za nje.

Mhe. Spika, ukurasa wa 220 kifungu cha (3d) kinasema:

“ Uanzishwaji wa taasisi”.

Kifungu (d) kinasema:

“Uwezo wa kununua na kuuza mali zake”.

Hii Mhe. Spika, ningeomba ikaundiwa taasisi maalumu ya kuangalia ununuzi na uuzaji wa vifaa vya taasisi hii, ili kuepuka baadhi ya wale wachache, ambako kuna vifaa muhimu tu vilivyokuwa havijaharibika au vilivyokuwa havijachakaa kuuzwa kwa njia ya udanganyifu au kubuniwa kununua vifaa vilivyokuwa si vya kileo au vilivyokuwa havina ubora ili kupata kuharibu masuala mazima ya utekelezaji wa kazi hii. Kwa hivyo, mimi ningeomba taasisi hii ikaunda idara maalumu ya kusimamia na kupitisha manunuzi na mauzaji ya vifaa vya taasisi hii.

Mhe. Spika, ukurasa wa 221 kifungu cha (5) kinasema:

“Kazi za Taasisi”.

Mhe. Spika, kazi za taasisi kama zilivyoidhinishwa hapa kuanzia kifungu (a). Hii mimi naunga mkono kwa mujibu wa taratibu jinsi ulivyojazwa katika *paper* hii. Kwa hivyo, ziendelee na zifanye kazi zake kwa mujibu wa taratibu zilivyo.

Mhe. Spika, ukurasa wa 221 kifungu cha (6) kinasema:

“Baraza la Taasisi”.

Baada ya kuundwa na wajumbe hao kuanzia (a mpaka c) na (i hadi viii) maelezo haya yote ambayo yameelezwa hapa mimi nayaunga mkono nayakubali ili yatekelezwe kwa mujibu wa utaratibu ulivyo na pindipo yatatekelezwa haya ufanisi tutaupata katika taasisi hii ya Sayansi na Teknolojia.

Mhe. Spika, kwa kuwa nia na madhumuni ya serikali hii kuanzisha taasisi hii kwa madhumuni ya kupata wataalamu tuwe nao wenyewe ili tusitegemee zaidi wataalamu kutoka nje. Kwa hivyo, taasisi hii itatupa mwanga wa kupunguza makero mengi ambayo tulikuwa tukiyapata baadhi ya sehemu nyingi kama vile

maskuli kukosa walimu wa sanyansi, hospitali kukosa wataalamu wa sayansi na taasisi nyengine kukosa wataalamu mbali mbali. Kwa hivyo, hili naliunga mkono Mhe. Spika, ili kupata kuboresha shughuli zetu mbali mbali za kimaendeleo.

Mhe. Spika , kubwa tu nitaloliomba katika Baraza hili litaloundwa la taasisi hii viongozi wake wawe waadilifu, wawe waaminifu wafanye kazi kizalendo ili kufanikisha azma hii ya maendeleo ya katika nchi yetu hii.

Ukurasa wa 227 kifungu (e) kinasema:

"Malipo ya ada kwa watahiniwa".

Mhe. Spika, hapa mimi ningeomba sana wahusika wa taasisi hii, wakaangalia sana katika watahiniwa wa kizalendo pindipo wanapotaka kulipa ada hii. Wapewe nafasi ya mkopo ili kupata kufanya mitihani yao na wao wafanikishwe katika masomo ya taasisi hii. Kwa hivyo, pindipo tukifanya hivyo ndio tutafanikisha yale malengo ya Mapinduzi. Kwa kila mwananchi au kwa kila mzalendo afaidike na elimu na matunda mbali mbali ya Mapinduzi kama inavyoeleweka. Baadhi ya wananchi wengi wa visiwa hivi ni watoto wa wafanyakazi na wakulima wengi wao hali zao duni. Kwa hivyo, pindipo kama tutapatiwa nafasi hii ya kupatiwa mikopo na wao waendelee na masomo tutafanikisha kupata wataalamu wetu wenyewe wa kizalendo kutoka nchini mwetu.

Mhe. Spika kwa kuwa mchango huu una baadhi ya wachangiaji wengi, kwa hivyo kwa upande wangu tunaupa baraka nauombea heri na mafanikio ili wajumbe sote tuupitishe tupate tufanikishe na sisi tuwe na chuo hiki, ili kuleta faida kwa wananchi wetu. Mhe. Spika, kwa hayo yote naunga mkono mswada huu pamoja na wananchi wenzangu wa jimbo la Amani mia kwa mia ahsante sana.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Spika, kwanza nakushukuru na kwa kweli sina mchango mkubwa sana kwa sababu nilishiriki katika kuujadili mswada huu katika kamati tulikuwa pamoja na Mhe. Waziri na watendaji wake na kwa kweli tulishirikiana vizuri na tukafanya marekebisho mengi ambayo yapo hapa. Kwa hivyo, na mimi ni mwanachama na nimechangia katika marekebisho haya. Lakini hata hivyo ipo haja niseme machache sana katika mswada huu.

Mhe. Spika, kwanza dhamira ya kuanzisha chuo nadhani kila mmoja wetu anakubali kwamba ni nzuri. Kwa hivyo, dhamira ni nzuri haina mashaka hata kidogo. Lakini sasa suala linalokuja ni maandalizi. Kwa sababu kuwa na dhamira nzuri lakini ikawa haina maanadalizi mazuri. Mara nyingi hili ndio

kelele zetu ndani ya Baraza na tunakuwa tunajipongeza sana Zanzibar kwamba ni mahodari sana kwa kuanzisha vyombo vipya. Lakini tatizo letu Mhe. Spika, mara nyingi huwa hatufanyi vizuri katika kusimamia vile vyombo tunavyovianzisha na kufikia lile lengo lililotarajiwa.

Sasa tunazungumza haya ili kama kutoa changamoto kwa Mhe. Waziri, wizara yake kwa ujumla, lakini zaidi naona ni serikali kwa ujumla. Kwa sababu serikali ndio inayowawezesha hawa wakaweza kufanya vizuri. Na mimi mara nyingi sana Mhe. Spika, huwa sipendi kuwabebesha wenzetu lawama kwa sababu huwa wanajua kwamba haya mambo mengine yako nje ya uwezo wao. Kwa hivyo, inatosha niseme tu kwamba Mhe. Waziri katika karatasi yake hii kaeleza wazi wazi kwamba hii taasisi itakwenda hatua kwa hatua. Mhe. Waziri kasema uzuri kwamba itakwenda hatua kidogo kidogo mpaka kufikia huko juu. Lakini hatutarajii mwendo wetu uwe wa konokono, hii taasisi ikianzishwa watu wanatarajia iwe mwendo wa wastani sio wa mbio sana lakini vile vile usiwe mwendo wa konokono.

Mhe. Spika, mimi ushauri wangu kwa Mhe. Waziri na kwa serikali kwa ujumla kwamba madhali tumedhamiria kuanzisha hii taasisi basi tujiandae na nyenzo za kuendeshea hii taasisi yenyewe.

Mhe. Spika, sisi katika kamati yetu nasema bahati mbaya tumeghafilika sana na bahati mbaya hatukujua kwamba Mhe. Waziri atakuja na huu mswada. Lakini kama ingekuwa tunajua kama Mhe. Waziri atakuja na huu mswada nadhani ilikuwa ni busara wakati wa ziara za kamati ilikuwa tuombe tukaone kwanza kile chuo chenyewe hali ilivyo hivi sasa. Lakini bahati mbaya sana nasema sisi katika kamati hatukujua kwamba waziri atakuja na huu mswada na kwa maana hiyo tukapendekeza kupelekwe maeneo mengine ya wizara yake hili hatukupelekwa.

Naomba mara ya pili namshauri Katibu wetu wa Kamati tutakapofanya ziara katika kamati tutaiomba wizara itupeleke ili tukajiridhishe kuona kwanza hali ya sasa ya chuo ilivyo na tukafanye mazungumzo pale na wenzetu tuone huko tunakokwenda.

Mhe. Spika, kwa nini nikasema hivi, sisi si watendaji Baraza kazi yake kushauri na kuielekeza serikali hiyo ndio kazi yetu. Nasema hivi kwa sababu kuanzia jana vyombo vya habari vimekuwa vikitangaza kuna chuo kimoja kilikuwa kinatoa shahada Bara cha Ustawi wa Jamii, lakini kimezuiliwa kwasababu shahada zake ziko chini ya kiwango. Kwa hivyo, naogopa na sisi kuja kwenda huko. Wenzetu Bara mara nyingi wanakuwa wanafanya vizuri katika vyuo lakini pamoja na wao vile vile limewakumba hilo. Wameanzisha

chuo wanatoa shahada lakini shahada zao zimeoneka dhaifu sasa mimi sipendelei twende huko katika hali kama hiyo.

Mhe. Spika, kwa taarifa za kijuu juu tu ambazo ninazo ni kwamba hali ya Chuo cha Karume kilivyo sasa ni tofauti na kilivyokuwa miaka ya 60, 70, 80 kila kikienda ile hali ya majengo yanachakaa hali ya mazingira vile vile yanazidi kuchakaa na chuo hiki ndio tunataka kukifanya taasisi ambayo lengo lake kama alivyozungumza Mhe. Waziri hatua kwa hatua, ni kwenda katika kutoa shahada.

Sasa Mhe. Spika, mimi nimevutika sana, haidhuru sijafanya utafiti wa kina, lakini na wenzetu walipoanzisha ile *DARTEC* walipoifanya kwamba ni Taasisi ya Sayansi na Teknolojia. Kwa sababu mimi sikusoma *DARTEC*, lakini hii miaka ya nyuma nilipata fursa ya kwenda, kwa kweli niliiona *DARTEC* ya wakati huo. Hivi karibuni nimebahatika kwenda nimeona *DARTEC* ya leo ilivyo ikiwa ni taasisi. Kwa hivyo, kuna mabadiliko makubwa na kwa kweli yanatia matumaini. Sasa na sisi Mhe. Spika, tunataka tunapoanzisha vyombo kama hivi twende huko.

Mhe. Spika, jengine linalonitia wasi wasi nasema wizara ina watu makini, serikali ina dhamira nzuri, mimi ninachozungumzia zaidi uwezeshaji. Sasa katika kukiwezesha hiki chuo kuna mambo mengi ya kuzungumza. Lakini uwezeshaji mmoja wa hiki chuo ni kukipatia wanafunzi walio bora watakaoingia. Lakini Mhe. Spika, tunaona hali sasa hivi katika maskuli yetu ya masomo ya sayansi na hisabati yalivyoanguka. Sasa hivi wanafunzi wetu wengi wanakimbilia kwenye masomo haya ya sanaa *(arts)*, lakini hisabati na sayansi watoto wengi hawapendi. Sasa kama hatukuweka msingi mzuri kuanzia katika elimu ya msingi, sekondari ya awali na sekondari ya juu katika haya masomo ya sayansi na hisabati hiki chuo kitakosa wateja. Si wateja wa unga, nakusudia wale wanafunzi ambao wazuri tunaowahitajia.

Mhe. Spika, nasema hilo kwa sababu hata ukiangalia hivi vyuo vyetu vya Zanzibar, wanafunzi wetu wanaoingia viwango vyao vya kufaulu viko chini ukilinganisha na Bara. Tanzania Bara sasa hivi wenye nafasi kubwa ya kuingia vyuo vikuu ni wale waliokuwa wana *division I* na *division II*, kama huna *division* hizo nafasi ya kuingia vyuo vikuu vya Bara ni ndogo. Lakini kwetu sisi tunawatafuta hao wenye *division III* waingie vyuo vikuu mara nyengine inakuwa shida. Sasa kwa misingi hiyo unaweza ukaona kwamba lazima mtu aliyekuwa na *division I* na *division III* uwezo wao bila shaka ni tofauti na wote wanapoingia vyuo vikuu wanakwenda kusoma kitu cha aina moja. Haidhuru kupasi mitihani pekee sio kigezo kwamba mwanafunzi hodari, lakini wakati mwengine ndio vigezo vinavyotumika. Wataalam wasingetumia kutaka lazima

mtu awe na *division I* au *division II* kwa sababu wanatafuta *cream*, lakini sisi *cream* tunazikosa.

Mhe. Spika, nina wasi wasi kwamba sasa hivi wanafunzi wetu wanaoingia vyuo vikuu vya Jamhuri ya Muungano kwa Zanzibar ni wachache mno. Haidhuru vile ni vyuo vya Muungano na sisi tuna haki na hiyo miaka ya nyuma vilipoanzishwa ilikuwa tuna *quarter* yetu hasa, lakini tukaiua sisi wenyewe hatukuisimamia ipasavyo.

Mhe. Spika, sasa hivi sijui ni kiasi gani, labda hili wakati wa bajeti Mhe. Waziri tutakuja kumuuliza. Lakini sijui kwa kipindi hiki Zanzibar tuna wanafunzi wangapi wanaosoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wangapi wanaosoma Mzumbe, wangapi wanaosoma Chuo cha Usimamizi wa Fedha, wangapi Sokoine na kadhalika. Kwa sababu hii Mhe. Spika, sasa hivi masharti makubwa uwe na *division I* au *division II*. Kwetu sisi hapa wanaozipata wanakuwa ni watu wachache sana, *division I* wanakuwa ni wachache zaidi ni ajabu hasa.

Tuliona wakati wa bajeti nafikiri Mhe. Hamad Masoud Hamad alitoa takwimu, sekondari moja tu Bara tuliona idadi ya wanafunzi waliopata *division I* na tukaona sisi Zanzibar nzima waliopata *division I* walikuwa ni wangapi. Yaani hamna kitu ukilinganisha na sekondari moja tu ya Bara na hawa ndio sasa tuna vyuo vikuu vingi na taasisi hii nayo inaelekea huko katika kutoa diploma pamoja na shahada. Mhe. Spika, mimi kinachonitia wasi wasi. Je, kwa hali yetu hii tunayokwenda ya masomo haya ya sayansi na hisabati kuanguka vibaya sana na tunaongeza vyuo hivi ambavyo vinatoa elimu ya juu. Wakati huo huo, Mhe. Waziri anajiandaaa vile vile Chuo Kikuu hiki cha SUZA kufungua Kitivo cha Uhandisi ambacho kinahitaji wataalam zaidi. Sasa hapo ndio hofu inapokuja. Je, lengo letu, dhamira yetu tunaifikia. Kwa hivyo Mhe. Spika, ushauri wangu katika hili kwanza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iimarishe mikakati yake ya kuimarisha masomo ya sayansi na hisabati kuanzia skuli za msingi mpaka juu.

Ushauri wangu wa pili katika huo mkakati wao basi lazima sasa hivi wizara na serikali kwa ujumla akiwemo Dk. Mwinyihaji Makame, kwa kweli lazima wajikubalishe kutoa motisha maalum kwa walimu wa sayansi kuanzia sekondari mpaka kuja juu, vyenginevyo tutakuwa hatupati watu. Kwa sababu hawa wachache tunaotegemea wanaomaliza watusomeshee watoto wetu katika vyuo vyetu wanachukuliwa Bara kwa kukosa motisha. Hapa mishahara midogo hakuna motisha, leo vijana wetu wakimaliza SUZA wanachukuliwa Bara

inakuwa sisi tunachukua maji kwenye pakacha na huku tunataka kuiendeleza taasisi, huku SUZA inataka kujitanua kuongeza Kitivo cha Uhandisi.

Sasa Mhe. Spika, ukiangalia sheria mimi sina matatizo nayo, nasema *wording* yake sina matatizo nayo wala sipingani na dhamira hii. Lakini sasa hofu yangu ipo hapo kwamba haya tuliyonayo sasa tunasuasua na huku tunaongeza mapya. Je, tutayaweza?

Sasa ushauri wa pili ukiacha ule wa wizara, najua wizara ina watu makini. lakini kwa upande wa serikali kwa ujumla kama kweli tunataka vyuo hivi viende kama tunavyotaka na tunataka elimu yote kwa ujumla iboreke, basi lazima bajeti ya elimu tuitazame upya. Mhe. Spika, hivi karibuni katika kamati yetu mimi na wenzangu tulikwenda SUZA wakatueleza matumizi yao hasa halisi ni yepi na wanachopata ni kipi, yaani hawafikii hata nusu. Mhe. Spika, kama kweli tupo makini hivi vyuo vyetu viwe katika viwango vizuri, huwezi bajeti ya SUZA wakakadiria bilioni 6 ukawapa bilioni 2, hapo umakini haupo. Mimi naamini bado kama tuna nia njema yapo maeneo mengi ya kukata kata tukaongeza *ceiling* yetu katika elimu. Mimi naamini serikali ikikusudia hasa, basi SUZA kama wakitaka bilioni 6 uwezo wa kupewa upo.

Lakini SUZA ikitaka bilioni 6 ukawapa bilioni 2 huo ni ucheza. Au kama hii taasisi tunayotaka tuitungie sheria leo hii itakuja kutaka vile vile. Maana yake waziri kasema anakwenda hatua kwa hatua. lakini haitakuwa *sledge path.* Ikija ikikaa miaka 20 hatujaona shahada hata mimi nitamgeuka Mhe. Haroun Ali Suleiman maana hatua zake itakuwa siridhiki nazo. Nategemea hatua zake kwa vyovyote isipindukie miaka 10 chuo hiki kitoe shahada. Hiyo miaka 10 mingi labda tuseme mitano tutoe shahada. Tunaona Dar es Salaam pale.

Mhe. Spika, mimi nafikiri serikali kwa hili lazima ikubali kubadilika na lazima ikubali ku-*invest* katika elimu. Kama serikali haijakubali ku-*invest* katika elimu kikweli kweli Mhe. Spika, haya nasema itakuwa ni ndoto. Huu mswada tunaoupitisha utakuwa ni ndoto na haya mambo yetu mengi tunayofanya kwa kweli itakuwa ni ndoto.

Mhe. Spika, nakumbuka kusoma ripoti mbili, moja sikumbuki mwaka gani, lakini moja nakumbuka mwaka 2007 ya Profesa Msolwa kuhusu hali ya vyuo vyetu hivi vikuu vya Zanzibar vyote vikiwemo hivi vya binafsi. Kwa kweli si nzuri, nakumbuka nilizungumza katika bajeti, lakini ile ripoti ya Profesa Msolwa haikuwa nzuri. Ripoti hii ya *Credential Council* kwa Kiswahili sijui

nini. Lakini ripoti hiyo haikuwa nzuri kuhusu vyuo vikuu vyetu. Sasa mimi sipendi tubakie hapo lazima tutoke hapo. Je, vipi tutatoka hapo? Serikali sasa ibadilike ikubali kweli kweli ku-*invest* katika elimu. Najua watu watajenga hoja, kwamba sasa hivi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanapata bajeti kubwa zaidi kuliko wizara nyengine. Lakini sasa tazama Wizara ya Elimu wanapata bajeti kubwa, lakini ndio wizara inayoongoza kwa watumishi wengi. Wizara hii sio kwamba inapata pesa nyingi kwa sababu ya upendeleo. Hakuna namna, kwa sababu wizara hii kwa Zanzibar ndio wizara inayoongoza kwa watumishi wengi. Ndio iliyokuwa imeenea katika kila kijiji ipo.

Lakini sasa angalia kama Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, Shidi haipo, Mkanyageni haipo, hakuna Mahakama kule wala hakuna taasisi yoyote ya wizara hii. Au Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Wanawake na Watoto, hakuna taasisi ya wanawake na watoto katika jimbo langu. Sasa ukiona bajeti yake kwamba inakuwa ndogo kuliko Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haijawa hoja hiyo. Nadhani watu wanaweza wakajenga hoja pengine hata katika serikali, wakasema sasa hivi Wizara ya Elimu ndio inayopata fedha nyingi, ndio lakini hizi zote zinakwenda kwenye mishahara ya kulipa walimu na kuhudumia maskuli. Nadhani hapa namsaidia waziri ikija ikijengwa hoja hii. Kwa hivyo, isihusishwe tena hapa kwamba tusivitanue vyuo vikuu vyetu. Mhe. Spika, hiyo ilikuwa sina budi niieleze.

Mhe. Spika, mimi kama nilivyosema kwamba nilipata bahati ya kushiriki katika kamati, lakini kwa sababu ni mjumbe wa kamati hii mimi nimeamua niwaambie Wizara ya Elimu na serikali haya niliyokuwa nayo. Kwa sababu Mhe. Spika, mimi katika jambo nisilolipenda kujidanganya, maana yake nikijidanganya mwenyewe nitakuwa namdanganya nani. Haya tunayofanya mengi itakuwa kama tunajidanganya. Hebu tutazameni kweli, hiki Chuo cha Ufundi Karume kilivyo leo, ndivyo kilivyokuwa Karume wakati wa Karume mkubwa. Jibu sio. Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana.

**Mhe. Assaa Othman Hamad:** Mhe. Spika, nakushukuru na mimi jioni hii kunipa nafasi ya kuweza kusema machache sana juu ya mswada wa sheria uliopo mbele yetu. Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake na mapenzi makubwa kwetu kutujaalia jioni hii tukakutana tena kuendeleza shughuli ya uwakilishi wa wananchi ndani ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, ni imani yangu ya dhati kwamba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na wivu wake wa kimaendeleo, anayahitaji mengi ili nasi

kwa heshima ya nchi tuwe nayo ndani ya sayari ya leo. Lakini mimi nasikitika kwamba mazingira tuliyonayo bado hayajamruhusu. Mhe. Spika, kila vinavyoelea huwa vinaundwa. Sisi tulivibomoa, nashukuru kwamba sasa tumetanabahi baada ya miaka 45 turudi tufanane na wenzetu.

Mhe. Spika, mimi nitaanza kumuuliza swali Mhe. Waziri ili atakaporudi hapo kwanza anipe na mimi taaluma. Hii Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia nafahamu kwamba ni Wizara ya Muungano. Je, taasisi hii tunayoizungumza leo na *inshaallah* sheria itapitishwa ndani ya Baraza lako tukufu, tukishaipitisha na Mhe. Rais akasaini, taasisi itakuwa na sifa hizo za elimu ya juu, sayansi na teknolojia? Kwa maana yenyewe nayo itapata heshima ama sifa za hiyo Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ya Jamhuri ya Muungano? Nalitanguliza swali hili kwa wasi wasi kama walionao wenzangu kwamba mbona mzigo utakuwa ni mkubwa kwa Serikali ya Mapinduzi kwa hali tuliyonayo, hali ambayo kila siku haijatupa matumaini ya uchumi wetu kwamba tunakwenda juu. Bado tunapigana, *inflation* hatujaimudu, bajeti za mawizara nyengine hatuzifikii nusu.

Mhe. Spika, mheshimiwa aliyekaa punde hivi kaitaja Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba labda Dk. Mwinyihaji Makame angetia nguvu zaidi hapo. Lakini na Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry nae ili tupate watu wenye afya njema waweze kusoma vizuri, kinamama wajengeke vizuri kiafya wazae watoto wazuri wenye afya, vijana wanaozaliwa halikadhalika wawe na afya bora, tunahitaji Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iongezewe fungu. Lakini ili tuyapate hayo Mhe. Khatib Suleiman Bakari kilimo tunataka tuzalishe vizuri zaidi, tusafirishe, tule tushibe, tuyamudu hayo tushinde njaa, tushinde maradhi.

Sasa kwa ujumla bado tatizo lipo. Madhumuni ya mswada huu ni kukigeuza Chuo cha Ufundi Karume kuwa ni Chuo cha Sayansi na Teknolojia. Naiona *it is an over simplified answer to a very complicated matter* kwangu mimi. Tutaweza vipi? Kama Kengeja imetushinda kuipa tupa na patasi hadi leo. Chuo cha Karume waliosoma pale na wakasomesha pale wamejieleza vizuri asubuhi. Chuo cha Mikunguni mimi sijasoma pale, lakini napafahamu juzi na jana, leo hapatamaniki sifa zimeshuka vibaya mno, ndio ukweli wenyewe tukubali.

Mhe. Spika, nayasema haya kwa masikitiko, *foundation* haipo. Humu ndio tulitegemea tuwapate kuja kuingia hapa, lakini wakishafika hapa wakute mazingira yanayooana na sifa za hapa na matarajio. Ndio maana nikauliza je, tutakuwemo kwenye Muungano ili na sisi tuwe tunapata kutoka huko? Kama jibu litakuwa ndio sina wasi wasi mkubwa. Labda baada ya ile miaka kumi, ingawaje Mhe. Haji Faki Shaali kasema mitano, huenda tukaanza kubadilika. Lakini mwelekeo ni upi? Mhe. Waziri kalenga walimu wa taasisi hii atatoa wapi? Kama tuta-*import* ni fedha ndio hilo hilo tatizo letu, tutahitaji fedha

nyingi. Kama ni hapa ndani angalau watahitaji *incentives* muda wao wa ziada. Mhe. Spika, *parameter* zote zinanitia mashaka.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri kwa ujasiri wake, umahiri na sifa nyengine nyingi Mwenyezi Mungu alizomjaalia, mwenzetu amepata yepi mpaka akaja na hii. Akitufikisha mahali tukamuunga mkono nia ni nzuri na sisi tunafarajika, lakini hatutofarajika kwa kuweka majina tu kwamba tunafanana na wenzetu. Mimi nataka Zanzibar tukifika mahali wanahitajika ma-*engineer* wa fani gani na ipi, yanakuja maombi na Wanyarwanda, Warundi, Waganda asilimia 90 iwe tunachukua wenyewe hapa nitashukuru sana na nitapenda sana. Hayo ndio nataka yawe mategemeo na madhumuni ya huu mswada.

Lakini kama tunapamba na sisi tuwe na sayansi na teknolojia hapana. Kama umesema tunataka twende hatua baada ya hatua kama mzee wetu Rais wa Awamu ya Pili, ni vizuri maana ukidandia huenda ukaja kujikwaa mambo yakawa mengine. Lakini hatua baada ya hatua tungetoka hapa ufundi tukenda teknolojia hiyo, tukasema ni *institute* tukaacha sayansi. Kwa sababu sayansi ndio ile niliyosema *complicated matter,* ndio maana yangu niliyoiona mimi, kwamba huku tunakotoka skuli zetu zote hazina vifaa vya sayansi wala walimu wa sayansi. Haidhuru wenzetu wanatusaidia, lakini wafundishaji wa vitabu hivyo hatuna na kama wapo ni wachache mno. Sura ya majengo yetu yanavunja heshima ya jina letu.

Mhe. Spika, Fidel Castro ya Maalim aliyekuwa akifundisha chemistry jina limenitoka, lakini anaifahamu Castro ya miaka ya 70, ukija kumpitisha leo kama hatolia atafumba macho asiione. Nkrumah mimi sikusoma lakini ilikuwa ndio dakhalia yangu nilisoma Lumumba, nasikia imeshabadilishwa hilo jina pia silo tena. Nasema jina si tatizo, cha msingi ni kupata ile *material* iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, kila anayesimama hapa hajakataa mswada tokea asubuhi sijasikia mtu kuupinga. Mimi pia siukatai, lakini hofu yangu je, mswada utakwenda na malengo yaliyokusudiwa? Hatutakuja kuchekwa? Ndio pale nilipouliza Mhe. Waziri amepata yepi mwenzetu mpaka akaja na hili? Kwa sababu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira nashukuru kuna watu wazuri, taaluma zao kubwa, wana uzoefu, ni mambo yanayohesabiwa hayo. Siku moja Mhe. Waziri nilikuuliza au huwasikilizi hawa mbona mambo yanakwenda hivi? Nikiitazama timu ni nzuri tu ya elimu, lakini mbona mambo si mazuri. Mhe. Spika, Mhe. Haji Faki Shaali kidogo kanisaidia kuona kumbe serikali haijawa tayari. Ndio ile uchumi upo, lakini mnaukalia hatujawa tayari kuutumia.

Tukisema serikali Waziri wa Fedha tutamkamua mpaka atoke maji. Kwa mapato yaliyopo anayokusanya bila ya kutia mkono kwenye mapato yetu halisi, mwenyewe atakuwa ananifahamu nikisema hivyo. Kwa haya haya yaliyotuzunguka hapa kama angalau tunayamiliki wenyewe tunaweza tukafanya kitu kikaonekana. Lakini bado kwa muhali uliopo hatutoweza kuyafanya haya tutachukua muda. Bahati nzuri ama mbaya, usishangae hata ndugu mbaya atakayekuonea wivu au ikawa hapendi maendeleo yako. Hayo ndio maradhi yaliyotusibu. Kwa hivyo, nasema hivyo, maeneo yetu ya kupata mapato yetu ya kuendesha shughuli zetu tuyamiliki wenyewe. Hapa tutoke, taasisi tunaianzisha na malengo yake iweze kufuatana na mkondo wa sasa. Kwa sababu kuna mambo tutakwenda hatua baada ya hatua, lakini kuna mambo tunahitaji tu-*jump* ili tufuatane na wenzetu.

Wakati hautusubiri jamani, Jumuiya kesho tukifika huko kwenye mkondo wa siasa tukishapata Rais wa Afrika Mashariki tutakuja kumlaumu nani? Anatoka hapa Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry, anatoka hapa Mhe. Haroun Ali Suleiman, anakwenda Arusha kakaa na wenziwe kule halafu kesho mtakuja kukataa hamkuwemo? Tumeshaitwa huko tunapiga kelele na nani? Watatwambia wale walikuwemo Wazanzibari. Ushapu ni ule ule Wazanzibari walikuwepo hapa, tunalalamika. Lakini wanaosema sasa kwamba Wazanzibari nao walikuwepo ndio wakati huu wa kuwakamata kile cha Wazanzibari tukipate tuweze na sisi kufanya shughuli hizi.

Mhe. Spika, suala la kuwapata vijana wa fani hii na nyenginezo nyingi kwa vyuo hivi, taasisi kama hii wakati ndio huu waswahili wanasema "kijua ndio hichi usipouanika hatima yake utaula mbichi".

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tulipokuwa na ile FTC vijana waliokuwa wakimaliza pale waliingia Chuo Kikuu moja kwa moja. Leo tumepata maelezo kwa wahusika kabisa, ni uzuri upi au ni sifa zipi nzuri walizorudi nazo hapa kwetu Zanzibar. Lakini hali kama ile ya miaka ile ni lazima tukae chini tujiulize, tulikosea wapi na leo tukashindwa hata angalau tu kutengeneza ile hali ya mwaka 1977 mpaka leo mwaka 2009. Tumerudi nyuma na kama tumerudi basi kuna kasoro, na kasoro hizo lazima kwanza tuzifute na tuweke mazingira mapya yatakayofuatana na taasisi hii mpya.

Mhe. Spika, sote tuna hamu kubwa ya kuona taasisi hii inafanya vizuri kwa faida ya wananchi wa nchi hii na maslahi yetu sote. Hatuna budi tutowe yale tunayofikiria kwamba ni vikwazo.

Mhe. Mwinyihaji waziri anayeshughulika na fedha na uchumi wa nchi. Narudi tena kukuambia kwamba fedha ipo Zanzibar, lakini peke yako tu hutoipata. Tukae sote tuidai, ili tupate kushughulikia mambo haya. Kwa sababu mambo

haya tusiyachanganye, yabaki tu kuwa ni mambo yetu kwa faida yetu, tukiharibikiwa, basi tunaharibikiwa sote na kama ni kudai basi tudaini sote.

Mhe. Spika, mimi najua sababu nzuri na kubwa ni kwamba dokta Mwinyihaji peke yako huwezi, lakini ukifuatana na Mhe. Moh'd Ali Salim ama Mhe. Haji Faki Shaali, basi utaweza. Kwa sababu wenzetu wanafanya hivyo, wanatoka nje wanafuatana na wenzao na wanakwenda huko ni timu ya Tanzania. Nasi tukitoka kama timu ya Zanzibar kwa faida ya Zanzibar na maslahi yao, hakuna cha aibu hapo ni haki yetu wala hujavunja miko, wala itikadi. Ni nani asiyejua kama Assaa mimi ni Mzanzibari, wananifahamu.

Juzi kuna mheshimiwa mmoja ni waziri wa kule Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Mhe. Spika, utaniwia radhi kidogo, nilikuwa nina matatizo pale katika hospitali ya Muhimbili kama siku ishirini na zaidi. Baada ya kujitambulisha kwao na kunifahamu, huwa sichelewi kuyalalamikia, huwa nayalalamikia sana. Basi wakaniambia hayo bwana ni matatizo yenu wenyewe, bila wasi wasi. Ndio nikamwambia dokta Mwinyihaji twende, kwa sababu nitamsuta yule, nitamwambia uliniambia kwamba ni yetu. Atasema nini.

Sasa dokta Mwinyihaji, ninakutanabahisha kwamba kwa sababu ya kibinaadamu kuna mambo mimi najua hutoweza kuyasimamia ipasavyo, kwa kiubinadamu tu. Lakini na mimi nikiwepo pale nitajifanya hivyo kuwa ni wa mkono wa pili, kwa hivyo mimi nitaweza na wewe utapata nguvu. Kwa hivyo, natoa siri kwamba hizi ni njia ambazo zitaweza kutusaidia katika shughuli kama hizi.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache sana nakushukuru kwa kunipa nafasi, ilikuwa na mimi nimsaidie Mhe. Waziri, ili akipata ile nafasi ya kufuatana na sisi, hususan na mimi nikamsaidie hii kazi, kwa sababu kuna mwahala tunakwama na yeye itakuwa vigumu kuweza kukwamua. Nakushukuru ahsante sana.

**Mhe. Suleiman Hemed Khamis:** Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi kidogo kuweza kuchangia katika mswada huu. Mimi kwa binafsi yangu nasema kwamba ni suala zuri, kwa sababu ni suala ambalo linategemea kwamba litatupa maendeleo kwa taifa letu. Hakuna mtu anayekataa maendeleo, hakuna mtu anayekataa jambo zuri, jambo zuri ni jambo zuri. Lakini hilo jambo zuri ni bora kwanza lizungumzwe mpaka lifikie hatima ya kuambiwa kuwa jambo hili ni zuri.

Mhe. Spika, mimi nataka tu niikumbushe Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba wizara hii imebeba mzigo mkubwa sana. Nafikiri si vibaya

tukaweza kuuchambua mzigo huu ili kila mtu aweze kuusikia mzigo huu na aweze kuona hali halisi.

Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina jukumu la kubeba wanafunzi wa visiwa vyote viwili ambapo wanafunzi hao ni wengi sana. Wanafunzi wote hao wanamahitaji mbali mbali ya maendeleo katika mashule yao waliyonayo. Huo ni mzigo mmoja.

Mhe. Spika, mzigo wa pili, ni kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imebeba walimu, ambapo tunasikia kilio cha walimu kila siku, kama kilio hiki kinatoka katika elimu ya msingi, ya sekondari au ya katika vyuo lakini haya malalamiko yapo kwa walimu. Kwa hivyo, huu tunauita ni mzigo mwingine.

Vile vile wizara hii hii imebeba wataalamu ambapo wataalamu wana matatizo yao mbali mbali. Wana kazi kwanza ya kuisaidia wizara katika kutoa utaalamu wao vipi wizara iende. Lakini wakati ule ule mtaalamu mzuri ni yule ambaye anapatiwa nafasi ya kuweza kujiendeleza. Kwa hivyo, huo ni mzigo mwingine. Wizara inahitaji kuhakikisha kwamba wataalamu wake wanapata nafasi ya kwenda nje kuongeza elimu yao, ili warudi katika nafasi zao kuisaidia wizara.

Halafu Mhe. Spika, tukiingia katika huo mzigo mwingine ambao wizara unao ni suala zima la majengo. Majengo katika mashule yetu mengi sasa hivi umekuwa ni mzigo wa wananchi, ingwa wizara inasaidia. Lakini pia nayo wizara ina mzigo katika kuhakikisha kwamba majengo ambayo wanajenga wananchi basi na wizara nayo inatia mkono wake, ili kusaidia kuyaendeleza.

Mhe. Spika, halafu wizara hii hii ina mzigo mwingine wa kuhakikisha haya majengo ambayo ni ya muda mrefu, basi ni lazima wizara ikae kitako na kuyakarabati majengo yale, ili yaweze kuwa mazuri na yawe salama kwa wanafunzi na walimu.

Mhe. Spika, mbali na hayo wizara kwa jumla itakuwa na mzigo mkubwa wa kuhakikisha wanafunzi wake kwa mujibu wa idadi yake waliopo katika mashule ya Pemba pamoja na mashule ya Unguja wanapata vifaa vya sayansi kwa mujibu wa hali ilivyo. Lakini wote huo utauona ni mzigo mkubwa sana kwa wizara. Ndio maana inashindwa saa nyengine wizara kuweza kutimiza vifaa hivi vya sayansi. Kwa hivyo kila siku kuna mapungufu makubwa sana, huo ni mzigo.

Mhe. Spika, kuna vifaa vya KK vya kujifunzia na kujifundishia, hivi havipo katika mskuli, huo ni mzigo mwingine. Mhe. Spika, mbali na hayo wizara imebeba mzigo wa kuhakikisha kwamba katika sehemu zake ina madaghalia. Katika madaghalia hayo kuna matatizo chungu nzima. Kuna matatizo ya

chakula, kuna matatizo ya malazi na makaazi, wote huo ni mzigo. Ufanisi upo, lakini sio mkubwa sana.

Mhe. Spika, kwa ufupi tunaiona ile hali ambayo wizara imebeba mzigo ambao si mdogo, tunawaonea huruma na tunawapa pole kwa kazi kubwa ambayo waliyonayo, kwa kuweza kuwatekelezea mahitaji yao walimu pamoja na jamii kwa jumla.

Mhe. Spika, tuone mifano mingine ambapo wizara hii hii imebeba. Imebeba vyuo, Pemba kuna vyuo na Unguja vipo vyuo. Lakini utakuta katika vyuo hivi bado kuna mapungufu makubwa katika vyuo hivi. Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuliambia Baraza hili kwamba pamoja na kuwa tunajitahidi kuweka vyuo, lakini mapungufu yake ni ya hatari. Kwa sababu mwanafunzi anachotakiwa kujifunza, anatakiwa ajifunze ile *theory* apate na *practical*. Sasa mwanafunzi mzuri ni yupi, ni yule anayesoma *theory* tu au ni yule anayesoma *theory* pamoja na *practical.*

Sasa utakuta wanafunzi wengi waliopo katika vyuo vyetu wanapata nafasi ndogo ya matumizi ya vifaa vya *practical*. Huu ni mzigo mwingine kwa wizara, ambapo wizara ihakikishe kwamba inaweza kuwatimizia. Kila tukiendelea basi tukumbuke miaka ya nyuma maskuli yetu tuliyokuwa nayo na tukilinganisha na idadi ya maskuli tuliyonayo hivi sasa, siku baada ya siku, basi maskuli yetu yanakuwa mengi zaidi. Bila shaka nyenzo zinaongezeka na hiyo yote ni fedha.

Mhe. Spika, jambo ambalo naliona linajitokeza hivi sasa, ni kwamba tunataka kujenga hoja katika chuo hiki. Lakini tuangalie asili ya chuo hiki au kukijenga chuo hiki asili yake itakuwa ni nini, asili yake ni mafunzo ya sayansi. Kuna wanafunzi wanaopenda kusoma masomo ya *art*, yaani masomo ya Kiingereza, Kiswahili, Dini na Kiarabu. Kuna wanafunzi ambao *by nature* wanapenda masomo ya sayansi, wanapenda kusoma Chemistry, wanapenda kusoma Physics na wanapenda kusoma Biology wapo wanafunzi hao. Lakini tukiwalinganisha katika maskuli yote baina ya wanafunzi wa *art* na wanafunzi wa sayansi, basi utaona wanafunzi wa *art* ni wengi zaidi kuliko wanafunzi wa sayansi.

Mhe. Spika, tukiangalia katika suala zima la ajira, basi utakuta hawa wanafunzi wa *art* mara nyingi wanapuuzwa. Mahitaji ya nchi hivi sasa yanahitaji ufundi watu ambao wamejiendeleza katika sayansi, hao ni kidogo. Sasa turudi nyuma tuangalie, kweli tuna shida ya kutaka kufungua chuo hiki, lakini chuo hiki kina taalaki na mambo ya sayansi.

Mhe. Spika, tuangalie kumbukumbu ya watoto wetu huko nyuma, ambao walikuwa wakipasi mitihani ya sekondari hapo wanapomaliza kidato cha nne na kuingia kidato cha sita. Pia tuangalie wanapofika kidato cha sita wanahitaji kuwa na *entry point* za kuweza kuingia katika Chuo Kikuu, basi wengi wao watakuwa ni wanafunzi wa *art* kuliko wanafunzi wa sayansi. Kwa hivyo, hilo ni jukumu letu sote, siwezi kusema kwamba ni jukumu la waziri peke yake. Tujuwe tutafanya vipi ili tuhakikishe kwamba na haya masomo ya sayansi yanapendwa na wanafunzi wanayapasi.

Mhe. Spika, mimi nasema hili suala ni muhimu, na kila kitu kinahitaji msingi. Msingi wa mwanafunzi anapoanzia katika *primary school* au anapokuwa katika *kindergarten*. Sisi hapa Zanzibar tunapofundishana, tunapenda sana kutumia mambo ya ubao, mwalimu anaridhika kwa kutumia ubao. Walimu wanaweza kuwa wa namna mbili, na ualimu ni kipaji. Anaweza kuwa mwanafunzi katoka skuli kidato cha sita, basi akashindwa na mwanafunzi anayetoka kidato cha nne.

Mwanafunzi unayemtoa *fresh* kidato cha sita na ukampeleka katika ualimu, basi atakuwa na matatizo mengi kwa sababu hajui mbinu za kufundishia, anaweza akashindwa na mwalimu aliyemaliza kidato cha nne akawa ni bora zaidi. Lakini katika ufundishaji wa namna hii wa kidato cha nne na kidato cha tano, basi utakuta mahitaji ni makubwa sana, matokeo yake wanafunzi wanashindwa kupasi mitihani kabisa.

Kwa hivyo, mimi nasema kama ikiwa wizara hii tunaweza tukasaidiana kwa pamoja, ili kuhakikisha kwamba masomo haya ya sayansi tunayapa kipaumbele, basi huenda tukapata wanafunzi wazuri baadae. Vyuo vyetu hivi wanavyoingia wanafunzi wanashindwa kumaliza vizuri, wanafika katikati wanafeli mitihani na kushindwa kuendelea. Au mimi niseme kwamba hiki chuo tunataka tukifunguwe kwa ajili ya kutafuta wanafunzi wengine watakaokuja baadae, au dhamira yetu kwa chuo hiki ni kwa ajili ya wanafunzi wetu waliopo Unguja. Kwa sababu watu wengine watakaposikia kwamba sisi tunafungua chuo hiki cha Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia Zanzibar, tuamini kwamba watu wataingia kwa wingi na watakuja kuomba nafasi za kuja kusoma.

Je, tuko tayari tutafute watu wengine kuja kusoma katika chuo hiki, au tuko tayari kuhakikisha kwamba sehemu kubwa ya wanafunzi wetu wanatoka hapa Unguja na Pemba. Sasa hili ni suala muhimu na linahitaji kuangaliwa kwa kina. Mimi nasema hili suala la chuo si kibaya kuwanacho, lakini ni lazima tujitayarishe vya kutosha au waziri aweze kusema kwamba maana yake mimi natoa hii kwanza, lakini labda itachukua baada ya miaka mitatu au miaka

minne tutatayarisha hiki chuo, au anataka mara moja kukianzisha kuna ugumu wake ambao kinaweza kuleta matatizo.

Mhe. Spika, tunataka kuweka vyuo, vyuo hivi si kusema tu kwa mdomo, vyuo vina mahitaji mengi. Tunahitaji walimu, tunahitaji vifaa, tunahitaji magari, tunahitaji wafanyakazi. Sasa kama hivi havijatimia sawa sawa na mimi wasi wasi wangu unavyonipa ni kwamba hivi vyuo sasa Unguja vimeshakuwa vingi, na wale ambao tulikuwa tunawategemea kutusaidia katika hivi vyuo, wameshaanza kujigawa katika vyuo mbali mbali. Je, hawa katika chuo hiki watakwenda kusaidiwa na nani? Je, wapo wengi wa kutosha kuweza kuwasaidia, au ni yale yale kwamba na mwalimu amemaliza kidato cha nne akasomeshe kidato cha nne, na hiyo sio haja. Tunataka wanafunzi wa kidato cha nne wasisomeshwe na walimu wa kidato cha nne, lakini wasomeshwe na mwalimu ambaye aliyekuwa na elimu ya juu zaidi.

Mhe. Spika, vyuo vinahitaji komyuta na vinahitaji magari, fedha nyingi vyuo vinahitaji. Mimi kama ingekuwa inakubalika, badala ya kuwa vyuo vinafanywa vingi sana katika nchi, basi tungeweza kuweka jengo moja kubwa sana ambapo f*aculty* zote za *education* tukaziweka mahala pamoja au *faculties* mbali mbali, ikiwa katika chuo kile tunakihudumia sote kwa pamoja, nyenzo zote tunazipeleka pale, walimu wote tunawapeleka pale, lakini kila mmoja anachukua *faculty* yake ya *education*. Hii ingepunguza kuliko tunavyofanya hivi sasa mtawanyiko, au huu ni wigo, tunafanya wigo. Ukija kitu tayari uwenacho, uwe na nyenzo za kukimalizia kile kitu.

Sasa tunajaribu kuona ule mtandao kuwa mkubwa sana kila pahala tunaeneza vyuo na kila chuo kina mapungufu hakikutimia. Unaonaje ingekuwa elimu hizi tukazikusanya katika jengo moja, ambapo mahitaji ya jengo hilo yote yanatimizwa magari yapo, makompyuta yapo, wataalamu wapo na wanafunzi wote wanaokuja pale, lakini kila mmoja anachukua *faculty* yake mbali mbali. Ingekuwa ni bora zaidi kuliko huu mtawanyiko tuliokuwa nao hivi sasa wa kuwa tuna vyuo vingi, lakini katika kila chuo kuna mapungufu ya kutosha. Kwa hivyo, si vibaya, ushauri wake ni mzuri. Lakini unahitaji uangalifu na wataalamu alionao awatumilie vizuri na wapate ushauri mzuri katika kuliongoza hili suala.

Mhe. Spika, jengine kubwa ni juu ya suala zima la mgao wa fedha. Mgao wa fedha ndio matatizo makubwa sana. Fedha zina matatizo, kwa sababu fedha yetu tuliyonayo ni ndogo, mapato yetu katika nchi hii ni ndogo na tuna mambo mengi sana ya kufanya. Ndio maana utaona fedha zinazotolewa za maendeleo hazionekani, zinatolewa za matumizi mengineyo zikimaliza basi ndio fatiha, hizo ndio zinazopatikana na nyengine kidogo za kusaidia saidia. Lakini za

maendeleo hakuna. Hii ni kuonesha maana yake *income* yetu tuliyopata ni ndigo na hatuwezi kufanya mambo yaliyokuwa makubwa sana na mazito.

Kwa hivyo, mimi nasema hii Wizara ya Fedha na Uchumi tutaiumiza, maana yake kila mtu anadai. Sasa huyu waziri hana mitambo ya kuzalisha fedha, fedha mpaka ichumwe ndani ya nchi ndio aweze kusaidia kila mahala. Fedha ile ni ile *income* ambayo *revenue* tunayoipata tunagawana kidogo kidogo, tunatakiwa tuwe waangalifu. Halafu tutakuja kumlaumu Waziri wa Fedha kwamba mgao wake wa fedha anaoutoa ni mdogo. Hatuwezi kumlaumu sana kwa sababu ile hali anakwenda kwa mujibu wa hali, atafanya nini? *Demand* ni kubwa zaidi na mgao unaokuja wa fedha ni mdogo. Sasa inabidi tuhangaike hangaike, tuwasubiri wenzetu watupe misaada kutoka nje, wamekubali sawa, hawakukubali ni matatizo.

Mhe. Spika, Ni mawazo mazuri kuwa nayo hii *instute* yetu si vibaya, lakini tuangalie *future* yetu itakuwa vipi. Tunaanza vipi na tutaendelea vipi au kama kuna watu ambao wa kuweza kukisaidia hiki chuo, wakatusaidia katika utaratibu mzima, kwanza wa kufanya *expansion* ya jengo, pakajulikana malazi yako wapi, kama ni chuo cha kulala au cha kwenda na kurudi ijulikane vile vile, wanawake watakuwepo wapi na wanaume watakuwepo wapi, madarasa yatakuwepo vipi na madarasa mangapi tutahitajia. Je, madarasa hayo itabidi kila mwaka tujenge au tujenge chuo kikubwa ambacho kitaweza kudumu kwa muda wa miaka mitano au kumi. Sasa hili ni suala la kupanga.

Mhe. Spika, mimi nashukuru kwamba katika Wizara yake ya Elimu na Mafunzo ya Amali anao watu wazuri, na washauri wazuri anao ambao wanaweza wakamshauri vizuri, kwa hivyo, yeye waziri mwenyewe ni lazima afanyekazi pamoja nao. Mimi ninaona kwamba kama Waziri wa Elimu ni lazima uwe karibu sana na watu wako, ili kuweza kupata ushauri wao, kwa sababu ipo saa nyengine ku-*outrule*, uki-*outrule* wale wadogo watasema *ok minister* kasema hivi.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, jitahidi utumie Kiswahili zaidi, naona mchanganyiko umekuwa mkubwa kweli.

**Mhe. Suleiman Hemed Khamis:** Ahsante sana. Ndio hivyo, maana yake nasema lazima waziri awe nao watu wake, maafisa wake anao ili aweze kusaidiana nao pamoja katika kuliendeleza hili suala.

Mhe. Spika, litakapoweza kufanyika vizuri hili suala, basi ni sifa ya wizara na ni sifa ya taifa na sisi tunahitaji kitu kama hiki tuwe nacho, lakini tunahitaji kujipanga vizuri, tukaangalia matatizo ndio tukayaweka mbele. Je, ni namna gani tutaweza kuyasawazisha matatizo yetu na namna gani hiki chombo

kitaweza kufanya kazi. Mimi nafikiri kupanga tu kwa mdomo si kazi kubwa sana, tunaweza tukapanga mara moja tu na mambo yakawa mazuri. Lakini utekelezaji ukaja ukawa mgumu, siku zote kupanga si tatizo, lakini kutekeleza ndio tatizo na kutekeleza kunahitaji fedha. Sasa sijui kwa mujibu wa mgao ama mwenyewe keshazungumza vipi na waziri. Kwanza hatujajua hili suala litaanzwa lina na litaanza muda gani, kama ni kesho ama keshokutwa au baada ya miaka mitano au miaka sita ijayo. Lakini mimi nafikiri ni wazo zuri, si wazo baya, tunalifurahia, lakini linahitaji uangalifu mkubwa sana.

Mhe. Spika, nafikiri kwa hayo machache yanatosha kwa hivi sasa.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kutoa mawaidha mawili au matatu. Mhe. Spika, michango yetu leo zaidi huwa inatoa nasaha kwa Mhe. Waziri, kuliko hata kuingia ndani ya huu mswada wenyewe.

Mhe. Spika, humu hamna makosa mengi, lakini tunavutana sana kwa hili wazo zima la kuanzisha hiki chuo. Mhe. Spika, mimi nataka niungane na wengi waliosema kuwa hili wazo ni zuri. Ni zuri kwa sababu vitu kama hivi vina faida mbili kubwa, kwanza ni nyenzo ya maendeleo katika nchi. Lakini pili, ndivyo vinavyoipa sifa hii nchi kuwa nchi.

Mhe. Spika, hivi karibuni tulikuwa na manung'uniko mengi kwamba wenzetu wanasema nchi yetu kuwa si nchi. Sasa tukiwa na taasisi hizi nyingi ni miongoni mwa vigezo kwamba hii ni nchi na pia ni nyenzo ya maendeleo, kwa sababu ukiwa na taasisi kubwa kama hii na ikiwa kwa kweli itafanyakazi kama ilivyokusudiwa uzalishaji wake utakuwa ni maendeleo makubwa. Tutakuwa na ma-*engineer* ambao ndio mambo muhimu katika nchi.

Mhe. Spika, bado wazo linakuja pale pale kwamba tutaweza kuliendeleza hili. Maana Mhe. Spika, mimi si mtu wa zamani sana, hapo ninapopakumbuka mimi kuna taasisi nyingi hazikuwa taasisi, zilikuwa ni vyuo na mashule mengine yaliyokuwa chini ya Wizara ya Elimu na yalipokuwa yakianzishwa kwa kweli yalikuwa yakienda vizuri, lakini hayakuwa na maisha marefu sana yamekufa.

Mhe. Spika, nitatoa mfano tulikuwa na chuo kimoja pale tukikiita Mikunguni *Trade School*, kilikuwa kizuri na ufundishaji wake ulikuwa mzuri. Wanafunzi waliokuwa wakitoka pale ndio wale hasa ambao walikuwa wanafaa na walikuwa wana-*qualification* nzuri za kuingia kwenye kile Chuo cha Karume pale. Tulikuwa tupo pale tulikuwa tunawaona mara nyingi Chuo cha Karume kinapokea wanafunzi waliomaliza pale *Trade School*, kwa sababu yale masomo yao yalikuwa yanafanana. Hiki chuo Mhe. Spika, sasa hivi hata kutajwa hakitajwi kimekufa.

Mhe. Spika, tulikuwa na Taasisi ya Kiswahili hapo na leo haipo tena, tulikuwa na Chuo cha Uchumi na kilianzishwa kwa matumaini makubwa sana, leo Chuo cha Uchumi hakipo tena. Sasa hivi yote ni majengo ya SUZA yale. Hata muelekeo wa Chuo cha Kiislamu sasa hivi umebadilika. Chuo cha Kiislamu kilikuwa kinatoa Masheikh tu kama mimi hivi. Sasa hivi Chuo cha Kiislamu kimechukua nafasi kama ile ya Nkruma, Nkuruma nayo pia sasa hivi ni SUZA. Kwa hivyo, utakuta kuna mambo ya kubadilika badilika, leo tunaanzisha kesho tunaua tunafanya jengine.

Mhe. Spika, hiki Chuo cha Ufundi cha Karume waliokuwepo pale wakisoma wamekieleza vizuri sana. Mimi nilikuwa pale dakhalia tu, lakini nilikuwa naona vile chuo kinavyokwenda. Kilikuwa kikienda kistaarabu kweli kweli. Leo hadhi ya chuo kile kwa kweli ina garagara chini. Ndio sasa hivi labda ningejiuliza, Mhe. Waziri kutaka kuinua tena ile hadhi yake lakini imekufa. Elimu inayotolewa pale hailingani hata siku moja na ile iliyokuwa ikitolewa siku za nyuma.

Chuo kilichoitwa cha Ufundi cha Kengeja kile hata hakikufikia ile hadhi ya kuwa Chuo cha Ufundi. Mhe. Assaa kasema hapa, hakiwezi kumudu hata tupa na patasi hakina. Ttulipokuwa tukifanya kazi za kamati tulitembelea pale, kwa kweli ni manung'uniko matupu hakistahiki hata kuitwa chuo cha ufundi, labda ni skuli ya kawaida.

Mhe. Spika, leo tunaanzisha jambo jengine lakini haya tuliyoanzisha yashakufa. Kwa hiyo, wengine wanapata mashaka kwamba jee na hili nalo litakwenda au litakufa kama yaliyokufa. Mhe. Spika, chuo hiki ambacho Mhe. Waziri anania ya kukianzisha kwanza ninadhani Mhe. Waziri angefanya utafiti wa kina kwa kutafuta fedha za kuweza kuyatanua yale majengo na kupata mwelekeo walimu watakuwa nani na nani ndio tukaanzisha.

Lakini hali ya uchumi wetu wa Zanzibar ninasema bado hairuhusu kuanzisha kile chuo. Suala hili nalizungumza kwa masikitiko makubwa sana, kwa sababu Mhe. Assaa Othman Hamad amewahi kusema hapa kwamba tulihitaji kupata fedha za kuanzishia na alisema fedha zipo, lakini namna ya kuzipata ndio kazi, aliwahi kutania kusema labda tufanye kazi kwa pamoja ndio tunaweza kujikwamua katika hii hali.

Mhe. Spika, masikitio yangu ni kwamba wenzetu tulioshirikiana nao wametufunga sisi miguu na halafu wao wakaenda mbele. Hali ya uchumi wao ni tofauti kubwa na uchumi wetu sisi, ndio maana leo tunapata tabu maana tunataka tuwafuate wao na wala sio wakuwafuata. Tulikuwa tukiomba ile

asilimia 4.5 kwa upande wa Zanzibar, tumechukua muda mrefu mpaka tuligombana na mtafaruku mkubwa ndio juzi imeletwa.
Sasa katika hali kama hii tusiwaige hatuwawezi. Katika waraka wake Mhe. Waziri alipokuwa akiwasilisha ametoa mifano mingi kuhusu vyuo kama hivi ambavyo siku za nyuma vilikuwa na hadhi kama Karume *Technical College*, lakini wao wenzetu wameanzisha taasisi hivi sasa na sisi tunataka twende huko. Lakini hatuwezi tena kwa sababu wakati tulipoanzisha Chuo cha Karume uchumi wetu ulikuwa mzuri, ni tofauti na hali tuliyonayo hivi sasa.

Wazo langu kwanza tungesita kidogo mpaka tukapata nyenzo ndio tukaanzisha. Kwa sababu mambo haya yanahitaji nyenzo, ambapo nyenzo kuu ni fedha na sisi hatuna fedha za kuanzishia.

Mhe. Spika, ninadhani tungeahirisha mipango hii mizuri mpaka pale Wazanzibari tutakapofanikiwa kuchimba mafuta yetu. Tukichapata mafuta tutakuwa na uwezo wa kuanzisha taasisi kubwa zaidi kuliko hizi, kwa sababu tutakuwa na fedha. Kwa hivyo, ni vyema tukaacha masuala haya tukapigana na mafuta mpaka ya kawa yetu.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi jana alitoa mwelekeo wa suala hili. Sasa tungefika mwezi wa Aprili na kuamua, baada ya maamuzi serikali ikalishughulikia suala hili kwa umakini zaidi, basi hapo tungekuwa na wakati mzuri wa kuanzisha mambo kama hayo.

Lakini hivi sasa tutakuwa na tunawapa tamaa kubwa, vijana wetu wakisikia kuna chuo kama hiki watataka kujiunga na pengine itakuwa ni usumbufu mtupu na mafanikio ni madogo sana.

Mhe. Spika, wenzangu wameshalizungumzia sana suala hilo na wala sitaki nilizungumzie tena. Isipokuwa niliutizama huu mswada na nikaona kuna mambo kidogo yanataka kuzungumziwa. Kifungu cha 6 kinazungumzia kuhusu kuanzishwa Baraza la Taasisi.

Kifungu cha 6 (1) kinachosema hivi:

> "Kutakuwa na Baraza la Taasisi ambalo litakuwa na wajumbe wafuatao:-
>
> (a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais."

Mhe. Spika, hii ni taasisi kubwa ambayo ni nyeti sana tena ni ya kitaaluma. Basi imezungumzwa tu kutakuwa na mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais na wala hakuielezwa sifa ya aina yoyote.

Ninadhani Mhe. Waziri angeliainisha, Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais, mwenye sifa hata *master* kwa taasisi kama hiyo ninaona ni mtu mdogo, maana yake ni taasisi kubwa sana. Basi angalau hiyo *master* ya masuala ya *technician*, lakini inaachwa tu akichaguliwa Abdalla Juma hatamudu kuongoza na kwa sababu iko hivi bila ya sifa na Mhe. Rais anaweza kumteua Abdalla Juma.

Kwa hivyo, ni bora angewekewa sifa kidogo licha ya wengine wanasema ni kumbana Rais, lakini si mbano mbaya isipokuwa ni kuuelekeza kwa ajili ya kufanya lile ambalo litatusaidia zaidi.

Vile vile katika kifungu cha 6 (c) naomba kunukuu.

> Kifungu cha 6 (c)
>
> > "Wajumbe wengine watano watakaoteuliwa na Waziri baada ya kufanya mashauriano na vyuo husika.

Wajumbe waliotajwa katika kifungu hiki ni watano, lakini kuna nambari za Kirumi (i) mpaka (viii) kwa hivyo badala ya kuwa watano watakuwa wanane. Ninafikiri hapa panahitaji marekebisho ya lugha maana kama ni watano ingeliishia namba tano ya Kirumi, lakini imeongezeka, kwa hiyo ni vyema pakarekebishwa.

Mhe. Spika, kifungu cha 7 (f) kinazungumzia uwezo wa Baraza pamoja na kazi zake. Sasa kazi hii kifungu (f) ni kupitisha mitaala, vyeti, stashahada, shahada na tunzo nyengine mpaka mwisho. Kwa upande wangu sina tatizo na masuala ya vyeti, stashahada, shahada, tunzo pamoja na mambo mengine, lakini kuhusu suala la kupitisha mitaala ninadhani ingeliachiwa Bodi ya Taaluma, kwa sababu ni mambo ya kitaaluma haya.

Kwa hivyo, ingelifaa zaidi hii Bodi ya Taaluma ikaachiwa hizi kazi za kushughulikia mitaala ya chuo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba mswada hauna makosa sana, isipokuwa wazo ni gumu kuonekana kuwa litatekelezeka. Baada ya hayo machache ninakushukuru sana.

**Mhe. Haji Mkema Haji:** Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa maoni yangu juu ya Mswada huu wa Kuanzisha Taasisi ya Karume. Katika kuuchangia nitaanza kama ifuatavyo.

Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na wenziwe wote kwa kukomaa katika uadilifu, kwa kuwa na nia njema ya kuendeleza taifa letu katika suala zima la taaluma.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali anastahiki sifa za pekee kwanza kwa matokeo mazuri ya mwaka huu, pili mwamko wa wananchi juu ya kujitokeza kwa wingi na kufanya vizuri na kuwa na sifa za kuingia kwenye mkondo wa elimu za juu. Katika historia ya miaka 45 ya Mapinduzi ya Zanzibar hii ni moja miongoni mwa vielelezo vya mafanikio makubwa. Mwaka huu wananchi au wanafunzi wetu wengi wameingia vyuo vikuu vya hapa Zanzibar vimejaa, Bara wamekwenda wengi na wengine wamekwenda katika nchi zetu za Afrika ya Mashariki, yaani Uganda na Kenya.

Sambamba na hilo wasingekwenda huko bila ya kuwa na sifa, ambazo zimetengenezwa na wenzetu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambao ni walimu wakisimamiwa na Mhe. Waziri wa Elimu. Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo ninampongeza sana Mhe. Waziri *(Makofi)*.

Mhe. Spika, leo Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ametuletea mswada huu wa Kuanzisha Taasisi ya Karume, ambayo itatoa taaluma ya ufundi, sayansi pamoja na mambo yote ya teknologia.

Madhumuni ya mswada huu yanakidhi haja hiyo. Kwa sababu hivi sasa tunao wataalamu wa masuala ya biashara, utawala na wengine hawana kazi za kufanya. Lakini watu hawa waliohitimu kwenye vyuo vikuu na kuwa na *degree* za kwanza na za pili, kama wangelikuwa na taaluma za ufundi ajira zipo wazi.

Hivi sasa serikali yetu inapambana na tatizo kubwa la ajira. Kwa hivyo, tutakapokuwa na wataalamu wa masuala ya taaluma ya ufundi, ninahakika tutapiga hatua katika kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la ajira nchini.

Suala la kwanza wataalamu hao watatusaidia katika kujikwamua na uchumi, kwa sababu watakuwa wabunifu wa kuunda mitambo. Mara nyingi tunawasikia waheshimiwa wenzetu hapa kusema kwamba tunataka viwanda vya embe, achari, samaki. Vitu hivi kwa kutegemea watu wawili bila ya sisi wenyewe kujitahidi itachukua muda mrefu sana.

Wenzetu wa China katika miaka 45 kama hii walikuwa wameshafika hatua kubwa sana na hata kuweza kuchimba mafuta yao wenyewe na wao walikuwa na dhiki kama sisi. Kwa hiyo, na hili tatizo linalozungumzwa la mafuta, ninafikiri taasisi hii tunaweza kupata wataalamu wa masuala hayo. Sambamba na hilo ndio watakao buni zana na vifaa vya kuweza kuchimbia mafuta na wala si lazima zitumike zile za kisasa japo zile za kuanzia.

Mhe. Spika, ukumbi huu kama tunakumbuka kabla haujawa Baraza la Wawakilishi Wachina walionesha mambo mbali mbali likiwemo suala la uchimbaji wa mafuta na aina tofauti walizozitengeneza na waliweza kuzitumia kwa utaalamu wao.

Kwa hivyo, maendeleo yoyote kama sisi wenyewe hatujaanza kujipinda, basi itatuchukua muda mrefu. Kwa maana hiyo, madhumuni ya taasisi hii ninaunga mkono iundwe. Pia ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tuukubali. Kwa kuanzia na fedha hizo kidogo na wenye machozi karibu watatusaidia na hivyo ndivyo nchi nyingi zilivyoweza kuanza. Kwa sababu lazima tuanze na kutia nia, lakini tukeshakutia nia na njia hupatikana na wala halina matatizo.

Kutokana na hali hiyo Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu naomba kwanza tutie nia kwa ajili ya kukiunda chombo hiki, kiweze kufanyakazi ili tupate wataalamu ambao wataisadia nchi hii katika masuala mbali mbali.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo niseme mswada huu unafaa kwenye kazi za Baraza, ninadhani ni kuwaelekeza vizuri wale Wajumbe wetu wa Baraza. Kwa sababu kwanza limezungumzwa suala zima la mitaala, sasa chombo hiki tunachokianzisha lazima kitakuwa kinahitaji malighafi ambayo ni wanafunzi watakaokuwa na sifa kuweza kuingia kwenye chuo na kujipatia elimu.

Wazo langu kuhusu mitaala yetu ya elimu ya msingi ianze kubadilika kidogo kidogo na wakati tunapokuja elimu ya sekondari, basi itanuliwe. Mitaala ya mafunzo ya ufundi itanuliwe, ili wanaomaliza darasa la 12 na 14 waweze kuchukuliwa kwa sifa zao na kuingia katika chuo hiki cha Taasisi ya Karume.

Kwa maana hiyo mitaala ianzie tokea msingi. Hali hii itatusaidia katika kuwajua wenye vipaji, pia taasisi yetu itaweza kupata wanafunzi wenye vipaji ambao hao watakuwa waadilifu kwa mambo mengi makubwa katika taaluma ya kubuni mitambo na masuala mengine.

Mhe. Spika, katika mitaala hiyo tukafikiria yale matatizo yetu, yaani hii elimu ambayo itakayotolewa ya ufundi iweze kutatua matatizo yetu. Kwanza kuwapata walimu wa kutosha wa ufundi, kwa sababu tunakokwenda lazima elimu hii ienee mpaka vijijini. Kama nilivyosema kwamba elimu hii isomeshwe katika skuli za sekondari pamoja na msingi, kwa hiyo ni lazima tuhakikishe chuo hiki kinatoa watalamu wa kutosha wa fani hii ya ufundi.

Suala la jengine ni kutoa mafunzo ya kupata wataalamu wa kuweza kuunda vyombo vya kutumia wenyewe, yaani wabunifu wa viwanda vidogo vidogo kama nilivyovitaja mwanzo Mhe. Spika. Kwa mfano, viwanda vya usindikaji, usagaji nafaka pamoja na matunda.

Sambamba na hilo kwa kuwa miongoni mwa shughuli zetu katika visiwa vya Unguja na Pemba ni uvuvi, hivyo ni vyema wapatikane wataalamu wa kutengeneza marikebu pamoja na boti za uvuvi, ambazo zinaweza kusaidia wavuvi wetu kwa shughuli za kila siku. Vile vile kupunguza gharama za serikali kwa kutoa fedha zake kwenda nje kwa ajili ya kununua boti.

Mhe. Spika, ninahakika kuwa wataalamu wetu watabuni boti zitakazoweza kuhimili mazingira ya bahari yetu, ambazo zitakazotumiwa vizuri na wananchi wa visiwa hivi.

Nikiendelea na mchango wangu sina pingamizi na suala zima la utawala, baraza na hata bodi. Napenda kusisitiza kuhusu hawa wataalamu wetu ambao watakuwa ndio wafundishaji na kwa sababu chuo tunataka kifanikiwe, basi maslahi yao yawe ya kuvutia pamoja na wale watakaohitimu kuijua hatma, kwa maana hiyo wanafunzi wengi watapenda kwenda kwenye taaluma hii.

Mhe. Spika, limezungumzwa kuhusu suala la majengo. Kweli lakini mtu huanza na pahala pale aliponapo. Wakati tulipokuwa wadogo tukisoma Quraan chini ya mwembe na waliosoma hivi sasa wengine ni Makadh wa nchi hii. Kwa hivyo, suala la majengo ni kweli, lakini lisituzuie sisi kuukataa mswada huu kwa sababu majengo yetu hayana hadhi hiyo.

Jambo la msingi ni kuwa napo wanafunzi watakuwa wanasoma na wala siku za mvua hawavujiwi nafasi ya kufanyia mazoezi ipi. Mhe. Spika, ninawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu tuukubali mswada huu na serikali kwa upande wake kidogo kidogo kadri ya uwezo wa kifedha utakavyoruhusu majengo hayo yatatanuliwa mpaka yafikie hadhi ya majengo ya vyuo vya kisasa au yanayokubalika.

Vile vile niunge mkono wajumbe waliozungumzia kuhusu suala la vifaa. Kwa sababu matarajio yangu mengi kwenye taasisi hii tutapata wataalamu. Kwa hivyo, wakati wa mafunzo vipatikane vifaa vya kweli ambavyo vitasaidia katika masomo ya vitendo, ili wanapomaliza pale mimi nijue kwa hakika mtaalamu nikimwita na kumwambia leo nataka unifanyie kiwanda kidogo cha kuhifadhia embe, awe na uwezo huo.

Kwa sababu vifaa alikuwa navyo na atakuwa ameshafanya mazoezi ya kutosha na anaporudi katika jamii, basi atakuwa na uwezo kamili wa kutengeneza kitu kamili ambacho kitakuwa kinahitajika.

Mhe. Spika, mimi sikuwa na mengi lengo langu ni kuunga mkono mswada huu. Kwa hivyo, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Koani ninakubaliana na wazo la Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali la kuletwa mswada

huu mbele ya Baraza lako tukufu, ili mswada huu uwe sheria na kuweza kuanzishwa chuo hiki. Sisi hatuna shaka na tunakubaliana na suala hilo na tunaunga mkono ahsante sana.

**Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja:** Mhe. Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mawazo yangu kidogo tu kwenye mswada huu. Kwanza napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kufikiria jambo zuri la kuweza kumuenzi Marehemu Mzee Abeid Amani Karume.

Kwa sababu tulipitisha sheria hapa ya Kuwaenzi Viongozi waliopita, sasa hii imenipa faraja kuona kutoka kwenye Chuo cha Karume na hivi sasa tunaingia katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknologia. Kwa kweli hii ni njia nzuri ya kumuenzi Mzee Karume ninawapongeza sana.

Mhe. Spika, nilikuwa nikisikiliza majadiliano mbali mbali yaliyokuwa yakiendelea hapa, ambapo wajumbe wengi walionesha wasi wasi kwamba hatuna majengo ya kutosha kwa kuanzisha taasisi. Ninasema tusiogope katika kuanzisha kitu chochote.

Kwa mfano, hapa tulipo leo hii ilikuwa Club tu ya matajiri kabla ya Mapinduzi walikuwa wakija hapa kustarehe. Baada ya Mapinduzi ikaitwa *Peoples Club,* ilikuwa tunakuja kupiga *dance* na wakati ule kulikuwa na ile aina ya mchezo wa *Twist*, yaani wenyewe tulikuwa tunakuja ku-*twist* hapa.

Lakini kwenye miaka ya 1986 ambapo Baraza la Wawakilishi limeshaanzisha na linatafuta sehemu ya kufanyia kazi zake ikaonekana hapa panafaa na mpaka leo tupo hapa miaka 29 na hivi sasa tunafikiri kujenga jengine sijui kama tutaliwahi sisi tuliomo humu. Lakini tayari limeshaanzishwa na ndio mambo yanavyokwenda.

Tukiangalia mfano mwengine tumeanzisha *SUZA* katika majengo mbali mbali. Lakini katika majengo yale tayari watu wameshasoma na wenye kupata vyeti vyao wameshapata, wenye kupata kazi wameshapata na bado yanaendelea na hivi sasa tumeona kuna eneo Tunguu, basi waanze kujenga na harakati za kupima zimeshaanza na huko tayari tumeshaanza.

Kwa hivyo, tusiopoge katika kuanzisha taasisi hizi za elimu kwa kuhofia labda hatuna maeneo ya kuanzia. Kwa kuanzia eneo la Chuo cha Karume ni zuri sana wanaweza kuanzisha pale kwa majengo yaliyokuwepo na baadaye yakaendelea sehemu nyengine.

Mhe. Spika, teknologia tunaihitaji sana katika nchi yetu na lazima tusomeshe watoto wetu. Kwa kweli viongozi wetu wanapokwenda nje ya nchi kwa ajili ya kuomba wataalamu wakati mwengine huwa wanaona haja. Maana huambiwa hivi sasa ni miaka 45 tokea Mapinduzi mpaka leo bado hamjakuwa na wataalamu tu.

Mfano mzuri Marekani alipoombwa atusaidie walimu wa sayansi alisema mimi sikuleteeni walimu wa kuja kufundisha madarasani. Isipokuwa nitakuleteeni walimu wa kuwasomesha walimu wenu halafu wao ndio wasomeshe. Sasa kama hatuna taasisi hizi, basi tatizo tutakuwa tunaendelea nalo la upungufu wa wataalamu.

Mhe. Spika, teknologia ina maana pana sana. Niliwahi kusoma kitabu kimoja, kuna mtu mmoja alivumbua nimesahau sijui kitu gani akafanyiwa *party* kubwa. Sasa kuna watu wengine wakawa wanaponda kwa nini kafanyiwa pati kubwa kwa kuvumbua kitu kidogo kama hiki, Yeye mwenyewe akasikia, basi siku ya pati ile alikwenda na yai, akasema kuna watu wamesema nilichovumbua ni kidogo haifai kufanyiwa pati kubwa kama hii. Sasa mimi nakupeni yai hili nataka mtu alisimamishe lisilale lisimame, limezunguka meza yote mpaka mwisho limemfikia mwenyewe hakuna aliyeweza kulisimamisha akasimama akasema mmeshindwa nyote kulisimamisha, basi sasa nitalisimamisha mie, akachukua kijiko akaligonga kule chini kidogo akalisimamisha likasimama, kila mmoja anasema na mimi naweza anaambiwa si limefika kwako hukufanya, sasa hiyo ndio aliyotumia ambayo wengine imewashinda.

Mhe. Spika, mimi jana nilikuwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete akanambia kule Morogoro hivi sasa kwenye hii migomba wana teknolojia nyengine. Anasema ule mkungu wa ndizi unaweza kufika kimo kama chako, sasa kwa kuwa tulikwenda kule Makunduchi akaona ile migomba akaahidi atatuletea wale wataalam waje watusaidie. Kwa hivyo, lile shamba lako la Mzuri kule Mhe. Spika, liweke vizuri utapata wataalam wa kufundisha uzalishe ndizi kubwa sana.

Lakini sasa nije kwenye mswada kifungu cha kwanza tu hapa mimi kidogo nataka Mhe. Waziri aniwekee vizuri, sijakifahamu vizuri na haya makaratasi yanaumiza macho.

Kifungu cha 1 kinasema.

" *Sheria hii itajulikana kama Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia ya 2008 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri kwa kutoa tangazo katika Gazeti atachagua".*

Mimi hapa atachagua sijafahamu, atachagua gazeti la Zanzibar leo, Nipashe au vipi au baada ya kutiwa saini na Rais ndio atatangaza, sasa hii atachagua mimi imenichanganya changanya sijaifahamu vizuri. Namuomba hapa kidogo aje anifahamishe.

Lakini jengine kifungu cha 19 kinasema.

"*Baraza linaweza kutunga sheria ndogo ndogo ili kuhakikisha nidhamu miongoni mwa wanafunzi na wafanyakazi".*

Halafu huku zimetajwa adhabu pamoja na kila kitu, lakini kilichonitia mashaka chengine anasema hakutakuwa na ulazima wa kutangaza kwenye gazeti sheria ndogo ndogo zilizotungwa na kila sheria ndogo itawasilishwa kwa wanafunzi au wafanyakazi kwa njia ambazo baraza litaamua. Sasa kwa nini sheria zisitangazwe ziwe siri.

Lakini katika kifungu cha 23(2) kinasema.

*"Kanuni zilizotungwa chini ya kifungu hiki zitatangazwa katika gazeti rasmi la serikali".*

Sheria hazitangazwi, lakini kanuni zitatangazwa, sasa hapa sijafahamu. Lakini pia katika kutunga hizi sheria wasi wasi wangu sijui kwa mujibu wa katiba sheria zote si zinatungwa kwenye Baraza la Wawakilishi, au taasisi nyengine zinatunga sheria ndogo ndogo, lakini ukimpa mtu nafasi ya kutunga sheria ndogo baadae atatunga kubwa halafu. Sasa nafikiri hapa kwenye sheria Mhe. Waziri angetuwekea wazi.

Lakini jengine ambalo nimeliona lipo hapa kwenye kifungu cha 21 (5).

Kifungu cha 21 (5) kinasema.

*"Uamuzi wa Baraza chini ya kifungu hiki utakuwa wa mwisho".*

Mhe. Spika, tuna Mahakama ya mwanzo, tuna mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Mkoa mpaka Mahakama kuu, lakini hawa wa nidhamu tu wao ndio wanaweza kumuadhibu mwanafunzi au mfanyakazi, rufaa wanaweza kukata kwenye baraza hakuna baada ya hapo imekwisha. Nafikiri hapa wangeongeza angalau na Waziri akapata nafasi nae kuwa muamuzi wa mwisho baada ya baraza. Panaweza kutumika mambo mengine hapa ya kumuonea mtu kwa sababu hao nidhamu na hilo baraza ndio hao kwa hao, sasa pangeongezwa kipengele cha Waziri akawa muamuzi wa mwisho, isiwe uamuzi wa baraza ndio wa mwisho. Hapo tutakuwa waziri tumempa nafasi ya kutizama hasa hizo

adhabu zilizotolewa na kama mtu kaonewa, pengine mtu anaweza kuonewa kisiasa tu hapo, sasa tukimpa nafasi waziri anaweza kusaidia hapo katika kuweka mambo vizuri.

Mimi nasema huu mswada ni mzuri wa kumtukuza Marehemu Mzee Karume mimi naukubali mia kwa mia sina pingamizi nao. Ahsante.

**Mhe. Omar Ali Jadi:** Mhe. Spika, sina budi kukushukuru na mimi kunipatia nafasi hii ili kutoa mawazo yangu katika mswada huu wa kuanzisha taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia, niungane na wenzangu kumshukuru Mungu, pili nikushukuru wewe binafsi. La tatu, nianze katika mswada huu ambao nitazungumza machache.

Mhe. Spika, kila kitu kina wakati na si kweli kama kilichokuja leo kimepitwa na wakati na kinachokuja kesho kimeshindwa kutangulia na wakati, isipokuwa utendaji ndio kuwa unapaswa kulaumiwa, Tumeyapanga mengi, lakini kutekelezwa yameshindikana kwa ukosefu wa fedha na bila ya kupata fedha hatuwezi kufanya jambo lolote la kimaendeleo. Wazee wa zamani walisema kwenda ni hatua moja na kusema ni mipango, tunajitahidi mawaziri wetu wanatafuta na kutathmini kuleta maendeleo, lakini hatima yake wanakwama njiani kutokana na fedha.

Sasa ingekuwa ni vyema tukakipanga kitu kidogo, lakini tukakihitimisha kwa ule wakati ambaokuwa tumeupangia. tumeanzisha vyuo vingi, tumeanzisha taasisi nyingi, lakini hatua za kimaendeleo bado zimekwama kutokana na ukosefu wa fedha. Yote haya tunayapanga kwa kutegemea maendeleo au misaada kutoka nje na wahisani. Wahisani ni watu, wana hiyari yao, wahisani ni watu wanaochekecha mambo yao, akija atakupangia mengi, lakini kutekeleza kwake kunashindwa halafu alete lawama kunako wahusika. Watu wengi wanasema waziri akishapanga ndio atatekeleza tu, kumbe anapanga kwa kutafuta nyenzo za kuendeleza, sidhani mtu kama Mhe. Harouna Ali Suleiman alipange jambo halafu alione linafeli yeye mwenyewe anajisikia aibu, lakini afanye nini.

Mfano mmoja hai kabisa nitautoa katika bajeti yake kaja kachambua sana na moja alilofanikisha, kasema hata jimbo la Kojani atajenga chuo cha walimu, nina imani mipango yake mizuri, lakini fedha za kumwezesha hana afanye nini. Sasa kwa sababu Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha hayupo, Waziri Kiongozi anasikia.

Tunaiomba serikali wakati tunapopanga majukumu kama haya ya kimaendeleo, basi yawe yana kasma maalum ya dharura, ili tufanikishe malengo na mawaziri wasipate kubweteka wakaona nimepanga jambo la maendeleo, lakini halafu

yake limekwama. Tuwe na fedha maalum za dharura ambazo kuwa zinahitaji taasisi kama hivi ziwezeshwe ili zifanye kazi. Mimi nina imani kubwa kuwa tulikotoka nyuma miaka sitini, sitini na nne, sabiini mpaka leo, tumepiga hatua tukitaka tusitake, kwenda sio kusimama, tunakwenda japo polepole. Lakini kwenda huko sasa kunataka kufanyiwa tathmini, tulikotoka, tulipo na tunapokwenda. Nina imani Zanzibar miaka ya sabiini, Baraza la Wawakilishi likuwa na watu waliokuwa na elimu ya Form IV wachache, sio Diploma wala Digree. Nasema waliokuwa na Form IV, lakini leo tuna mainjinia wengi tu, ni maendeleo na hatua kubwa.

Ili tufanikishe maendeleo haya na nina imani wataalam tunao wa kutosha, miaka hiyo kulikuwa hakuna watu wenye Degree, lakini leo tunaweza kujinata mbele ya nchi za wenzetu, tuna Madaktari na Maprofesa, japokuwa bado ni wachache. Lakini wenye vyeti vya Master wanafika si chini ya mia moja, mfano ulio hai kama kisiwa changu cha Kojani sasa hivi sikosi vijana watatu mpaka wanne ambao kuwa wanachukua master, mwaka huu wanamaliza. Hiyo ni hatua ya maendeleo sisemi majimbo mengine ambayokuwa yamepata mwamko mapema.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ningeishauri serikali tukawatumia watalam wetu wakaendeleza vyuo vyetu kwa kuwezeshwa, bila ya kuwezeshwa tutalaumu kwamba wataalam hatuna, kumbe wataalam tunawatumia vyengine na vile wanavyotaka wao, tungepanga siku tukawasikiliza wataalam, tukawauliza mahitaji yao nini, kelele zao nini. Lakini yote hayo yanakosekana kutokana na nyenzo kuwa hawana, kuwezeshwa ni kufupi, vijana wetu wengi ambaokuwa wamechukua vyeti hivi karibuni wako Dar es Salaam wanasomesha, wengine wanaajiriwa katika mahospitali ya binafsi kwa sababu ya kuwezeshwa kwao ni kufupi na hiki ndio kilio kikubwa kwa wafanyakazi wote au kwa sekta zote za serikali.

Mhe. Spika, bila ya kupanga na bila ya kuweka hakiba hatuwezi kuwapata wataalam , kuna hadithi moja nilikaa na bibi yangu wakati huo mdogo akasema leo nataka nikupe ulimwengu unaokuja, mkija mkichagua wake kuna wake mafungu manne.

Fungu la kwanza atakuwa ni mke mame nisikilizeni vizuri. Akasema Mke mame imani yake unakwenda na kipande cha nazi, basi kile kipande kimoja atakikuna mpaka atabakisha, kipande atakificha wewe mume hujui. Utakwenda na dagaa lako kifungu kimoja hakitoshelezi, lakini kwa hali ilivyo atalikasimu na kulichemsha halafu analiweka pembeni nusu analipika. Siku ya pili baba anaingia nyumbani na kutoka hajui afanye nini, nazi hana na dagaa hana, mhogo umeshakuja halafu akiona jua linatua unamuona mke anahangaika. Kwa

sababu alijua uzoefu na matatizo yaliyopo pale nyumbani ya uwezeshaji, kwa hivyo anamsaidia mume siku ile kupata huyo ndio mke mame.

Mke wa pili kasema ni mke mwenye huruma tu na imani ukienda na nazi moja yote ataipikia, hakulazimishi uje na ya pili, lakini ile moja haibakishi ataipikia huyo ni mke mwenye huruma na imani.

Mke wa tatu kasema huyu ni shupa ya ukwake, nazi moja haimtoshi, ukitoka anatoka, mke wa tatu huyo.

Mke wa nne kasema ni shupa kupwa ya kungena, maana huyo humuwezi kwa tabia yoyote *(Kicheko)*, ukivaa kofia yeye atataka apate shore, ukivaa seruni yeye atataka uvae jinzi. Anasema huyo hata ufanye vipi humwezi, hizo ni tabia ambazo zilikuwa zinajengeka huko nyuma.

Mhe. Spika, sasa maana yangu serikali yetu iwe mke mame nifahamuni vizuri tulichokuwa nacho ni kidogo, lakini tukigawe kwa udogo wake, tusikitumie kwa mara moja kwa kutegemea wahisani. Kila siku tutapanga mambo yetu hayafiki tupendapo. Tukiwa na tamia ya shupa nkungena na shupa nkwake, nina imani hatutojua tunakwenda wapi, tunakotoka ni wapi hatukujui. Kwa hivyo, nasema tujenge tabia kama hizi tufuate wasia na ushauri wa wazazi, kile kidogo tunachokipata katika bajeti yetu kwa makusudi tuweke mfuko wa dharura wa kukumbuka kama kutakuja hili na lile, leo tayari imekuja taasisi ya elimu hii tunataka kuenzi viongozi wetu wa kitaifa ambao kuwa walipigania nchi hii kuwezeshwa hakuna.

Hivyo tunategemea nani atakuja kuwezesha taasisi hizi, wenzetu Bara juzi walianzisha taasisi ya Mwalimu Nyerere, hivyo wanavyoienzi usiombe mchango siku kwa siku na kila baada ya miezi maandamo, kuiwezesha taasisi ile, ili kuenzi kumbu kumbu za viongozi wetu wa kitaifa. Kwa hivyo na hili nina imani kwa sababu nia ni njema tungeliishia vizuri tukafanya taratibu, ili tukaliwezesha na vijana wetu wakaweza kusoma vizuri na hatimae kupata maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, wakati wa bajeti ulisema kama Wizara hii tukitaka tusitake iwe ni wizara mama tulisema kilimo, lakini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndio mama na ndio baba hiyo hiyo. Hii ndio inayotoa wataalam katika fani mbali mbali, huwezi kuunda Wizara ya Kilimo kama huna wataalam kwanza. Huwezi kuunda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kama hujapata wataalam waliosoma katika wizara hii. Huwezi kupata injinia wazuri kama hujapata watu waliosoma wizara hii. Huwezi kubwetesha ukitaka usitake. Wewe na usiite kama wizara mama ukaita na jina wizara baba, lakini inaitika hiyo.

Mhe. Spika, sasa kwa sababu madhumuni ya mswada huu umeeleweka na umejigawa vifungu 23 na ina sehemu tano, kama ilivyotajwa katika mswada huu na madhumuni yake basi ni vyema Mhe. Waziri na kwa sababu anajitahidi kutafuta, hii bajeti ya mwaka huu nafikiri tunaweza kumchochea kidogo tu kwa sababu itakuwa ni mapema, huwezi kumpa mke mtu leo keshokutwa ukamuuliza mtoto yuko wapi wakati umempa mke mwezi mmoja.

Lakini bajeti ya mwaka 2010 tukitaka kuhitimisha huko mbele tutauliza hatima na maendeleo ya taasisi hii wapi tumefikia, isije kuwa kama taasisi nyengine au vyuo vyengine tulivyovianzisha tumevianzisha, lakini hatujui vimefikia wapi. Tumeanzisha Chuo cha kilimo hapa karibuni tena kwa furaha kubwa sana, lakini mpaka leo taarifa za kimaendeleo kwamba kinaendelea vipi hatujapata na ndicho tulichotegemea kisaidie wakulima wetu na wataalam kueneza taarifa vijijini. Lakini mpaka leo taarifa zake hatujazipata.

Mhe. Spika, kwa hivyo tunamwomba Mhe. Waziri kwa jitihada zake zote kama vitabu vilivyosema, ukijitahidi na Mungu anakupa nguvu na ukijitahidi Mungu anakupa bahati, sasa na Waziri ajitahidi na inshaala Mungu atampa nguvu afanikishe malengo.

Lakini sasa nataka niulize suala moja tu na nina imani mwenzangu ameliuliza lakini kwa utaalam wake, katika hii bodi tumeambiwa wajumbe watakuwa ni kama wafuatavyo:-

Kamtaja Mwenyekiti, akamtaja Mkurugenzi ataingia kwa nafasi yake, lakini hakutajwa kwamba atateuliwa na nani labda iwe sikusoma vizuri au sikuiona, Mwenyekiti katajwa ni Rais, lakini Mkurugenzi sikumuona pale sijui *paper* yangu imekosewa kuandikwa za wenzangu zimeandikwa vizuri au pengine zimekosewa zote, hilo nilikuwa nataka niwekwe sawa.

Lakini la pili katika hilo la wajumbe, alisema ni watano watakaochaguliwa na Waziri baada ya kuzungumza na taasisi husika, lakini Mhe. Spika, Mhe. Abdalla Juma kasema labda ni herufi za kirumi, mimi niseme labda za Kichina baada ya watano kuna sehemu nane zilizotajwa, katika wajumbe wale watano ukiacha Mwenyekiti na Mkurugenzi, kuna na watu wanane. Sasa hao watatu sijui watateuliwa na nani, wawili tumeshapewa nafasi yake tutajua hilo, watano ni Waziri sasa watatu sijui atawateua nani? Hilo mimi naomba lipatiwe ufafanuzi.

Halafu la mwisho Mhe. Spika, taasisi na watu wametaja vyuo kutokana na elimu mbali mbali ambazo zitasomeshwa, lakini naona elimu moja na ambayo kuwa ni vigezo kote duniani ni historia. Ninavyokumbuka mimi historia ni vigezo hata vya mwanafunzi wa dini ya kiislaam, hata kwa mtoto nyumbani ni

kigezo cha kumwelimisha ukoo wake ulivyotoka ili kujua alipo na anapokwenda ni wapi. Sasa historia tunaiwacha tusomesheni yote hayo kwa sababu ni maendeleo. Lakini tukumbuke na historia ili kizazi kinachokuja kijue kilitokea wapi mwanzo, kilipofikia ni wapi na kinakokwenda ni wapi, ndio tutaipata elimu iliyo bora vyenginevyo tukiacha historia yetu basi tunakwenda ovyo.

Mhe. Spika, mimi hapo nyuma nilipokumbuka ni karibu sana, lakini wakati zinaanza kuja skuli kule kwetu basi kulikuwa watu wanafuatwa nyumba kwa nyumba wakasomeshwe, basi alfajiri watoto wanakimbizwa na baba zao wanaambiwa kimbieni kwa sababu mnakuja kuandikishwa skuli, na haifai kusoma. Bahati nzuri kulikuwa na wazazi wanaelimika na dunia inayokuja, lakini kulikuwa na wengine hawafahamu wanakotoka na walipo na wanapokwenda na hatimae ndio ukaona vijiji vingi vilinyimika wataalam hapo nyuma, sasa ndio wanaanza kujinyanyua.

Kwa hivyo tukisema tunaiwacha historia, basi malengo yetu tutafikia lakini itakuwa adhima ya fungu la nyuma halipo na huwezi kuanza fungu kabla hujapata mgao sahihi wa pale unapotokea. Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, kwa sababu waziri ni mtu ambae hadhi yake ni kubwa katika kuendeleza nchi hii, historia aipe kipaumbele, ili kujua Mzanzibari alikotoka, walipo sasa hivi na wanapokokwenda ni wapi.

Mhe. Spika, kwa hayo machache kwa sababu nilisema sina mchango mkubwa, halafu kwa sababu Mhe. Harouna ni rafiki yangu mkubwa mpenzi huona kama sijatia kauli yangu itakuwa hafurahi roho yake, imani yangu ni kwamba bajeti inakaribia tena ingawa si mjumbe wa kamati yake, lakini waliopo watafanya kazi nao na kwa lengo lile lile la kimaendeleo. Lakini namkumbusha bajeti iko karibu sijaona hata *foundation* ya chuo changu. Naomba ajitahidi chuo cha walimu jimbo la Kojani. Ajitahidi tushirikiane pamoja japo gari moja la maji nitampa, lakini watu wakute japo dalili.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Spika,** *message* imefika.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kuwepo hapa tukajadili maendeleo ya nchi, pili nimshukuru Mhe. Waziri kwa busara zake za kuendeleza nchi kwa kuleta mswada huu wa Kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia.

Mhe. Spika, kwa michango ya asubuhi mimi nilitishika sana, lakini nilikuwa natishika halafu najiuliza wale waliowasomesha wale mahodari na wakahitimu,

sasa sijui mtu baada ya kuhitimu si anakuwa anasomesha na wenzake, nahisi wale mahodari wakati wamesomeshwa wakahitimu na wakasomesha wengine bila ya shaka kuanzishwa kwa taasisi hii sio kitu cha kutisha, nasema taasisi ianzishwe na Mwenyezi Mungu akitaka tutafanikiwa.

Mhe. Spika, kaba ya Mapinduzi wakoloni walikuwa wana mambo ya hekma ya kuwafanya Waafrika wasiendelee, maana wanatwambia ukisoma kizungu utamtukana Mungu halafu utatiwa motoni, kwa hivyo sisi tulikuwa tukikaa vichakani hatukwenda kwa sababu tulikuwa tukiliogopa hilo. Lakini baada ya muda wazee wakaelimisha watu ili waone kwamba kusoma kizungu sio kumtukana Mungu na wala huingii peponi na kweli. Sasa na sisi tusione kwamba tunapoanzisha taasisi hii tunaweza tukawa na mzigo mkubwa, tukashindwa kufanya mambo mengine. Kitu cha msingi wakati nia hiyo umeshaitia watu wapo, ardhi ya kujenga majengo ipo, wanafunzi wa kusoma wapo. Hoja kubwa kama walivyozungumza wajumbe wengine, ni kusomesha msingi wa mambo ya sayansi.

Kwa kweli sayansi ilianza kusomeshwa zamani, lakini sio ile ambayo tunaitaka sasa hivi. Teknolojia ukimuuliza mtu kwa hafla nini teknolojia, hawezi kujua. Lakini mambo ya teknolojia watu wanayajua, mambo ya sayansi kwa hafla kama mtu hajasoma sayansi yenyewe kila mtu atatafsiri vyake. Lakini bila ya kusomeshwa sayansi ipo kwa sababu watu ni mafundi na Wazanzibari wana vichwa vya kusomea kila kitu.

Namkumbuka shehe mmoja anavyofanya mahesabu yake ya sayansi akakwambia mwezi 29 utavuka saa ngapi, pahala fulani utaonekana na sehemu fulani hauonekani sasa hii yote ni mambo ya sayansi, lakini usome kwa undani. Sasa mimi naamini kwamba wanasayansi wapo mradi tu waangaliwe na tutakuwa tunakosea vimoja tu, yale masomo ambayo yanatakiwa yawemo ndani ya nchi tusianzishe juu moja kwa moja, lazima tuwe na maandalizi yake ujue nataka kutengeneza madarasa ya sayansi mwaka 2020, unaandaa leo. Unajua hawa wana unawapa *toys* wanachezea unajua huyu ana fani hii na huyu ana fani hii.

Lakini tukianza juu moja kwa moja tunaweza kupata tabu sana kuandaa watu wa sayansi na hii sayansi tunayokusudia sio kwamba tunaanza mwaka 2009 tunamalizia mwaka 2010 hamna, sisi tunaanzisha taasisi ya sayansi tunawategemea hao wajukuu zetu waje wafaidike zaidi, kwa sababu wakati huo ndio kutakuwa na ushindani wa soko, maandalizi ya ushindani wa soko kwa mambo ya sayansi na teknolojia, lakini waki huo ndio wakati wenyewe hasa. Tutizame hivi sasa ndio hatua za mwanzo mwanzo katika mambo ambayo tunahojiwa, uwe una taaluma ya kompyuta, sio kiwango kikubwa lakini watu wengi unaweza ukawakosa na wana fani lakini watakosa kwa sababu

hawakupata maandalizi ya taaluma ile. Kwa hivyo Mheshimiwa naomba hiki chuo tuanzishe, tuende pole pole mpaka tufike kule kunakokusudiwa.

Mhe. Spika, mambo mengi tunayoyaanzisha tusiseme kwamba hatujapiga hatua,. tunapiga lakini hatuzioni kwa sababu kila mtu anapata nafasi ya kulifanyia tathmini yake yeye mwenyewe. Nitatoa mfano Chuo cha Mikunguni na Kengeja. Nchi imefanikiwa kweli kweli kwa chuo kile. Nitaulizwa kwa vipi? Ukitaka kipimo kila Jumatano na Jumapili nenda mnadani ukatizame fenisha zote zinazofika pale zinatengenezwa Zanzibar. Miaka ya nyumba hakuna mambo kama hayo. Sasa sijui mafanikio tunayoyatafuta ni yepi. Hivi vitu vizuri vyote wataalamu wake wanatoka hapa. Lakini pamoja na hayo kama walivyopendekeza wenzangu kwamba ipo haja ya kuwatafutia vifaa vya kuwawezesha ili wawe wataalamu zaidi badala ya kutumia misumari tutumie gundi na mambo mengine, ili meza ziwe nzuri na hazichuni. Tunapiga hatua na hakuna lisilo wezekana.

Mhe. Spika, katika taasisi hii ya sayansi na teknolojia nashindwa kuelewa tunachokitafuta kipi. Nitatoa mfano, unapotaka kujua sayansi inayohitajika kwa ghafla huwezi ukaijua. Mhe. Haroun mimi nikuulize tunahitaji sayansi ya kutengeneza vitu au tunahitaji sayansi ya kutumia vitu ambavyo vinakuja katika nchi yetu na sehemu nyengine tunazokwenda. Maana kama tunataka sayansi ya kutengeneza vitu kuna baadhi ya malighafi Zanzibar hakuna. Sasa kama sanyansi ya nadharia kama wanavyozungumza wenzangu basi hatupati tabu sana.  Kwa sababu maarifa ya kuitumia yapo. Lakini kama ni sayansi ya vitendo ya kuwa tunahitaji kutengeneza vitu vya sayansi, basi tutakula gharama kubwa maana itabidi malighafi tuagize nje na kama tulivyozungumza uchumi wetu sio mkubwa sana. Ipo haja ya kutaka kuona tafsiri ya kifungu hiki tunachokikusudia.

Mhe. Spika, chengine nilichotaka kuzungumza ni kweli tunapoanzisha taasisi ni vyema sifa kubwa kuziendeleza. Tunapoanzisha taasisi ni vizuri tuunganishe kuliko kuziondoa kabisa au tuzitenge maeneo mengine. Taasisi nyengine zimekuja kutokana na kumbukumbu ya wale watu ambao wameanza kutuamsha kama zilivyozungumzwa. Kama tunahitaji kuanzisha taasisi mpya, basi ni kweli tujiandae tutafute maeneo na tuoneshe kwamba taasisi hii ni mpya na italeta sifa kwa mtu ambaye ataanzisha pale. Hata wewe Mhe. Waziri ipo haja uanzishe taasisi moja iwe kwa jina lako. Kama walivyozungumza kwamba katika nchi hii una mchango mkubwa sana. Watu wote wanaamini kwamba mchango wako katika nchi hii ni mkubwa.

Mnamo miaka ya 1970, mahitaji ya Wizara ya Elimu yalikuwa yana tabu zaidi kuliko miaka hii ya 2007/2008. Kwa kweli umewapunguzia wananchi mzigo na umewatoa wasi wasi mkubwa. Zamani wazee wakihamasika wakitaka kujenga

shule, basi wanaweza wakakwama katika maeneo mengine kwa muda mkubwa, sasa hivi tunashukuru.

Mhe. Spika, sasa hivi tunapiga hatua katika mambo ambayo tunayapanga tofauti na vile ambavyo tunalalamika tu. Mfano Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka, hapo nyuma tulikuwa tuna tatizo kubwa sana la wahasibu na pesa zilikuwa zinapotea ovyo. Baada ya kujengwa chuo kile kikafanya kazi zake kwa vipindi. Tunashukuru, sasa hivi kimeondoa tatizo la wahasibu, wala hatuagizi nje, akiagizwa nje labda ndugu yetu kaondoka zamani. Kwa juhudi za serikali tumo kuondoa matatizo kidogo kidogo. Chuo kile hivi sasa kimepiga hatua, si ajabu baada ya muda kikafanywa taasisi. Taasisi ni kukuza, lakini maarifa yanayohitajika ndio yale yale na matumizi yake ndio yale yale yanayotumika ndani ya nchi.

Mhe. Waziri, hivi sasa wizara yako inatakiwa ikimbie kweli, ingawa unakimbia lakini uzidi kukimbia kwa sababu mahitaji ya Wazanzibari na hasa mambo ya elimu tunapotoka ni tofauti na sasa tulipo. Sasa hivi tumeongezeka na tunaongezeka kwa njia zote mbili za wageni kuingia, lakini na hata sisi wenyewe ule uzazi wa mpango tunaukimbia sana. Kwa hivyo tunaongezeka kwa idadi kubwa na vyovyote tunavyofanikiwa tunahisi bado hatujafanikiwa kwa sababu tuna mzigo wetu na wa ndugu zetu. Mheshimiwa Waziri unahitajika ukimbie sana ili kupunguza tatizo, Mwenyezi Mungu atakujaalia, kwani yeye humpa cheo yule mwenye imani na watu. Mfano mzuri nimeona juzi unawakabidhi walemavu kina Bi Raya hundi ya shilingi milioni 50, mate yananidondoka. Kutokana na juhudi yako na Mwenyezi Mungu alivyokupangia. Mheshimiwa nakusifu, una mapesa sana sijui kama unatoa wewe au yanatoka wapi.

Mhe. Spika, chengine ninachotaka kuchangia ni ukurasa wa 224 kifungu cha 15, hiki kinazungumzia uwekezaji wa fedha. Unajua fedha za taasisi ni mtego mkubwa, unataka imani na maarifa juu ya uwekezaji wa fedha hizi. Kwa sababu fedha ni kitu fitna na fitna ya fedha hasa inakuja wakati matumizi na mapato yanapokuwa hayatambuliki. Hii mimi bado siafiki kwa utaratibu gani ambapo chuo kinaweza kuekeza au kufanya biashara. Ninahofu bado kitakuwa kichanga, haidhuru kina uwezo wa kukopa na uwezo wa kukopesha, hili ulifikirie sana. Nina wasi wasi, kwamba linaweza likaleta migogoro hasa pale zitakapokuwa fedha zimewekezwa, lakini mahitaji ya matumizi ya chuo yanahitajika na zile fedha zikawa zimekwama. Tatizo hili linaweza likaleta migogoro kwa wanafunzi kwa sababu ni haki yao. Wanaweza wakaonekana kama hawana nidhamu na wakachukuliwa hatua za kinidhamu. Kumbe tatizo limeanza kwenye huu uwekezaji wa fedha. Hili lifanyiwe kazi vizuri sana.

Mhe. Spika, kuna mtu kanambia kwamba mbona taasisi hii bado iko Zanzibar, lakini haina tawi kule Pemba kama vile kilivyo Chuo cha Elimu. Kaninong'oneza lakini hakunituma ni rafiki yangu Omari Ali Jadi. Kwa nini vyuo hivi vyote vinakuwa viko hapa hapa, haidhuru Chuo cha Taasisi cha Karume cha Sayansi na Teknolojia kwamba kimeanzia pale. Wanasema na wao wawe na nafasi ya kuona baadhi ya taasisi ziweko kule, kwa sababu Zanzibar ni Unguja na Pemba. Hilo lilikuwa ni ombi kama unavyojua Mhe. Omari Ali Jadi huwa hadharauliki, kwa hivyo utakavyokuja kutoa ufafanuzi Mhe. Waziri naomba uje umsaidie sana.

Mhe. Spika, chengine ninachotaka kuzungumza ni sehemu ya sheria ndogo ndogo katika kifungu cha 19 sehemu inayosema kwamba,

Kifungu cha 19 "Baraza linaweza kutunga sheria ndogo ndogo ili kuhakikisha nidhamu miongoni mwa wanafunzi na wafanyakazi."

Mhe. Spika, sheria ndogo ndogo ni sheria ambazo zinatungwa ambazo huwa hazipitii katika Baraza la Wawakilishi. Sheria hii inapitia Baraza la Wawakilishi. Tunahofu kutokana na kwamba inaweza katika sheria ndogo ndogo yakaingia mambo makubwa ambayo yanaweza kukiuka hii sheria mama. Je, Mhe. Waziri likitokea kama hilo unatuhakikishia vipi kwamba sheria hiyo itarejeshwa na itafutwa. Kwa sababu hakuna utaratibu na sijapata kusikia katika mabunge yote kama imeingizwa sheria katika sheria ndogo ndogo na ikazidi au ikasababisha kuharibu madhumuni katika ile sheria ambayo imetungwa. Vipi inaweza ikakataliwa. Tungeomba au tungependekeza Mhe. Spika, akawa na utaratibu wa zile sheria ambazo tunatunga zitakapotungwa sheria ndogo ndogo angalau zile kopi zake tupewe tuzione kwamba hili na hili tumepitisha na hili limo kwenye sheria ndogo haliathiri sheria ambazo zimetungwa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, chengine ni madhumuni na sababu. Naomba kunukuu katika madhumuni na sababu kwenye *paragraph* ya kwanza inasema kwamba,

"Mswada huu unamadhumuni ya kukigeuza Chuo cha Ufundi cha Karume kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknologia ya Karume inayojitegemea kiutawala."

Sasa hii sheria ukiiangalia sana ina nia ya kugeuza. Hapa haikusema kwamba inageuza jina, ina madhumuni ya kugeuza sababu, ina madhumuni ya kugeuza maana. Ina sababu ya kugeuza mantiki ya Chuo cha Karume. Sasa kwa wale watu ambao sasa hivi wapo chuo na wao watageuka kuwa wanachuo cha Sayansi cha Karume au wale wataondokea vipi. Wale kwa mujibu wa sheria hii

inageuza na inapogeuza sina wasi wasi ni kwamba inageuza mambo yote. Hili tungelizingatia sana kwa upana wake, kwa ukubwa wake na hata kwa madhumuni hasa ya Mswada wenyewe. Haikutaja kingine chochote, isipokuwa ina madhumuni ya kugeuza chuo. Mimi si mwana sheria, lakini naona kwamba hii madhumuni na sababu *paragraph* ya mwanzo ingekuzwa ikaonekana hasa kwamba Mswada huu una madhumuni yepi ya kugeuza mantiki au kugeuza jina tu, ili kuona kwamba hivi sasa tunaingia kwenye mambo ya sayanzi na teknolojia.

Mhe. Spika, baada ya hayo, mimi na wananchi wangu, Mswada huu kama utafanya kazi iliyokusudiwa tunauunga mkono mia kwa mia ili na sisi tuingie katika ulimwengu wa Sayansi na Teknolojia. Nakushukuru Mhe. Spika.

*(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 26/01/2009 saa 3:00 asubuhi)*